*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 18 Aprili, 2019

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, leo ni Kikao cha Kumi na Tatu cha Mkutano wetu wa Kumi na Tano, Katibu!

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. ROSE C. TWEVE - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu!

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Mkuu, swali la kwanza linauliza na Mheshimiwa Suzana Chogisasi Mgonukulima.

Na.107

### Karatasi Maalum za Kupigia Kura kwa Ajili ya Walemavu wa Macho

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA** aliuliza:-

Watu wenye ulemavu wa macho wanakosa haki ya kuchagua viongozi wanaowataka kutokana na kusaidiwa kupiga kura na watu wengine ambao wanaweza kuwapigia

kura kinyume na ridhaa zao, hivyo kura zao kwenda kwa watu ambao si chaguo lao:-

Je, Serikali iko tayari kuchapisha karatasi maalum za kupiga kura kwa kutumia mfumo wa nukta nundu kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa macho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mbunge wa hapa tulipo Dodoma.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI,VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suzana Chogisasi Mgonukulima, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 61(3)(b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 na Kifungu cha 62H cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Sura ya 292 vinafafanua kuwa ikiwa Mpiga kura ni mlemavu wa macho au ana ulemavu wa viungo (mfano, ulemavu wa mikono), au hawezi kusoma na kuandika anaweza kumchagua mtu anayemwamini amsaidie kupiga kura. Mtu huyo anapaswa asiwe Msimamizi wa Kituo cha kupigia Kura, Msimamizi Msaidizi wa Kituo au Wakala wa Chama cha Siasa. Aidha, Kanuni ya 53 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2015 na Kanuni ya 46 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za (Madiwani) zimeweka utaratibu kuwa iwapo Mpiga Kura mwenye ulemavu wa macho ataomba kupewa karatasi ya kupigia kura ya nukta nundu *(tactile ballot paper),* Msimamizi wa Kituo atapaswa kumpatia Mpiga Kura karatasi hiyo ili aweze kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, katika Uchaguzi wa mwaka 2015, Tume iliandaa karatasi maalum za kupigia kura kwa mfano wa nukta nundu kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais pekee. Hivyo, katika chaguzi zijazo, Serikali kupitia Tume ya Taifa Uchaguzi, itaandaa karatasi hizo maalum wa kutumia mfumo wa nukta kwa ngazi zote za uchaguzi.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Mgonukulima, uliza swali.

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri nitakuwa na maswali ya nyongeza mawili. Swali la kwanza, kutokana na maelekezo ya kuwa mtu mwenye ulemavu wa macho atamwomba Msimamizi wa Uchaguzi karatasi ya nukta nundu. Je, Serikali imetoa elimu kiwango gani kwa watu wasioona ili wajue wakifika kwenye kituo hicho wamuone huyo mtu atakayetoa karatasi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni miaka 58 ya uhuru wa nchi yetu, ni mwaka 2015 kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyokiri Serikali iliweza kutoa makaratasi ya nukta nundu kwa watu wenye ulemavu wa macho napo kwa kumchagua Rais tu. Je, Serikali haioni haiwatendei haki watu wenye ulemavu wa macho kutokumchagua Mwenyekiti, Diwani na Mbunge hatimaye kupata *set* ya Serikali ambayo anaitarajia imuongoze? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mazuri, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI,VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suzana Mgonukulima, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza la kuhusu elimu kwa watu wenye ulemavu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu kwa pamoja, tutafanya kazi ya kutoa elimu kwa makundi mbalimbali likiwemo kundi hili la watu wenye ulemavu ili waweze kutimiza haki yao ya Kikatiba ya kupiga kura. Hivyo nichukue fursa hii kuwaondoa hofu watu wote wenye ulemavu wa macho, kwamba wakati wa uchaguzi wa mwaka 2020 watapata fursa ya kupiga kura kwa kupata elimu kupitia Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na shirikisho ambao tunafanya nao kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kuhusu haki za watu wenye ulemavu kuwapigia kura wagombea wengine zaidi ya mgombea wa urais. Katika majibu yangu ya msingi nimeeleza kwamba mwaka 2015 ilikuwa ni fursa hiyo tu ya kuweza kumchagua mgombea wa urais, lakini kwa mwaka 2020 nataka nilihakikishie Bunge lako kwamba tunaweka utaratibu mzuri ili pia watu wenye ulemavu wawe na haki ya kuchagua viongozi wote kwa ngazi zote kama majibu yangu ya msingi yalivyosema.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mbunge wa Mgogoni, kwa niaba yake.

Na. 108

**Kujenga Bandari Kubwa - Zanzibar**

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN (K.n.y MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF)** aliuliza:-

Zanzibar kwa namna ilivyo inahitaji uchumi wa Visiwa ambapo Bandari ni kitu cha lazima:-

Je, Serikali ya Muungano inaungaje mkono nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kujenga Bandari kubwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mbunge wa Mgogoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Bandari Na. 17 ya mwaka 2004 (*The Ports Act No. 17*), majukumu ya

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* ni kuendeleza bandari, kuendesha shughuli za bandari, kutangaza huduma za bandari na kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa bandari.

Aidha, Shirika la Bandari Zanzibar *(ZPC)* lilianzishwa kwa Sheria ya Bandari ya mwaka 1997, Sheria hii ilifanyiwa marekebisho mwaka 2013. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, *ZPC* ina majukumu ya kuendeleza bandari, kuendesha shughuli za bandari na kutangaza huduma za bandari ndani na nje ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Nyongeza ya Kwanza imeorodhesha Mambo ya Muungano ambapo kipengele cha 11 katika orodha ya Mambo ya Muungano kinahusu Bandari, mambo yanayohusika na usafirishaji wa anga na posta na simu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo hayo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kushirikiana katika masuala mbalimbali ya uendelezaji wa bandari nchini. Ushirikiano huo umedhihirika zaidi katika kupanga miradi ya kipaumbele na kutafuta fedha za uendeshaji wa miradi hiyo kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Washirika wa Maendeleo. *TPA* na *ZPC* zimeendelea kushirikiana kwa utaalam na kushirikiana katika kutoa huduma za bandari nchini hususan katika uongozi wa meli kutoka nje ya nchi. Aidha, tunaendelea kuboresha ushirikiano kupitia vikao vya mara kwa mara vya Sekta za Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo hayo, Serikali ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikiunga mkono nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kujenga bandari kubwa ili kuimarisha miundombinu na huduma ya bandari nchini.

**SPIKA:** Uliza swali lako, Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri mahiri katika Wizara hii ya Muungano, lakini pamoja na hayo nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; bandari hiyo ambayo inatakiwa ijengwe Zanzibar pale Mpigaduru ina thamani au itagharimu dola za Kimarekani milioni 430, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshapata mdhamini au mkopo kutoka *Exam Bank* wa dola milioni 200, ni miaka nane sasa tokea mradi huu upite, Serikali ya Muungano imeisaidiaje Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupata mikopo au msahada wa kumalizia hapo palipobaki ikajengwa gati hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu Serikali ya Muungano imeingia mkataba wa kujenga gati ya Bagamoyo na Oman ndiyo wafadhili wa gati hii, lakini mkataba ule unaizuia Oman kusaidia tena nchi yoyote ya Afrika Mashariki kwa mujibu wa kilometa zilizowekwa kujengwa gati kama ile.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba mkataba huu ndiyo ulioifanya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikose msaada kutoka Oman kwa ajili ya kujenga gati ile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimekuwa katika mazungumzo na mazungumzo hayo yanaelekea ukingoni kuhusu kukamilisha kipande cha rasilimali zinazotakiwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Mpigaduru. Tunafahamu kwamba ni moja ya ahadi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM na ni bandari muhimu sana kwa uchumi wa Zanzibar na wote tunajua hivyo na tunafahamu hali ya bandari ya Zanzibar, sasa hivi ilivyo na msongamano. Kwa hiyo tunazungumza na wenzetu kuhakikisha kwamba tunafanikiwa katika hilo.

Mheshimiwa Spika, la pili, mkakataba wa ujenzi wa bandari ya Bagamoyo bado haujaingiwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kampuni ya China kwa kushirikiana na Oman. Kwa hiyo yale masharti yaliyopo yanayozungumzwa hayatumiki sasa kwa sababu bado utekelezaji rasmi haujaanza. Hata hivyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wazanzibari wote kwamba Serikali haitaingia katika maamuzi ambayo yataathiri ustawi na uchumi wa Zanzibar. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Martha Mosses Mlata na kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Ritta.

Na. 109

**Sherehe za Muungano Kufanyika Kitaifa**

**MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MHE. MARTHA M. MLATA)** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Sherehe za Muungano zimekuwa zikifanyika na kupewa nafasi kubwa Kitaifa tu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, tafadhali

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Singida, kama ifuatavyo-

Mheshimiwa Spika, Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar huazimishwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa wa mwaka 2011 uliotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ndiyo

ina dhamana ya kuratibu sherehe zote za Kitaifa. Aidha, katika Mwongozo huo, Sura ya Tano katika maelezo ya Utangulizi imeelezwa kuwa "Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar zitafanyika tarehe 26 Aprili ya kila mwaka katika uwanja wa Uhuru, Dar es Salam mahali ambapo udongo wa Tanganyika na Zanzibar ulichanganywa. Sherehe hizo zinaweza kufanyika nje ya Dar es Salam kama Kamati ya Maadhimisho ya Sherehe za Kitaifa itakavyoelekeza"

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuzingatia Mwongozo huo wa Maadhimisho ya Sherehe za Kitaifa hadi hapo kutakapokuwa na sababu za msingi zitakazofanya Mwongozo huo kufanyiwa marekebisho kwa nia ya kuuboresha. Hata hivyo, Serikali inahimiza wananchi kuadhimisha sherehe hizo kwa kufanya shughuli mbalmbali za maendeleo ikiwemo usafi, michezo, makongamano na shughuli mbalimbali za kijamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa Muungano umetuletea faida nyingi sana katika nchi yetu na ndiyo maana viongozi wetu, waasisi na sisi wenyewe tumekuwa tukiuenzi na kuulinda kwa nguvu zote na kwa kuwa sasa huko vijijini vijana wetu wengi wamekuwa hawana uwelewa sana wa kutosha kuhusiana na huu Muungano. Je, ni ni kwa nini sasa Serikali isiweke utaratibu wakati wa sherehe hizi elimu itolewe kwa ajili ya vijana wetu na wananchi walioko vijijini kuliko kufanya sherehe kitaifa zaidi? (Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati kwa niaba yake ambapo swali la msingi lilikuwa la

Mheshimiwa Martha Moses Mlata. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mlata kwa swali hili ambalo litatoa ufahamu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kutoa rai, siku ya tarehe 26 nafahamu itakuwa siku ya Ijumaa mwezi wa Nne kwamba Taasisi zote za Elimu zitumie fursa hii ya kutoa elimu kuhakikisha kwamba wanakuwa na makongamano na mijadala mbalimbali juu ya historia ya Muungano wetu. Ahsante.

**SPIKA:** *Okay,* siku ya Muungano mwaka huu tunatarajia kutakuwa na mechi kati ya timu ya Baraza la Wawakilishi ya mpira wa miguu na mpira pamoja na timu ya Bunge *Sports Club* hapa Dodoma, kwa hiyo tuendelee na maandalizi.

Swali linalofuata linakwenda Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano linaulizwa na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo.

Na. 110

**Ujenzi wa Barabara Inayounganisha Mbeya na Njombe**

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE** aliuliza:-

Wananchi wa Busokelo katika Kata ya Luteba walianza kutengeneza barabara inayounganisha Mikoa ya Mbeya na Njombe kupitia Mlima ya safu za *Livingstone:-*

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kuunga mkono juhudi za wananchi hao?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua Barabara ya Njombe-Makete-Isyonje Mbeya (kilometa 203.6) kama barabara rasmi inayounganisha Mikoa ya Njombe na Mbeya. Barabara anayoitaja Mheshimiwa Mbunge inayounganisha Wilaya ya Makete, Mkoa wa Njombe na Rungwe, Mkoa wa Mbeya ambayo ni barabara ya Mkoa. Aidha, kutoka Luteba hadi Ipelele katika Wilaya ya Makete kilometa 7.5, hakuna barabara inayoonekana wazi ni eneo la Milima mikali ya *Livingstone.*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Njombe-Makate kilometa 107.4 ambayo ni sehemu ya barabara ya Njombe-Makate-Isyonje-Mbeya inayounganisha Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Mbeya. Sehemu hii ya barabara hadi sasa ujenzi wake umefikia asilimia 26.

Mheshimiwa Spika, barabara inayopita katika safu ya Milima ya Livingstone inahitaji upembuzi yakinifu ambao ndiyo itakuwa msingi wa kufanya maamuzi. Kuhusu sehemu inayotengenezwa na wananchi katika safu ya Mlima Livingstone, Serikali itaangalia namna ya kusaidiana na wananchi waliojitolea kutengeneza sehemu hiyo ya barabara pamoja na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Busokelo, tafadhali.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nisikitike kwa niaba ya wananchi wa Busokelo kwa sababu barabara hii aliitembelea aliyekuwa Naibu Waziri wa Ujenzi kipindi hicho, Mheshimiwa Eng. Ngonyani tangu tarehe 21 Novemba, 2016 na aliahidi kwamba ingetengenezwa kwa kiwango cha changarawe

kilometa 7.5. Hili swali nimeliuliza Bungeni zaidi ya mara tatu na kila jibu linalokuja linakuwa tofauti na jibu lililotangulia. Wananchi wa Busokelo wanataka kujua ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za wananchi wa Jimbo la Busekelo, Kata ya Luteba ambao wameanza kutengeneza barabara hii kwa kilometa 4 wao wenyewe kwa jembe la mkono pamoja na Mbunge wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa barabara hii imeanzishwa na nguvu za wananchi na kwa maana hiyo Serikali haitambui kama iko *TARURA, TANROADS* ama kwenye vijiji. Ni lini sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuunganisha nguvu za pamoja za *TANROADS* na *TARURA* ili tujue ni nani atakayehusika na barabara hii? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, kumbe barabara hii hata haijulikani iko wapi? Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tumezungumza sana juu ya barabara hii na mimi kipande hiki cha barabara nilikitembelea eneo hili kweli lina changamoto kubwa. Barabara hii kimsingi inasimamiwa na wenzetu upande wa *TARURA* na sisi kwa maelekezo ya aliyekuwa Naibu Waziri wakati ule ni kwamba *TANROADS* twende tusaidie kutambua mahitaji na namna nzuri ya kuiboresha barabara hii, kazi ilifanyika na mawasiliano yalikuwa yanaendelea ya kupata fedha. Nitumie nafasi hii kuwaelekeza wenzetu wa Mfuko wa Barabara wafanye haraka kwa maana ya kuitoboa barabara hii ili ianze kutumiwa na wananchi na mimi nitaifuatilia ili kuhakikisha tunaitoboa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, lakini tunasanifu barabara hii ambayo nimeitaja kutoka Isyonje – Kikondo - Makete na hiki

kipande cha kilometa 7.5 kinatoka eneo la Busokelo kinaunga kwenye barabara hii ambayo itasanifiwa. Labda nielekeze pia wakati wa usanifu tuiangalie barabara hii kwa sababu kwenye milima hii ni hatari sana, kama itawezekana tuifanye kuwa *spur* ya barabara hii ambayo tutakuwa tukiisanifu. Kwa hiyo, wakati wa usanifu wa kilometa 7.5 tuiweke ili siku za usoni barabara hii iwe bora na iendelee kuwasaidia wananchi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mama Sitta nilikuona, uliza swali lako tafadhali.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru sana Serikali yetu kwa kujenga barabara ya Ndono - Urambo ambayo imekuwa msaada kwetu sana. Tatizo tulilonalo katika barabara hiyo ni kona inayoingia Urambo kwa kuanzia Ndorobo. Kona hiyo ni hatari kwa magari na pia kwa watembeaji wa miguu. Je, Serikali ni lini itaturekebishia barabara hiyo inayoingia Urambo Mjini kwa usalama wa watembea kwa miguu na magari kwa kutuwekea *round about?*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la wananchi wa Urambo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mama yangu Mheshimiwa Sitta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli eneo analolitaja Mheshimiwa Mbunge hata mimi mwenyewe nimeliona, ni

eneo ambalo linaunganisha barabara tatu lakini wataalam wa *TANROADS,* Mkoa wa Tabora wanapatazama hapa ili tuone kama tutaweza kuwa na *design* ya kuweka mzunguko hapo tutaweka lakini kama italazimika kuweka eneo lingine ili kuweza kudhibiti usalama wa watumiaji wa barabara maeneo hayo tutafanya hivyo. Tunalitazama kwa upana mkubwa ili tukitengeneza kitu tuweke kitu ambacho kitaweza kusaidia lakini kuleta maana na mahitaji ambayo Mheshimiwa Mbunge anayataja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira wanapatazama kwa sababu kwa namna inavyounganisha barabara tatu pale kidogo kulikuwa kuna changamoto fulani ambazo wataalam wanazifanyia kazi ili tuje tupate mchoro mzuri ambao pia hata gharama zake kuweza kurekebisha zitakuwa nzuri. Tunalifanyia kazi, vuta subira na wananchi wa Urambo wanasikia kwamba tupo pamoja nao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza kwamba barabara ya Handeni – Kiberashi – Kiteto –Chemba - Kwamtoro - Singida ilishafanyiwa upembuzi yakinifu muda mrefu na wananchi walishawekewa alama za X. Naomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie katika bajeti ya mwaka huu wataanza kulipwa fidia na kuanza ujenzi wa barabara hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tuibie bajeti yako kidogo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nkamia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli usanifu wa barabara hii ya Handeni – Kiberashi - Chemba - Singida kilometa 461

usanifu wake ulishakamilika na Serikali inatafuta fedha. Hata hivyo, kabla ya kuanza ujenzi utaratibu ni kwamba lazima wananchi wote wanaopitiwa na eneo hili la barabara waweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Nkamia tunaendelea kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili wananchi hao walipwe haki zao ili tukipata fedha ya kuanza kujenga barabara isiwe kikwazo kwa sababu wananchi hawajalipwa fidia. Kwa hiyo, vuta subira na nitaendelea kukupa *update* ili basi ile *appetite* ya wananchi kupokea fedha za *compensation* waweze kujiandaa kwa maendeleo yao mengine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lubeleje, zamu yako.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spoika, kwa kuwa barabara ya kutoka Gulwe – Berege – Mima - Sazima - Seruka na barabara hiyo Spika unaifahamu kwa sababu umeishi Mima. Barabara hii *TARURA* hawawezi kuitengeneza kwa sababu hawana fedha za kutosha na Serikali ilikubali kuichukua barabara hii ili ifanyiwe matengenezo makubwa. Je, Mheshimiwa Waziri unasemaje kuhusu suala hili?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli eneo alilotaja Mheshimiwa Mbunge la Gulwe – Berege – Mima - Seruka ni eneo ambalo lina changamoto zake kwa sababu linapitiwa na maji mengi wakati wa mvua na kumekuwa na uharibifu mara kwa mara.

Kikubwa tu Mheshimiwa Lubeleje nikuondoe hofu usubirie ni wiki ijayo tu Jumanne utaona namna tulivyojipanga kurekebisha barabara hii ikiwa ni pamoja na eneo la Godegode.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Bunge lako likitupitishia fedha tunakwenda kufanya usanifu na kufanya ujenzi kwenye eneo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi eneo hili na mimi nililitembelea na yako maeneo mengine pia Mheshimiwa Lubeleje atayaona kwa maana ya Mpwapwa kwa ujumla wake tumeitazama kwa macho mawili kwa sababu tunajua changamoto za barabara katika maeneo yake.

**SPIKA:** Swali na mwisho, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona na kunipa fursa niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa moja ya changamoto za maendeleo vijijini ni ukosefu wa barabara zinazopitika na kwa kuwa *TARURA* imeundwa ili ku-*address* changamoto hiyo. Kwa kuwa katika Wilaya nyingi nchini, *TARURA* haina mitambo ya kutengeneza au hata kufungua hizo barabara vijijini ikiwemo Wilaya ya Longido. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Wilaya zote ambazo *TARURA* haina mitambo ya kufanyia kazi wanapata mitambo hiyo?

**SPIKA:** Mitambo ya *TARURA,* Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niseme kweli tumekuwa na chombo hiki *TARURA* na imeanza kufanya kazi vizuri na Waheshimiwa Wabunge watakuwa mashahidi. Yako

maeneo ambayo yalikuwa na changamoto kipindi cha nyuma sasa yanafayiwa kazi vizuri. *TARURA* watasimamia shughuli za ujenzi wa barabara za vijijini kama wanavyosimamia *TANROADS,* kwa maana hiyo wakipata fedha uko utaratibu wa kutangaza, tunapata wazabuni, wakandarasi mbalimbali wanakwenda kufanya matengenezo ya barabara kwa utaratibu ule ule kulingana na Sheria za Manunuzi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi na *TARURA* wamefanya kazi nzuri na kwa muda mfupi wameshazitambua barabara zote na kuziingiza kwenye mfumo kwa sababu kulikuwa na changamoto ya barabara zingine ambazo zilikuwa hazitambuliki. Hivi karibuni wamepita karibu maeneo yote nchini kufanya sasa uhakiki kuona kama kuna sehemu barabara ilisahaulika iweze kuingia katika mtandao wa barabara.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo la Longido ni sehemu ambayo pia *TARURA* wamefanya kazi ya kutambua barabara. Kama nilivyosema ni kazi yetu sisi Bunge tukiwapa fedha za kutosha ninaamini barabara zote zitaboreshwa kulingana na changamoto zilizoko katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mbande - Kongwa hamna kinachoendelea, mkandarasi ameweka mikono pembeni maana yake hajalipwa chochote, basi na hilo nalo uliweke kwenye mambo ya ufuatiliaji wa karibu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali la Mheshimiwa Mbunge wa Njombe Mjini, Mheshimiwa Mwalongo, tafadhali.

Na. 111

**Serikali Kuwahudumia Wagonjwa wa Akili**

**MHE. EDWARD F. MWALONGO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwahudumia wagonjwa wa akili wanaozurura mitaani katika masuala ya matibabu, mavazi na makazi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendelea kuimarisha huduma za afya nchini ikiwemo huduma ya afya ya akili. Uimarishaji wa huduma ya afya ya akili umekwenda mpaka katika ngazi ya afya ya msingi ambapo ndipo jamii ilipo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongezeka kwa wagonjwa wa akili wanaorandaranda barabarani, Sheria Afya ya Akili ya mwaka 2008 inawataka ndugu na jamii kuibua wagonjwa wa akili na kuwapeleka kwenye vituo vya kutolea huduma ili wapate matibabu. Wagonjwa wakishapata nafuu huruhusiwa kwenda kukaa na familia zao kwenye jamii wanazotoka. Jukumu la kwanza la kulinda afya ya jamii huanzia ngazi ya familia lakini jamii zetu zimekuwa zikiwanyanyapaa, kuwabagua na kuwatenga wagonjwa wa akili na kupelekea wagonjwa wa akili kurandaranda mtaani.

Mheshimiwa Soika, kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Akili ya mwaka 2008, Sehemu ya Tatu, kifungu cha sheria

namba 9(1)(3) imeeleza wazi kuwa Afisa Polisi, Afisa Usalama, Afisa Ustawi wa Jamii ngazi ya Wilaya pamoja na viongozi wa dini, Afisa Mtendaji wa Kata, Afisa wa Kijiji wana jukumu la kubainisha mtu yeyote anayerandaranda kwa kutishia amani au vinginevyo na kumfikisha kwenye sehemu ya uchunguzi wa magonjwa ya akili na ikithibitika taratibu za kumpatia matibabu huanza kama ilivyoainishwa kwenye Sehemu ya Tatu ya Sheria ya Afya ya Akili ya mwaka 2008, kifungu namba 11(7)(12) cha sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa rai kwa jamii kuibua watu wanaoonekana kuwa na dalili za ugonjwa wa akili na kuwapeleka kwenye vituo cha afya ili waweze kupata matibabu kwani huduma hii ipo na inatolewa bila gharama yoyote. Magonjwa ya akili yanatibika, hivyo, nitoe rai kwa jamii waache kuwanyanyapaa wagonjwa wa akili na badala yake wawafikishe kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuwa ugonjwa wa akili hauna uhusiano na imani za ushirikina.

**SPIKA:** Muuliza swali, Mheshimiwa Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo la wagonjwa wa akili wanaorandaranda limekuwa sasa ni tishio kwenye jamii. Kwa mfano, wiki iliyopita tu mama mmoja Wilaya ya Nzega ameua watoto sita na amejeruhi watoto wengine wanne lakini katika jitihada za kumdhibiti na yeye mwenyewe ameuawa. Tunaona tena pia wagonjwa hawa wa akili wakiwa wamebeba mizigo na madudu chungu nzima na wanatishia usalama wa watu wengine.

Je, Serikali iko tayari sasa kuwaagiza Maafisa Ustawi wa Jamii kuchukua hatua haraka iwezekanavyo ili kukabiliana na tatizo hili?

**SPIKA:** Majibu ya swali hili, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, Naibu Waziri wa Afya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Franz Mwalongo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tunaendelea kuboresha huduma za afya ikiwa ni pamoja na masuala haya ya magonjwa ya afya ya akili. Tunachokifanya sasa hivi tumeweka Waratibu katika ngazi za Mikoa na Halmashauri zote. Kwa hiyo, katika masuala yanayohusiana na masuala ya afya ya akili, majukumu ya msingi yapo kwa Waratibu wa Afya ya Akili ngazi ya Mkoa na Halmashauri na tutaendelea kuwahimiza na kuwasimamia kuhakikisha kwamba wanatimiza wajibu wao huo.

**SPIKA:** Hili swali linawauliza maswali ya nyongeza wengi, inaelekea eneo hili lina *special interest* nchi nzima. Wiki hii Mheshimiwa Naibu Waziri kulikuwa kuna kitu kina-*trend* kwenye mitandao kinasema nchi nzima kulijengwa miradi ya maana Dodoma wakaletewa Hospitali ya Mirembe. Sasa sijui kama unaweza kutuambia kwa nini wali- *locate* hivyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Selasini, tafadhali.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa akili una sababu nyingi kama kurithi, matumizi ya madawa ya kulevya lakini vilevile mifadhaiko. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, zamani kulikuwa na vituo vya *couseling* kwenye shule, vyuo vikuu, taasisi ambazo zinajumuisha watu wengi kama hata hapa Bunge ambapo watu walikuwa wanakwenda wanapewa ushauri nasaha. Je, Serikali iko tayari kufufua vituo hivyo ili kusaidia kukabiliana na ugonjwa huu wakati unapoanza?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**: Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Selasini, nichangie kidogo katika suala hili ambalo umelisema, siyo kwamba wagonjwa wengi wa akili wako Dodoma, la hasha. Tulianzisha taasisi hii kubwa ya Hospitali ya Rufaa ya Kitaifa ya Mirembe Dodoma kwa sababu tu ya *nature,* pale tuna Gereza la Isanga na wengi wa wafungwa wanaopelekwa katika gereza lile ni wenye kesi kubwa hususani za mauaji, kwa hiyo, lengo ilikuwa ni kujihakikishia kama afya yao ya akili iko vizuri. Kwa hiyo, Mirembe ipo Dodoma siyo kwa sababu Mkoa wa Dodoma una wagonjwa wengi wa ugonjwa wa afya ya akili.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nirejee katika swali la msingi la Mheshimiwa Joseph Selasini, ni kweli visababishi vya afya ya akili ni pamoja na kurithi. Kuna watu ambao ndani ya familia yao wanapata magonjwa haya ya akili kutoka kwa baba na mama kwenda kwa watoto. Visababishi vingine ni matumizi ya madawa ya kulevya, vileo mbalimbali lakini hali ya maisha na *stress* ambazo watu wanazipata nazo zinapelekea watu kupata afya ya akili.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa mkubwa ambao unasumbua sana sasa hivi ni ugonjwa wa sonona *(depression).* Ugonjwa huu kidogo ni mgumu sana kuweza kutambulika, mtu huwa anaanza kujitenga, anajiona kwamba hana thamani katika jamii, anaona hathaminiwi na wengi wanaishia kwenda kujiua. Ni kweli hili jambo na sisi tumeliona kwa sababu tumeona matukio mengi ya aidha mtu kujidhuru yeye mwenyewe ama kudhuru familia yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hili tumeliona na tunaendelea kuimarisha huduma za msingi ikiwa ni pamoja na ushauri nasaha lakini vilevile naendelea kutoa rai jamii kuanza kubaini zile dalili za awali na kumpatia mtu huduma za afya ambazo anazihitaji. Magonjwa mengine haya si rahisi sana kuyabaini katika hatua za mwanzo lakini mtu anapoanza kuona mabadiliko ya kitabia kwa mtu ambaye yuko karibu naye ni vizuri basi mtu yule apate ushauri na nasaha au aende katika hospitali kupata huduma za afya.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hawa jamaa zetu wanaopita hospitali maarufu hii ya Mirembe wana heshima zao huko vijijini. Eeh, kilabuni kule pombe ikishakubali, basi akichokozwa anawaambia, msinicheze, mimi nina *file* Mirembe. Kwa hiyo, anaheshimika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Goodluck Mlinga, tafadhali.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ugonjwa wa kifafa una mahusiano makubwa sana na ugonjwa wa akili, kwa sababu mgonjwa wa kifafa akikosa zile dawa zake anakuwa amechanganyikiwa na anakuwa mkorofi na kibaya zaidi mgonjwa wa kifafa huwa anaanguka, kwa hiyo, anaweza kuangukia kwenye moto ama kwenye maji.

Mheshimiwa Spika, Ulanga ni miongoni mwa maeneo kinara duniani kwa kuwa na wagonjwa wengi wa kifafa na Serikali kwa uzito huo ikaamua kutoa dawa hizo bure kwa nchi nzima, lakini mgao tunaoupata Ulanga haukidhi mahitaji na Serikali inalitambua hilo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipa Ulanga kipaumbele kwa upatikanaji wa dawa hizi za kifafa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali. Inasemekena Ulanga inaongoza nchi nzima kwa tatizo hili, sijui kuna nini huko.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika mikoa ndani ya nchi yetu ambayo inaonekana kuna wagonjwa wengi wa kifafa ni pamoja na Ulanga. Nasi kama wataalaam wa afya tunajaribu kufanya utafiti kubaini chanzo, kwa nini Mkoa huu wa Morogoro na hususan katika Wilaya hii ya Ulanga kumekuwa na wagonjwa wengi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dawa za wagonjwa wa kifafa pamoja na wagonjwa akili tunazo za kutosha, tutafuatilia

katika Wilaya hii ya Ulanga kwa nini hizi dawa hazifiki ili kuhakikisha kwamba wale wote ambao wana ugonjwa huu wa kifafa katika Wilaya ya Ulanga wanapata tiba sahihi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii. Wauguzi wanaofanya kazi katika Wodi za Wagonjwa wa Akili, wanafanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi sana kwa sababu wagonjwa hao mara nyingi wako *hyper*:-

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwakatia Wauguzi hao bima ya maisha?

**SPIKA:** Swali muhimu sana hili. Sijui wauguzi wale wanafanyeje kazi yao; na kipekee Hospitali ya Mirembe wanatakiwa wawe na *scales* tofauti kabisa. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, matibabu ya afya ya akili ni taaluma na wataalam wetu hawa wamepata mafunzo mazuri tu ya jinsi gani ya kuweza kuwatibu wagonjwa hawa wenye matatizo ya afya ya akili katika hatua zile za awali ambazo sisi mara nyingi katika lugha ya kitaalaam tunaita a*cute phase,* lakini vilevile katika hatua ya mwendelezo wa yale matibabu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimthibitishie tu kwamba wataalam wetu wako vizuri na ndiyo maana hujawahi kusikia kwamba kuna muuguzi wala daktari amefariki au amepata kipigo kikubwa kutokana na kuhudumia wagonjwa hawa wa afya ya akili. Kwa hiyo, kwa sasa hatuna *evidence* ya kutosha ya kusema kwamba sasa watu wote ambao wanatoa huduma za afya kwa wagonjwa wa akili tuweze kuwakatia bima ya maisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa tuishie tu hapo kwa sababu mambo ya leo ni mengi. Niwatambue wageni haraka haraka.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; ambao ni viongozi wa Wizara na Taasisi za chini ya Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Susan Mlawi, ahsante, karibu sana Katibu Mkuu; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Nicholaus William, karibu Naibu; Mkurugenzi wa Habari, Dkt. Hassan Abbas, karibu sana; Mkurugenzi Mkuu wa *TBC,* Dkt. Ayoub Rioba, karibu sana; Kaimu Mhariri Mtendaji wa Magazeti ya Serikali *TSN,* Ndugu Tuma Abdallah, karibu sana; Mkurugenzi wa Utamaduni Dkt. Immanuel Temu, karibu sana; Mkurugenzi wa Sanaa, Dkt. Thiagho Kilonzo, karibu sana; na Kaimu Mkurugenzi wa Michezo Ndugu Addo Komba. *(Makofi)*

Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya BAKITA Dkt. Method Samuel; Mwakilishi wa Bodi ya Baraza la Michezo la Taifa, Col. Mstaafu Juma Ikangaa; Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)*, Ndugu Wallace Karia; Mwenyekiti wa Bodi ya *TASUBA*, Ndugu George Yambesi; Mtendaji Mkuu wa *TASUBA* Dkt. Herbert Makoye; Katibu wa Chama ha Muziki wa Disko Tanzania, Ndugu Asanterabi Mtaki; kutoka Chama cha Disko Ndugu Swalehe Besta; na Mkurugenzi Mtendaji wa *Multi Choice,* Jacqueline Wosco. Wameambatana na Viongozi na Maafisa wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya ofisi hiyo ya Wizara ya Habari. *(Makofi)*

Pia wako wadau wa habari nchini ambao ni pamoja na Mwakilishi wa Umoja wa Vyama vya Wanahabari Nchini *(UPTC),* Ndugu Abubakari Karsan; Mwakilishi wa Wamiliki wa Vyombo vya Habari Nchini *(MOAT),* Ndugu Henry Mhaiki; Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri, Ndugu Deodatus Balile *(TEF);* Mwenyekiti wa *MISA Tanzania*, Ndugu Salome Kitomari. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Mwakyembe ambao ni Wanamichezo na wasanii akiwemo msanii wa muziki wa kizazi kipya, Ndugu Raymond Mwakyusa, jina lake maarufu Rayvany; yuko msanii Ndugu Tenya Brown, karibu; yuko msanii mwingine Sayles Simon; pia yuko bondia wetu Bingwa wa Afrika Ndugu Hassan Mwakinyo. Yuko upande

gani Mwakinyo? Aah, yuko kule juu, karibu sana Hassan Mwakinyo. Wako wengine wanapenda ubondia humu ndani, haya bondia kaja sasa. *(Makofi/Kicheko)*

Pia wako wachezaji wa timu ya *Olympic* Maalum ambao wamechukua ubingwa wa Dunia katika michezo ya riadha na *Volleyball* wakiongozwa na ndugu Charles Rays, naomba msimame. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hii ni Timu ya Wanamichezo Walemavu ambao walienda kule Dubai wakatupatia ushindi huo mkubwa sana katika mchezo wa riadha na mchezo wa *Volleyball.* Hongereni sana, mmepeperusha bendera ya nchi yetu, mmetupatia heshima kubwa. Bunge letu linawashukuru na tunawapongezeni sana, karibuni Bungeni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wengine watano wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni wapiga kura wake kutoka Kyela Mkoani Mbeya wakiongozwa na Ndugu David Mwakinonge, ahsante, karibuni sana wageni wetu kutoka Kyela. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na Mchungaji Daniel Ngeneyan akiwa na wenzake 35, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Gibson Ole Meiseyeki, ni Wanakwaya ya Neema kutoka Sokoni Mkoani Arusha. Karibuni sana wanakwaya kutoka Sokoni kule Arusha, mnaitwa Neema, basi Neema iwe kwenu. Karibuni sana Dodoma. Wageni wawili wa Mheshimiwa George Lubeleje ambao ni Diwani wa Kata ya Berege, Mheshimiwa Yesse Mchiwa na Mwenyekiti wa CCM wa Kata ya Mpwapwa, Ndugu Erasto Mlewa, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Lubeleje pale mlipo. *(Makofi)*

Wapo wageni 18 wa Mheshimiwa Salum Khamis Salum ambao ni Walimu kutoka Shule ya Sekondari ya Kimali iliyopo Wilayani Meatu Mkoa wa Simiyu wakiongozwa na Katibu Tarafa wa Nyalanja, Ndugu Clara Joseph, karibuni sana, wako pale.

Wageni 44 wa Mheshimiwa Hassan Masala ambao ni wanachuo kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini na Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Juma Chikandanga. UDOM na Mipango karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Abdallah Ulega ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini wakiongozwa na Ndugu Masoud Katundu, karibuni pale mlipo.

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni kocha na wachezaji bora waliochaguliwa kucheza mpira wa miguu chini ya miaka 18 nchini Afrika Kusini, wanaotokea Mkoani Iringa; Ndugu Paulo Ngalawa, Ndugu Agapito Luhwago na Ndugu Lameck Mnyalape. Karibuni sana na hongereni sana kuwa katika wachezaji bora. Kumbe Iringa nayo imo eeh. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula, ambaye ni mdogo wake kutoka Jijini Mwanza, Ndugu Lilian Charles, karibu sana Lilian. Wageni watatu wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni viongozi wawili wa Chama cha MaDJ na mwanamziki Banana Zoro, Ndugu Asanterabi Mtaki na Ndugu Elizabeth Kilili. Eeh, wako pale, karibuni sana. Banana hatujawahi kukuona hapa bwana, karibu sana. Siku moja utunge wimbo kuhusu Mjengo bwana, tutashukuru. *(Makofi/ Kicheko)*

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni pamoja na wanafunzi watano kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Kitivo cha Elimu wakiongozwa na Ndugu Nancy Eliamani, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi wawili kutoka Jijini Dodoma ambao walitembea Bunge kujifunza jinsi linavyofanya kazi zake; Ndugu Pius Mboya na Ndugu Christian Charles. *(Makofi)*

Mwisho ni wanafunzi wanne kutoka Jijini Dodoma, Ndugu Hafsa Msonga, Ndugu Mariam Shaban, Ndugu Maria

Nyamhanga na Ndugu shaffy Zuberi. Karibuni sana wageni wetu wote. *(Makofi)*

Pia ninalo tangazo hapa kwamba tuna wageni saba wa Mheshimiwa Naibu Waziri Juliana Shonza, hawa wanatoka Taasisi ya *Tanzania Gospel Artists Network,* naomba msimame. Ahsanteni na karibuni sana.

Mheshimiwa Shally Raymond anawatangazia kwamba leo tarehe 18 Aprili kutakuwa na Ibada ya Alhamisi Kuu kwa Wakristo Wakatoliki mara baada ya kuahirishwa shughuli za Bunge saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge wote wanaopenda kushiriki Ibada hiyo, mnakaribishwa. Wanawakaribisha Waheshimiwa Wabunge pamoja na Wakristo wote wakiwemo wafanyakazi wa Bunge na wageni waliopo hapa Bungeni leo. Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moo Bungeni Mheshimiwa Shally Raymond anawaomba Wakatoliki saa 7.00 mchana ghorofa ya pili pale Msekwa juu. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo Waheshimiwa Wabunge najua tunaanza kesho shughuli za Pasaka, niwatakie kila la kheri kwa Pasaka njema popote pale mtakapokuwa. Kwa wale mtakaosafiri, mwende taratibu, tunawaombea kila la heri, tutaonana mara tu baada ya Pasaka. *(Makofi)*

Kwa jinsi hiyo nachukua hnafasi hii kumkaribisha Mheshimiwa Naibu Spika ili aweze kuendelea na ratiba iliyoko Mezani. *(Makofi)*

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo kwenye Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena kwenye Bunge lako Tukufu tukiwa wenye afya na uzima. Nashukuru pia kwa kuijalia nchi yetu kubaki katika hali ya amani na utulivu. Aidha, sina budi kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote pamoja Mheshimiwa Spika kwa ushirikiano mzuri mnaonipa unaoniwezesha kutekeleza kikamilifu majukumu niliyokabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii pia kumshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuniamini nisimamie Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kufuatilia kwa karibu maendeleo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano ambao imeendelea kutoa kwa Wizara yangu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba Mbunge wa Kigoma Kaskazini na Makamu wake Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Chemba. Kamati hii

ilijadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2019/2020 tarehe 29 Machi, 2019 na kuyapitisha kwa kauli moja. Wizara yangu itazingatia ushauri uliotolewa na Kamati katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge wote waliojiunga na Bunge lako Tukufu au kurejea Bungeni wengi wakiwa katika sura tofauti kichama. Nitumie fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kyela kwa imani, upendo, uelewa na ushirikiano mkubwa wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu yangu Kijimbo na Kitaifa kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, naomba niwahakikishie wana Kyela kuwa tutaendelea kushirikiana ili kuhakikisha Jimbo linaendelea kupiga hatua za uhakika za maendeleo na kutatua changamoto zinazoibuka. Aidha, naishukuru familia yangu kwa upendo na ushirikiano inayonipa ambayo umeniwezesha nyakati zote kutekeleza majukumu yangu kwa ari, weledi na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge na Naibu Waziri; Bi Suzan Paul Mlawi, Katibu Mkuu wa Wizara na Bwana Nicholas Benjamini William, Naibu Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma tija na ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhuhi ya hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2018/2019 na mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utelelezaji wa majukumu kwa kipindi cha mwaka 2018/2019, nianze na makusanyo ya maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2018/2019 Wizara ilikadiria kukusanya shilingi 1,077,804,000/= kutokana na vyanzo mbalimbali. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 650 zilipangwa kukusanywa kutokana na viingilio katika viwanja vya Taifa na Uhuru ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 shilingi 392,726,058/= sawa na asilimia 60 zilikusanywa.

Aidha, shilingi 369,002,000/= zilipangwa kukusanywa kutokana na malipo ya usajili wa magazeti na majarida. Ukodishaji wa ukumbi wa mikutano katika Idara ya Habari, Maelezo pamoja na mauzo ya vitambulisho vya uandishi wa habari na picha mbalimbali za viongozi wa Kitaifa ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 shilingi 127,347,929/= sawa na asilimia 35 ya lengo zilikusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya; chuo hicho kilipanga kukusanya Sh.58,800,000 ikiwa ni maduhuli yatokanayo na ada za wanafunzi. Hadi Machi, 2016 chuo kilikusanya Sh.249,731,110, sawa na asilimia 425 ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuoneshwa mubashara kwa mechi za mpira wa miguu kupitia *television* na programu tumizi *(apps)* za simu za mkononi ni sehemu ya sababu za kutofikiwa ipasavyo kwa malengo ya makusanyo ya maduhuli yatokanayo na shughuli za michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa taasisi saba zilizo chini ya Wizara kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni jumla ya shilingi 32,761,620,000 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019, shilingi 14,376,803,454 zilikusanywa, sawa na asilimia 44 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa ushindani katika biashara ya huduma za utangazaji *(electronic media)* ikiwemo magazeti *(print media)* kutokana na kasi ya ukuaji wa teknolojia katika sekta ya habari, hususan katika matumizi ya mitandao ya kijamii katika utoaji wa matangazo na baadhi ya wadau wa sanaa, filamu na michezo kutojitokeza ipasavyo kujisajili na kutambulika kisheria ni baadhi ya sababu zilizoathiri ukusanyaji wa mapato. Wizara inaendelea kutoa elimu kuhusu manufaa ya kujisajili kwa kushirikiana na wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2018/2019 Wizara iliidhinishiwa shilingi 33,349,675,000, ambapo kati ya fedha hizo shilingi 28,649,675,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida zikijumuisha mishahara shilingi 15,253,265,000 na matumizi mengineyo shilingi 9,396,410,000. Miradi ya maendeleo iliidhinishiwa shilingi 8,700,000,000. Hadi mwezi Machi, mwaka huu Wizara ilipokea shilingi 20,333,690,478 ambayo ni sawa na asilimia 61 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo shilingi 15,159,784,478 ni matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na asilimia 62, ambapo shilingi 10,092,123,378 ni mishahara, sawa na asilimia 66 na shilingi 5,067,661,100 ni matumizi mengineyo sawa na asilimia 54. Kwa upande wa miradi ya maendeleo kiasi kilichopokelewa ni shilingi 5,173,906,000 sawa na asilimia 59 ya kiasi kilichopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2018/2019; hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 hadi mwezi Machi imeelezewa kwa kina kisekta katika sehemu ya 3.2, ukurasa wa 11 hadi 62 katika kitabu cha hotuba yangu. Kwa muhtasari naomba kutoa taarifa hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Habari; majukumu ya sekta ya habari ni pamoja na kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003, Sheria ya Huduma za Habari Na.12 ya Mwaka 2016 na kuisemea Serikali kwa kutumia njia anuwai kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati na shughuli mbalimbali za kuwaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ni kama ifuatavyo:-

(a) Jumla ya mikutano saba na wanahabari kwa ajili ya kuwajulisha wananchi kuhusu utekelezaji au ufafanuzi wa shughuli za Serikali ulifanyika.

(b) Vipindi 17 vya Tunatekeleza vilivyohusisha Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Watendaji Wakuu wa Wizara, Taasisi, viliratibiwa na kurushwa hewani kupitia *TBC One.* Vipindi hivi hutoa fursa kwa viongozi hao kuelezea umma kuhusu utekelezaji wa sera na mikakati ya Serikali katika maeneo yao pamoja na fursa zilizopo.

(c) Kikao kazi kilichohusisha Maafisa Habari na Mawasiliano Serikalini 350 kiliratibiwa na kufanyika Machi, 2019 Jijini Mwanza. Kikao hiki kililenga kuwanoa na kuwakumbusha wajibu wao wa kuhakikisha wananchi wanapata haki yao ya kupata habari kwa haraka na kwa usahihi.

(d) Jumla ya magazeti mapya saba yalipewa leseni na leseni kwa magazeti 59 zilihuishwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari Na.12 ya mwaka 2016 kadi ya kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019. Aidha, tangu kuanza kutekelezwa kwa sheria hii mwaka 2017 magazeti 216 yamesajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* lilianza maandalizi ya ujenzi wa Makao Makuu yake Jijini Dodoma kwa kukamilisha michoro ya jengo. Aidha, mkataba wa ukarabati wa studio za redio na *television* Jijini Dodoma kwa lengo la kuziimarisha ili kuendana na mahitaji ya sasa ulisainiwa tarehe Machi, mwaka huu. Majukumu mengine yaliyotekelezwa na shirika hilo ni:-

(a) Kwanza kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro *(NTAA),* Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA),* Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS),* Mamlaka ya Usimamizi wa

Wanyamapori Tanzania *(TAWA),* Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB),* Kamisheni ya Utalii Zanzibar na Bodi ya Filamu Tanzania *(TFB),* ilianzishwa *channel* ya utalii *(Tanzania Safari Channel)* iliyozinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 15 Disemba, mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na taasisi na wadau kwa mchango wao katika uanzishwaji na uendeshaji wa *channel* hii. Aidha, nitumie fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa jumla kuitazama *channel* hii inayoonekana bure kupitia visimbuzi mbalimbali, ili kujionea vivutio vyetu vya utalii ukiwemo utalii wa kiutamaduni na kiasili na vilevile kuchukua hatua ya kuvitembelea.

(b) Kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika kupitia Bajeti ya Maendeleo ya *TBC,* usikivu umeongezeka kutoka wilaya 87 mwaka 2017 ambayo ni asilimia 54 hadi wilaya 102 ambayo ni asilimia 63 kufikia mwezi Machi mwaka huu. Mpango uliopo ni kuhakikisha usikivu wa redio unafikia wilaya 117 ili tufikie asilimia 73 katika mwaka ujao wa fedha. Aidha, ukarabati wa studio za kuhifadhi kumbukumbu za waasisi wa harakati za ukombozi Kusini mwa Bara la Afrika ulikamilika kwa kufunga vifaa na mitambo itakayotumika katika kubadilisha na kuhifadhi taarifa zote zilizoko katika maktaba ya redio katika mfumo wa kidijiti *(Digital Archiving).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mawasiliano *(TCRA)* kupitia kamati ya maudhui iliendesha semina za kuhamasisha utengenezaji na uzalishaji wa maudhui ya ndani yanayozingatia maadili, mila na desturi za Mtanzania kwa wadau wa utangazaji, Wahariri na Watayarishaji yaani Wasimamizi na Vipindi vya Redio na *Television* katika Mikoa ya Dar-es-Salaam, Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Mara, Mbeya, Mwanza, Njombe, Shinyanga, Tabora, Rukwa, Ruvuma, Songwe na Simiyu. Jumla ya wadau 184 kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na 91 kutoka Kanda ya Ziwa walishiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, elimu juu ya kanuni za maudhui mitandaoni, redioni na kwenye *television* zilitolewa mwezi Agosti, 2018 kwa wasanii na waandaaji wa maudhui ya filamu na muziki 100. Vilevile semina hizi zilitolewa kwa vituo vya utangazaji vya redio na *television* katika Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Singida na Tabora mwezi Januari mwaka huu ambapo Waandishi na Wanahabari wakiwemo Watangazaji, Wasimamizi wa Vipindi na Waandaaji wa Vipindi 27 walishiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo sita vya *television,* 15 vya redio na vituo 72 vinavyotoa huduma za maudhui mtandaoni vilipewa leseni kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019. Hadi Machi 2019, idadi ya vituo vya redio nchini ilikuwa 163, *television* 36 na idadi ya waliojisajili kutoa huduma za maudhui mtandaoni ilikuwa ni 274.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN)* iliendelea kutumia Soko la Afrika Mashariki kwa kuuza Magazeti ya Habari Leo na *Daily News* nchini Kenya na Rwanda. Aidha, mtambo mpya wa uchapaji wa kibiashara uliwasili na kazi ya kukarabati jengo ambalo mtambo utafungwa ipo kwenye hatua za mwisho. Uzinduzi wa mtambo huu utakaotoa huduma za uchapaji ikiwemo vitabu, majarida, taarifa, vipeperushi, shajara na mabango unatarajiwa kufanyika kabla ya mwezi Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utamaduni; sekta ya maendeleo ya utamaduni inahusisha kuenzi, kulinda, kuhifadhi na kuweka kumbukumbu za urithi wa utamaduni, ikiwa ni pamoja na historia, mila, desturi, sanaa, lugha na maadili na uzalendo. Majukumu yaliyotekelezwa katika sekta hii ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Utafiti wa lugha, mila na desturi za makundi makuu manne ya kilugha kwa jamii zenye wazungumzaji wachache ulifanyika Wilaya ya Mbulu, Mkoani Manyara.

(b) Ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa na takwimu za maeneo ya kihistoria, utamaduni, mila na desturi ulifanyika

kwa Mikoa ya Arusha, Dar-es-Salaam, Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mara, Mtwara, Mwanza, Njombe, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe na Tanga.

(c) Katika hatua za kukuza na kuendeleza Kiswahili Kitaifa na Kimataifa Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeandaa rasimu ya awali ya hati ya makubaliano ya ushirikiano *(MOU)* na mwongozo kwa ajili ya nchi zenye uhitaji wa wataalam wa kufundisha Kiswahili. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na taasisi zinazohusika na lugha ya Kiswahili za BAKITA, BAKIZA, TATAKI na vyuo vikuu nchini zinaandaa mwongozo na vitabu kwa ajili ya nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni Mratibu wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika yenye jukumu la kubaini, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu kuhusu harakati za ukombozi wa bara hili. Kumbukumbu hizo ni pamoja na vifaa, maeneo, majengo, nyaraka, mahandaki, maelezo, sare, silaha na magari na kumbukumbu nyingine zilizotumika wakati wa harakati za kulikomboa Bara hili la Afrika. Aidha, Taifa letu lilipewa jukumu hili na umoja wa Afrika mwaka 2011 kutokana na kuwa kiongozi, ngome imara kwa kuongoza mapambano ya harakati za kulikomboa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutengeneza programu hii hatua mbalimbali zilichukuliwa kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza maeneo 94 yaliyotumika wakati wa harakati za ukombozi wa bara la Afrika yalibainishwa kwa lengo la kukarabatiwa ili yatumike kama vivutio vya utalii vya kiutamaduni na kuhifadhi urithi wa ukombozi. Aidha, vifaa na nyaraka mbalimbali 6,782 kuhusu historia ya ukombozi wa Bara la Afrika vilibainishwa na kukusanywa kwa lengo la kuhifadhiwa kwa njia ya kidijiti na kuwekwa katika makumbusho ya historia ya ukombozi wa Afrika itakayojengwa Jijini Dar-es-Salaam.

(b) Ukarabati wa jengo lililopo Jijini Dar-es-Salaam lililokuwa likitumiwa na Kamati ya Ukombozi wa Bara la Afrika kwa takribani miaka 30 umeendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujitawala nchi za kiafrika ziliendelea kutumia vitabu vya historia vilivyoandikwa na walewale waliotutawala. Hali hii imesababisha michango ya baadhi ya mashujaa wetu wa harakati za ukombozi kwa makusudi kutoakisiwa na kutothaminiwa kabisa katika historia yetu, mathalani shujaa Heti Lema wa Wanyaturu, mwanamama aliyesimama kidete kuzuia utawala wa Kijerumani kwa zaidi ya miaka mitatu kwa kutumia makundi ya nyuki yaliyouma wazungu tu na kuwazuia Wajerumani wasikaribie Kilima cha Ng'ombo Ipembe na maeneo yaliyokizunguka, sasa Singida Mjini. Hata alipouawa na Wajerumani baada ya kusalitiwa wakoloni hao hawakuridhika waliamua kukata kichwa chake na kukipeleka Ujerumani kwa uchunguzi wa kina, ili kubaini kama alikuwa na uwezo maalum kibaiolojia wa kufundisha wadudu wenye ubongo mdogo kama nyuki kuwashambulia wazungu tu na muujiza aliowaonesha alipokutana nao kwa mazungumzo yaliyovunjika kwa kukaa juu ya ncha kali ya mkuki badala ya kigoda cha kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, shujaa huyu pamoja na mashujaa wengine wengi wa harakati za ukombozi, kama vile Mtemi Isike wa Tabora aliyepigana na Wajerumani kwa zaidi ya miaka minne na hatimaye kuzidiwa nguvu na kujinyonga na Nduna Nkomanile wa Wangoni, mwanamama mwingine aliyepambana kishupavu dhidi ya Wajerumani na kuuawa hawajaandikwa wala mchango wao kuthaminiwa katika historia ya nchi yetu iliyoandikwa na Wazungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kufufua kampeni ya kurejesha fuvu la Sjhujaa Leti na mashujaa wengine, Wizara itasimamia kampeni ya kuhimiza utafiti wetu, kuandika upya historia ya ukombozi wa nchi yetu na Afrika kwa ujumla, ili kuwezesha wanafunzi na vijana wetu kusoma historia yetu ambayo haijapotishwa kwa makusudi na hivyo, kuwasjengea moyo wa uzalendo, utaifa, mshikamano, umoja na upendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi nyingi kwa wadau wa programu hii wakiwemo Waheshimiwa Wabunge ambao wanaunga mkono juhudi za kuhifadhi historia ya ukombozi wa Bara la Afrika kwa kubuni miradi mbalimbali, hususan ujenzi wa makumbusho katika maeneo yaliyotumiwa na wapigania uhuru kutoka nchi za Kusini mwa Afrika. Nianze na Mheshimiwa Spika na Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kwa wazo la kuanzisha mpango wa kujenga *Kongwa Freedom Fighters Memorial Park.*

Aidha, nampongeza pia Mbunge wa Tunduru Kaskazini, Mheshimiwa Mhandisi Ramo Matala Makani, kwa jitihada za kuendeleza eneo lililotumiwa na wapigania uhuru wa *FRELIMO* kutoka Msumbiji kwa kuandaa maadhimisho ya Siku ya Tunduru Masonya *(Tunduru Masonya Day)* yatakayofanyika mwezi Julai, mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wana maeneo yaliyotumiwa na wapigania uhuru katika majimbo yao waendelee kubuni miradi mbalimbali ya kuyaendeleza na kuyahifadhi kwa ajili ya kukuza utalii wa kiukombozi na wa kiutamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) lenye jukumu la kuratibu na kusimamia matumizi ya maendeleo ya lugha ya Kiswahili nchini, hatua zifuatazo zilichukuliwa:-

(a) Jumla ya vipindi 564 vya redio na *television* vilivyolenga kuelimisha umma kuhusu matumizi fasaha na sanifu ya lugha la Kiswahili pamoja na fursa za lugha hiyo, viliandaliwa.

(b) Vitabu 45 vya kiada na ziada vilipitiwa na kupewa ithibati na huduma ya tafsiri na ukalimani ilitolewa wakati wa Mkutano wa Bunge la Afrika Jijini Kigali Rwanda, tarehe 18 hadi tarehe 3 Novemba, mwaka jana. Aidha, nyaraka 1,293 za mashirika, kampuni na taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zilitafsiriwa.

(c) Matini za maneno milioni moja na nusu zilizotokana na vitabu vya waandishi nguli wa riwaya na siasa ziliandaliwa na kupakiwa kwenye seva ya kongoo la Kiswahili. Aidha, vituo vinne vinavyofundisha Kiswahili kwa wageni vilipewa vyeti vya utambuzi.

(d) Zoezi la kusajili wataalam wa Kiswahili katika kanzi data ya wataalam hao tuliyoianzisha iliendelea, zoezi liliendelea ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla ya wataalam 624, wanaume 284 na wanawake 340 walisajiliwa. Aidha, mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni yalitolewa kwa wataalam hao katika Mikoa ya Dar-es-Salaam, Dodoma, Mbeya na Mwanza na mipango ya kufikia mikoa mingine inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa wataalam wa lugha ya Kiswahili kote nchini kujisajili katika kanzidata hii, ili wanufaike na fursa zake ikiwemo ukalimani na kufundusha lugha ya Kiswahili kwa wageni. Hivi sasa tuna maombi kutoka nchi nyingi za ndani na nje ya Bara la Afrika yanayohitaji walimu wa Kiswahili kwa ngazi mbalimbali za masomo. Kama nilivyoeleza awali, kwa sasa tunakamilisha mwongozo wa ufundishaji wa Kiswahili kwa ngazi mbalimbali na zoezi hili ni shirikishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Maendeleo ya Sanaa; majukumu ya sekta hii ni pamoja na kusimamia maendeleo ya shughuli za sanaa, filamu na ubunifu. Mwezi Septemba mwaka huu Tanzania itakuwa mwenyeji wa Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki linaitwa *Jama Fest,* linalohusu kuhifadhi, kulinda, kuendeleza na kutangaza urithi wa utamaduni, sanaa na ubunifu pamoja na shughuli za filamu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Maandalizi yanaendelea kupitia Kamati ya Kitaifa na Kikanda. Kauli Mbiu ya Tamasha hili ni Uanuwai wa Kiutamaduni Msingi wa Utangamano wa Kikanda, Maendeleo ya Kiuchumi na Kushamiri kwa Utalii au kwa Kiingereza, *"Cultural Diversity A Key Driver To Regional Intergration Economic Growth And Promotion Of Tourism".*

Mheshimiwa Naibu Spika, tamasha hili litahusisha shughuli mbalimbali yakiwemo matembezi ya shamrashamra za ngoma, *carnival* na maleba, mavazi yanayotoa fursa kwa kila nchi mwanachama kuonyesha utajiri wake wa utamaduni, maonyesho na biashara ya bidhaa mbalimbali za kiutamaduni na sanaa, kongamano na warsha kuhusu utamaduni, maonyesho na mashindano ya kifilamu, michezo ya jadi na watoto na maonyesho na soko la vyakula vya asili, mavazi na ulimbende. Zaidi ya washiriki 1,200 kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki watakuwepo na washiriki na wanunuzi zaidi ya 100,000 tunawatarajia katika shamrashamra hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha wadau mbalimbali wakiwemo wajasiriamali na wanautamaduni katika maeneo yao kushiriki katika tamasha hili ili kutangaza na kuuza kazi zao pamoja na kuanzisha mitandao muhimu ya kibiashara itakayoimarisha masoko ya kazi zao ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni ya uzalendo na utaifa iliyobeba kauli mbiu 'Kiswahili utashi wetu, uhai wetu' ikiwa na lengo la kuenzi na kusisitiza matumizi sahihi na fasaha ya lugha adhimu ya Kisawahili pamoja na kuhamasisha uzalendo yalifanyika na kufikia kilele chake tarehe 8 Desemba, 2018 Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Baraza la Sanaa la Taifa majukumu yaliyotekelezwa ni pamoja na kuhakiki kazi za muziki 342 na kuzipa idhini ya kutumika. Aidha, usajili na utoaji wa vibali vya kuendeshea shughuli za sanaa kwa wasanii na wadau wa sanaa wapatao 1,084 Tanzania Bara ulifanyika. Kupitia mradi wa utambuzi wa wasanii wa sanaa za ufundi Tanzania *(TASIP),* takribani wasanii wa sanaa za ufundi wapatao 6,000 kutoka Halmashauri za Wilaya ya Kinondoni na Ubungo Mkoani Dar es Salaam wametambuliwa. Ushauri kwa wasanii na wadau wa sanaa 2,638 kutoka maeneo mbalimbali nchini katika masuala ya masoko ya kazi za sanaa, uendeshaji wa matukio, utafutaji

fedha kwa vikundi na taasisi pamoja na masuala ya usajili na vibali ulitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Filamu Tanzania yenye jukumu la kusimamia shughuli za filamu nchini, ikiwemo utayarishaji, uhakiki na usambazaji wa bidhaa za filamu ilitoa vibali 121 vya utayarishaji wa picha jongevu ambapo 22 ni kwa waombaji kutoka ndani ya nchi na 99 kutoka nje ya nchi. Aidha, jumla ya filamu (*DVDs)* 961 zilihakikiwa na kupangiwa madaraja ambapo 821 ni za Kitanzania na 140 ni kutoka nje ya nchi. Majukumu mengine yaliyotekelezwa ni jumla ya maeneo 317 yasiyokuwa rasmi ya kusambazia na kuoneshea filamu na picha jongevu yalibainishwa katika Mikoa ya Songwe, Manyara na Tanga kwa lengo la kuyarasimisha na kupanua wigo kwa soko la bidhaa za filamu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa majumba ya sinema Jijini Dar es salaam, Tanga, Mtwara na Arusha ulifanyika. Kufuatia ukaguzi huo, majumba rasmi ya uoneshwaji wa filamu na picha jongevu Tanzania yamefikia 11 ambapo 7 yako Dar es Salaam, moja lipo Tanga, mawili yapo Arusha na moja lipo Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya kuwajengea uwezo wadau wa filamu wa kuzalisha kazi bora kwa kuzingatia weledi yaliendeshwa katika Mkoa wa Manyara, wadau walikuwa 104, Mkoa wa Songwe wadau 215 na Mkoa wa Tanga wadau 260. Aidha, mafunzo hayo yaliendeshwa pia Mkoani Morogoro kwa viongozi wa Shirikisho la Filamu Tanzania *(TAFF),* Bodi ya Shirikisho hilo na vyama vyake 11 vinavyojishughulisha na masuala ya filamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia tangazo la Wizara la kupitia upya mikataba mibovu waliyoingia baadhi ya wasanii na hivyo kuathiri kipato chao, kamati ya kupitia mikataba ya wadau wa filamu iliundwa na kuchambua mikataba 11 iliyowasilishwa. Baadhi ya kampuni zimethibitisha kuwalipa wahusika viwango vya kuridhisha na zingine zimeingia kwenye makubaliano maalum na kamati kuongeza malipo kwa viwango mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Kampuni za *Pan-Africa Enterprises Ltd* na Ivori Iringa zimeshaingiza kwenye akaunti maalum shilingi milioni 30 kwa kazi alizotekeleza Marehemu Amri Athumani (King Majuto) kimkataba. Aidha, Kampuni ya *Azam-SSB* imeandaa malipo ya ziada ya shilingi milioni 20 na Kampuni ya Tanfoam Arusha shilingi milioni 15 ambayo yatawasilishwa kwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu King Majuto. Vilevile, baadhi ya kampuni ikiwemo *Neelkanth Salt Ltd.* zimejiwekea utaratibu wa kuridhishaa wa mawasiliano ya moja kwa moja na familia ya King Majuto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Steps Entertainment* imeshamkabidhi mama wa marehemu Stephen Kanumba malipo ya ziada ya shilingi milioni 15. Pia kampuni hiyo imeahidi kushirikiana naye kuandaa filamu ya maisha ya mwanae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kampuni ya *Steps Entertainment* tayari imemlipa msanii Sikujua Mbwewe shilingi 6,750,000 kutokana na kusambazwa kwa filamu yake ijulikanayo kwa jina la 'Utu Wangu" bila ya ridhaa yake. Filamu hiyo amerejeshewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli orodha ni ndefu ikizingatiwa kwamba hatua zingine za kuondoa manung'uniko katika tasnia zinafanyika kupitia Chama cha Hatimiliki Tanzania *(COSOTA)* ambacho kipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara lakini kinafanya kazi kwa karibu na taasisi zote za sanaa za Wizara yangu. Migogoro iliyotatuliwa na *COSOTA* ni pamoja na Akim Igembe kumlipa Anna Joseph shilingi milioni 6 kwa kuwahisha sokoni filamu yake 'Naina; bila ruhusa yake; *Murchy Ben International* imemlipa Jenista Raymond Mao Dola za Marekani 1,500 kwa kuingiza mtandaoni filamu yake ya '*Perfect White'* bila kibali chake na mwanamuziki Peter Msechu ameilipa bendi kongwe ya muziki wa dansi hapa nchini *Atomic Jazz Band* ya Tanga shilingi milioni 1 kwa kukarabati na kuimba wimbo wa 'Tanzania yetu' bila ruhusa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ya Kupitia Mikataba bado haijafikia maridhiano na kampuni 7 zifuatazo: Kwanza, kazi za Marehemu King Majuto, Kampuni za *Freedom Film Production, Afsar Furniture, Sterling Surfactants Ltd, Al-Riyamy Production, Al-Abdi's Entertainemnts* na Tigo. Pili, kazi za Marehemu Stepehen Kanumba, Kampuni ya StarTimes. Tatu, kazi za Wastara Juma, Kampuni ya *KZG Service Ltd.* Nimezitaja kwamba bado tunazifuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazihimiza kampuni hizi zifikie makubaliano na Kamati mapema iwezekanavyo bila kulazimika kuzipeleka Mahakamani. Nawahimiza vilevile wadau wote wa sanaa kuhakikisha hawaingii mikataba hovyo hovyo bila ushauri wa kisheria. Nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kwa kujitolea na kwa uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) yenye jukumu la kutoa mafunzo ya sanaa na utamaduni katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ilidahili wanachuo 251; wanaume 199 na wanawake 52. Aidha, jumla ya wanachuo 118; wanaume 96 na wanawake 22 walihitimu mafunzo ya kozi ngazi ya Astashahada na wanachuo 105; wanaume 90 na wanawake 15 walihitimu mafunzo ya muda mfupi. Aidha, mitaala ya kozi zinazotolewa na TaSUBa ilihuishwa ili kuendana na mahitaji kama inavyoonekana katika aya ya 85 ukurasa wa 49 wa kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maendeleo ya michezo, majukumu yafuatayo yalitekelezwa katika sekta hii. Kwanza, maandalizi ya Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Vijana wenye umri chini ya miaka 17 *(AFCON-U17)* yanayofanyika nchini tarehe 14 – 28 Aprili, 2019 yaliendelea kufanyika ikiwemo ukarabati miundombinu ya viwanja vya Taifa na Uhuru vitakavyotumika katika mashindano hayo. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa Uwanja wa Michezo Mkoani Dodoma yaliendelea kwa kushirikiana na Kamati Maalum iliyoundwa na Rais. Vilevile ujenzi wa uwanja wa *Baseball* na

*Softball* kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)* ulikamilika na kuzinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 9 Desemba, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimeendelea kutoa mafunzo ya michezo ya muda mrefu ambapo idadi ya wanafunzi waliodahiliwa mwaka 2018 ilifikia 141; wanaume 110 na wanawake 31 ikilinganishwa na wanafunzi 125; wanaume 94 na wanawake 31 waliodahiliwa mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki Taifa letu limepata mafanikio makubwa katika michezo mbalimbali kama ifuatavyo: Kwanza, Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu *(Taifa Stars)* imefuzu kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Barani Afika *(AFCON)* nchini Misri mwezi Juni, 2019 baada ya kushindwa kufuzu kuingia kwenye hatua hiyo kwa zaidi ya miaka 39.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Vijana chini ya umri wa miaka 17 *(Serengeti Boys)* imefuzu kushiriki Mashindano ya Afrika ya Mpira wa Miguu kwa Vijana wenye umri chini ya miaka 17 *(AFCON-U17)* yanayofanyika nchini mwezi huu. Pamoja na kwamba tumeanza vibaya katika michezo miwili ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Timu ya Riadha iliyoshiriki Mashindano ya *Nagai City Marathon* yaliyofanyika nchini Japan mwezi Oktoba, 2018 ilishinda medali saba (Dhahabu mbili, Shaba mbili na Fedha moja). Nne, Bi. Madina Iddi wa Arusha aliibuka mchezaji bora wa kike Barani Afrika katika Mashindano ya Golf ya Wanawake ya Afrika yaliyofanyika Agosti, 2018 nchini Ghana. Tano, Timu ya Olimpiki Maalum *(Special Olympics)* ilishinda jumla ya medali 15 katika Mashindano ya Riadha na Mpira wa Wavu yaliyofanyika Abu Dhabi, Falme za Kiarabu Machi, 2018. Kati ya medali hizo tulipata Dhahabu 12, Fedha 1 na Shaba 2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Timu ya Wanawake ya Mpira wa Miguu *(Kilimanjaro Queens)* ilishinda mashindano ya *CECAFA* yaliyofanyika Julai, 2018 nchini Rwanda kwa mara ya pili mfululizo. Aidha, timu hiyo iliibuka bingwa wa mashindano ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Jijini Bujumbura, Burundi Agosti, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, kufuatia mabadiliko makubwa yaliyosimamiwa na Wizara, katika Ngumi za Kulipwa Nchini, imeundwa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania. Chombo hiki kipya cha kusimamia mchezo huo kimeweza katika muda mfupi kuleta mafanikio makubwa katika ndondi za kulipwa kama ifuatavyo, naomba hili nilieleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Fadhili Majiha alimtwanga Rofhiwa Nemushungwa wa Afrika Kusini na kuchukua Mkanda wa *WBA Pan African Bantam Weight,* mchezo uliofanyika Gauteng, Afrika ya Kusini tarehe 20 Julai, 2018. Pili, Hassan Mwakinyo alimpiga bingwa wa Uingereza wa uzito wa *Super Welter,* Sam Eggington kwa *TKO* katika mzunguko wa pili, Birmingham - Uingereza, tarehe 8 Septemba, 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Twaha Kassim Rubaha a.k.a Twaha Kiduku alimchapa Sharrif Kassongo wa DRC na kutwaa Mkanda wa *UBO Africa Super Welter Weight* katika mchezo uliofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 26 Septemba, 2018. Nne, Bruno Melchiory a.k.a Vifuaviwili alimnyuka Joshua English wa Australia katika Uzito wa *Super Feather* katika pambano lililofanyika New South Wales, Australia tarehe 13 Oktoba, 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Iddi Pialari alimdunda Wilson Masumba wa Malawi na kutwaa Mkanda wa *UBO Africa Welter Weight* kwa TKO katika mzunguko wa tano Jijini Dar es Salaam tarehe 26 Januari, 2019. Sita, Bruno Melchiory a.k.a Vifuaviwili alimchanachana Joel Brunker wa Australia na kutwaa Mkanda wa *IBF Pan Pacific Super Featherweight, Windor,* Australia tarehe 9 Machi, 2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, Hassan Mwakinyo alimkung'uta Sergio Gonzalez wa Nicaragua kwa KO katika mzunguko wa tano katika mchezo uliofanyika Jijini Nairobi, Kenya, tarehe 13 Machi, 2019. Nane, Iddi Mkwela alimchakaza Nicholaus Mwangi wa uzito wa *Super Lightweight* nyumbani kwao Kenya kwa TKO katika mzunguko wa pili Jijini Nairobi tarehe 23 Machi, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati wanamichezo wote nchini kwa kupeperusha vyema bendera ya Taifa katika mashindano mbalimbali ya kimataifa na hivyo kuitangaza na kuiletea heshima kubwa nchi yetu. Nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti na hatua anazozichukua kuimarisha michezo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu kwa kuipa Wizara yangu ushirikiano mkubwa na msaada katika kuendeleza michezo nchini. Pia niwapongeze Watanzania kwa hamasa na uzalendo wanaoonyesha kwa timu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Baraza lilisajili vyama 14, vilabu 165, vituo vya michezo 11 na mawakala au wakuzaji wa michezo 23. Vilevile iliratibu mashindano ya vyama vya michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa. Pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara mwaka 2018/2019 pia zilijitokeza changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na kuendelea kutozingatiwa kwa nidhamu kwa baadhi ya wasanii katika uendeshaji wa kazi zao na taarifa za upotoshaji zinazotolewa na baadhi ya vyombo vya habari na maudhui hasi mitandaoni. Hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo ikiwemo kutoa elimu kupitia vyombo vya habari na pale ilipobidi hatua za kisheria zilichukuliwa ili kuhakikisha jamii haiendelei kupotoshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia maendeleo ya Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na taasisi zake ambapo majukumu mbalimbali yamepangwa kutekelezwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya habari kwa kifupi, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuimarisha Chaneli ya Utalii *(Tanzania Safari Chanel);* kuimarisha usikivu wa *TBC* katika maeneo yenye usikivu hafifu pamoja na kuboresha studio za redio na televisheni. Adiha, ujenzi wa jengo la *TBC* la utangazaji Jijini Dodoma utaendelea. Kwa upande wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN),* kampuni hiyo itaanza uchapishaji wa kibiashara baada ya kukamilika kufungwa kwa mtambo wao mpya wa kisasa pamoja na kuimarisha ubora wa bidhaa zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* itaendelea kuhamasisha utengenezaji na uzalishaji wa maudhui ya ndani yanayozingatia maadili, mila na desturi za Mtanzania. Pia itaendelea kutoa elimu juu ya Kanuni za Maudhui Mitandaoni na Kanuni za Maudhui Redioni na kwenye Televisheni na kuchukua hatua pale ukiukwaji wa kanuni unapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maendeleo ya utamaduni, Baraza la Kiswahili (BAKITA) litaendelea kutoa elimu kuhusu matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili; kusajili wataalam wa Kiswahili katika kanzidata iliyoanzishwa; kutoa ithibati ya vitabu na kusajili taasisi na vituo vinavyofundisha Kiswahili kwa wageni. Aidha, Baraza litatoa huduma ya tafsiri na ukalimani kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maendeleo ya sanaa, Wizara itaratibu na kuendesha Tamasha nililosema la *JAMAFEST* la Afrika Mashariki; kufanya utafiti wa ala za muziki wa asili zilizo hatarini kupotea na kuendelea kuwajengea uwezo wasanii wetu na wadau wa sanaa. Aidha, Bodi ya Filamu itahakiki kupanga katika madaraja na kutoa vibali kwa

kazi za filamu na picha jongevu; kuwajengea uwezo wadau wa filamu; kutoa ithibati na uendeshaji wa shughuli za picha jongevu na kuendesha operesheni dhidi ya kazi za filamu zinazoingia sokoni bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Sanaa la Taifa litaendelea kuibua na kukuza vipaji vya sanaa; kuimarisha masoko ya kazi za sanaa; kuitangaza sekta ya sanaa ndani na nje ya nchi pamoja na kuimarisha mifumo ya utoaji taarifa na huduma. Aidha, kwa kushirikiana na Kampuni ya *Clouds Media International,* vijana kwa wazee wenye vipaji mbalimbali watahamasishwa washiriki katika Mashindano ya Kuibua Vipaji vyao katika ukanda huu wa Afrika Mashariki *(East Africa's GOT Talent)* yatakayofanyika nchini kuanzia Mei, 2019. Vilevile, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) iaendelea kutoa mafunzo ya sanaa na utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya michezo, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia shughuli za michezo nchini ikiwemo kukamilisha uhuishwaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, miundombinu na vifaa vya michezo katika shule teule za michezo nchini itaboreshwa pamoja na kuendelea kutoa mafunzo ya taaluma za michezo katika Chuo cha Maendeleo cha Michezo Malya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo yake, Wizara itaendeleza mahusiano mazuri iliyoanzisha na wadau ikiwemo sekta binafsi katika kutunza na kuendeleza michezo na miundombinu yake. Mfano, ni uhusiano kati ya Wizara na Kampuni ya Azam ambayo katika maandalizi ya Michuano ya *AFCON* kwa vijana chini ya umri miaka 17, kampuni hiyo iliruhusu kiwanja chake kutumika na kukifanyia ukarabati mkubwa ili kukidhi viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni Kampuni ya *Sport Pesa* iliyoingia makubaliano na Wizara kuweka nyasi mpya Uwanja wa Taifa na kusimamia utunzaji wake kwa kipindi cha miaka miwili. Kuandaa *Sport Pesa Super Cup* kila mwaka kuanzia mwaka 2017 na kuwezesha Klabu

ya Ligi Kuu ya Uingereza *Everton FC* kushiriki katika fainali za kikombe hicho na sasa tuko kwenye maandalizi ya kuikaribisha Timu ya Sevilla inayoshiriki Ligi Kuu ya Hispania *(LaLiga)* kuja nchini mwishoni mwa mwezi Mei kucheza mechi moja ya kirafiki na kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania. Wizara yangu itashirikiana kwa karibu na Wizara ya Maliasili na Utalii katika kufanikisha ziara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kampuni ya *Multi Choice Tanzania* kupitia programu yao inayoitwa *Project National Anthem* kwa miaka mitatu sasa inadhamini mchezo wa riadha ambapo kumekuwa na mafanikio makubwa ikiwemo kumwezesha mkimbiaji wetu Alphonce Simbu ambaye amepata mafanikio katika riadha ikiwa ni pamoja na kushinda medali ya dhahabu katika *Mumbai Marathon* mwaka juzi 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni hii pia imedhamini Timu ya Taifa ya Mbio za Nyika iliyoshiriki katika mashindano ya dunia yaliyofanyika mwezi Machi mwaka huu nchini Denmark na kutuwezesha kama nchi kupeleka timu kubwa zaidi katika mashindano haya katika historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa shukrani maalum kwa wafanyabiashara wawili; Mzee Reginald Mengi, Mwenyekiti wa Makampuni ya *IPP* na Mzee Subhash Patel, Mwenyekiti wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania *(CTI),* kwa msaada mkubwa waliotoa kwa Timu yetu ya Taifa ya Vijana na kwa Wizara. Mzee Mengi ni mlezi wa *Serengeti Boys* ambaye anailea timu hii kwa hali na mali. Ushiriki wetu kwenye Kombe la *COSAFA* kwa kiasi kikubwa uliwezeshwa na mlezi, Mzee Mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mzee Subhash Patel yeye ametupatia katoni 11,000 za maji na juisi, ametoa kwa Maafisa wa *CAF* vyumba 27 vya kulala na vingine kufanyia kazi katika Hoteli ya nyota tano ya *Sea Cliff* kwa kipindi chote cha mashindano ya Afrika ya Mpira wa Miguu kwa vijana wenye umri chini ya miaka 17 *(AFCON U-17)* na ameturuhusu kuweka timu za nchi tatu Hoteli ya *White Sands* kwa siku 14

bila malipo. Nikishindwa kutambua mchango huo mkubwa katika hotuba yangu, basi nitakuwa nanyemelea au nanyemelewa na roho ya kichawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nizishukuru Kampuni za *Sahara Energy* na *Engen* kwa msaada wa mafuta ya magari yote yanayotumika katika Mashindano ya *AFCON Under Seventeen (U-17).* Aidha, nimshukuru msanii Rayvanny kwa kuitangaza Timu ya Taifa *(Taifa Stars)* na pia kujitolea kutumbuiza katika ufunguzi wa Mashindano ya *AFCON U-17.* Hii ndiyo *spirit* tunayoitaka kwa vijana wetu wasanii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Michezo la Taifa *(BMT)* litaendelea kusajili vyama na mashirikisho ya michezo, kuratibu na kusimamia ushiriki wa Timu ya Taifa katika mashindano ya Kimataifa ikiwemo *All Africa Games Olympics* na *East African Community Games* na kutoa mafunzo ya utawala bora kwa viongozi wa vyama vya michezo na kuratibu chaguzi za vyama vya Kitaifa kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019/2020, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 959,905,000/= kupitia vyanzo vyake vinavyokusanya kupitia Idara ya Habari Maelezo na Idara ya Maendeleo ya Michezo. Aidha, kwa upande wa taasisi saba zilizo chini ya Wizara, kiasi kinachokadiriwa kukusanywa ni jumla ya shilingi 37,324,804,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo; kwa mwaka 2019/2020 Wizara imetengewa bajeti ya shilingi 30,879,483,000/=. Kati ya fedha hizo, mishahara ni shilingi 15,483,073,000/=. Matumizi mengineyo ni shilingi 9,396,410,000/= na miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni sita tu. Kimbatisho Na. XIII kinabainisha mgawanyo wa bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu taasisi zilizo chini ya Wizara na miradi ya maendeleo; ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2019/2020, naomba sasa Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha bajeti ya Wizara yangu kwa

mwaka 2019/2020 jumla ya shilingi 30,879,483,000/=. Kati ya fedha hizo, mishahara ni shilingi 15,483,073,000/=. Matumizi mengineyo ni shilingi 9,396,410,000/= na miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2018/2019 yalichangiwa pia na ushirikiano ambao Wizara iliupata kutoka kwa wadau mbalimbali. Wadau hao ni pamoja na Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Korea Kusini, Morocco, Norway, Sweden, Ujerumani na Urusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau wengine ni Umoja wa Mataifa, hususan Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO)* na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan *(JICA)* pamoja na Umoja wa Ulaya *(EU). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni *Azam TV*, Benki za *CRDB* na *NBC,* Kampuni ya *Coca Cola*, *Multichoice Tanzania Ltd., Nabaki Africa, Shell Tanzania,* Kampuni ya Bia Serengeti *(SBL), Sport Pesa, Startimes, IPP, Shabiby Line Bus Service, Clouds Media Group, UCSAF* na wengine wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana wadau hawa na kuwaomba kuendelea kushirikiana na Wizara katika kuziendeleza Sekta zake za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waandishi wa Habari, Wanamichezo na Wasanii kwa mchango wao katika kufikia mafanikio ya Wizara. Aidha, naishukuru sana Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia *Press A* kwa kuchapa hotuba hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Mheshimiwa Spika na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kuniskiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.habari.go.tz* au *www.wananchi.go.tz* na *www.tanzaniangovernment.blogspot.com.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Tunaendelea. Sasa tumsikilize Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Deo Ngalawa kwa niaba ya Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA - K.n.y. MWENYEKITI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, naomba kusoma taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Msingi wa uwasilishaji wa taarifa hii ni Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kupongeza Timu ya Taifa *(Taifa Stars)* kwa kuendelea kufanya vizuri katika michezo kama ambavyo tumeshuhudia hivi karibuni timu yetu imefuzu kushiriki fainali za michezo ya *AFCON* inayotarajiwa kufanyika nchini Misri mwezi Juni, 2019. Haya ni mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka 39 tangu Tanzania ishiriki kwa mara ya mwisho mwaka 1980. Tunaitakia kila la heri katika maandalizi ya *AFCON.*

Aidha, Kamati inawatakiwa kila la heri vijana wetu wa *Serengeti Boys* kwenye Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Vijana wenye Umri Chini ya Miaka 17 Barani Afrika *(AFCON U-17)* ambayo yanafanyika hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 6(5)(b) na Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, pamoja na majukumu mengine, Kamati hii inasimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inaeleza masuala makuu manne ambayo ni pamoja na hatua zilizofikiwa katika kutekeleza maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa mwaka unaoisha. Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa utekelezaji wa maoni ya Kamati, mpango wa bajeti ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha na kubaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; katika taarifa ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2018/2019

iliwasilishwa Bungeni mnamo tarehe 27, Aprili, 2018. Jumla ya maoni 11 yalitolewa na Kamati kwa lengo la kwenda kufanyiwa kazi na Wizara. Kamati imefanya tathmini ya utekelezaji wa maoni hayo na kubaini kuwa utekelezaji ni wa kuridhisha. Baadhi ya maoni ambayo Wizara imetekeleza ni pamoja na uanzishwaji wa kanzidata ya kusajili wataalam wa Kiswahili. Kamati inapongeza jitihada hii.

Aidha, baadhi ya maoni utekelezaji wake unaendelea. Kwa mfano suala la maandalizi mazuri ya Timu za Taifa ili ziweze kushiriki kikamilifu katika mashindano ya Kimataifa kama ambavyo tumeona hivi karibuni Timu yetu ya *Taifa Stars* ilivyofanya vizuri na kuifunga Timu ya Uganda na hivyo kufuzu kushiriki kwenye Mashindano ya *AFCON* yatakayofanyika nchini Misri, mwaka huu 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini ya Kamati hii kuwa timu itaendelea kufanya vizuri kwenye mechi zijazo na hivyo kufuzu kuingia kwenye mashindano ya Kombe la Dunia. Ikumbukwe kuwa kufanya vizuri kunahitaji umoja na ushirikiano kama ambavyo mwanamichezo Babe Ruth alivyowahi kusema; *"The way a team plays as a whole determines its success. You may have the greatest bunch of individual stars in the world, but if they don't play together, the club won't be worth a dime."*

Aidha, kuhusu uundwaji wa Bodi ya Ithibati na Baraza la Habari, Kamati iliarifiwa kuwa mapendekezo ya Wajumbe wa kuteuliwa kwenye bodi yamekamilika na hatua za upekuzi zinaendelea na mara zoezi hili litakapokamilika Baraza la Habari litaundwa kwani miongoni mwa Wajumbe wake wanategemewa kutoka katika Bodi ya Ithibati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kukamilisha utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendkezo yaliyobaki ikiwemo kutoa fedha kwenye maoni ambayo utekelezaji wake unahitaji fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi bilioni

33.8 kutoka kwenye idara na tasisi zake. Hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 12,604,628,187/= sawa na asilimia 37.2 tu ya lengo kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Na. 1. Kamati inatoa rai kwa Wizara kwa kuwa imetambua changamoto ya teknolojia imeathiri ukusanyaji wa maduhuli, ni vyema basi makadirio kwa mwaka wa fedha ujao yakazingatia changamoto hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa mwaka wa fedha 2018/2019; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara, Fungu 96, iliidhinishiwa shilingi bilioni 33. 3 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida yaliyoidhinishwa yalikuwa ni shilingi biloni 24.6 sawa na asilimia 73.9 na miradi ya maendeleo iliidhinishwa shilingi bilioni 8.7 sawa na asilimia 26.1. Kufikia mwezi Februari, 2019 Wizara ilipokea shilingi bilioni 19.1 sawa na asilimia 57.5 tu ya makadirio kama yanavyooneshwa kwenye kielelezo Na. 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha fedha zake zilizopatikana kabla ya mwaka wa fedha kwisha zikiwemo fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo shilingi bilioni 2.5 za Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC)* ambazo Kamati inaliambia fedha hizi ni muhimu kwa *TBC* ili iweze kutekeleza majukumu yake ya upanuzi wa usikivu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maelezo kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa; kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Kanuni hii Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi miwili ambayo ni:-

(a) Mradi wa ujenzi wa eneo changamani la michezo Dar es Salaam, namba ya mradi ni 6523, Fungu 96. Katika mwaka huu wa fedha 2018/2019, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni moja kwa ajili ya kufanya marekebisho mbalimbali

katika Uwanja wa Taifa na Uhuru ili iweze kutumika katika Mashindano ya Afrika ya Mpria wa Miguu kwa Vijana Chini ya miaka 17 *(AFCON U-17)* ambayo yanafanyika mwezi huu wa Aprili, 2019. Fedha hizi zote zimetolewa na zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa viwanja hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi hiyo inayofanywa, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto mbalimbali ikiwemo ya Bajeti ndogo isiyoendana na gharama za kutunza viwanja vya Taifa na Uhuru na kufutwa kwa utaratibu wa kubaki na sehemu ya mapato *Retention* yanayokusanywa katika viwanja kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa viwanja hivyo. Pamoja na changamoto hiyo, Kamati pia ilielezwa juu ya Kampuni ya *Beijing Construction* inayofanya ukarabati katika uwanja kuwa itamaliza Mkataba wake mwezi Agosti, mwaka huu 2019 na hivyo uwanja kutokuwa na mdhamini wa kukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Upanuzi na Usikivu wa Shirika la Utangazaji la Taifa *(TBC)*; Mradi huu ulitengewa kiasi cha shilingi bilioni tano, hadi kufikia Machi wakati Kamati inatembelea *TBC* shilingi bilioni 2.5 ilikuwa zimetolewa na kupokelewa na *TBC,* sawa na asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitembelea Ofisi za *TBC* Dar es Salaam na kujionea maboresho makubwa ya Ofisi hiyo. Kamati inapongeza sana jitihada hizi za Serikali na inaamini kuwa itaendelea kuipa fedha *TBC* ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, Kamati ilioneshwa Chaneli ya Utalii (Tanzania Safari) ambayo imeanzishwa kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii, maliasili, malikale na utamaduni wa Tanzania ili kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi kubwa ambayo *TBC* imefanya, Kamati ilibaini kuwa Taasisi hiyo inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Uhaba wa Vitendea kazi kwa ajili ya shughuli za utangazaji mfano magari, Kamera na Studio pamoja na

ukosefu wa studio za televisheni katika Makao Mkuu ya Nchi –Dodoma;

(ii) Uhaba wa wafanyakazi kuendesha chaneli za *TBC* hususan Chaneli Mpya ya Utalii Tanzania Safari;

(iii) Ukosefu wa chanzo cha uhakika cha mapato; na

(iv) Upungufu wa Bajeti ya Maendeleo kwa ajili ya kuboresha Miundombinu ya utangazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tatu, uchambuzi wa Mpango wa Mpango wa makadirio ya mapato ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020; katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara imepanga kutekeleza majukumu mbalimbali kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri. Aidha, Kamati ilielezwa kuhusu mpango wa ukusanyaji wa maduhuli na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kama ifuatavyo moja ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka 2019/2020; katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, Wizara inakadiria kukusanya jumla shilingi bilioni 38.2 kutoka katika Idara na Vitengo na Taasisi na Wizara. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadirio ya makusanyo kwa mwaka huu wa fedha 2019/2020 yameongezeka kwa shilingi bilioni 4.4, sawa na ongezeko la asilimia 13 kama ilivyoonyeshwa kwenye kielelezo Na.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini ongezeko la makadirio hayo ya makusanyo ni kutokana na matarajio ya Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ya kuongeza udahili wa wanafunzi, kuanzisha mitaala mipya pamoja na jukumu ililonalo la kuratibu Tamasha la 38 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo. Hayo yote yatasaidia kuongeza mapato. Kamati inapongeza ongezeko hili la Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli na ina imani kuwa lengo litafikiwa kabla ya mwaka ujao wa fedha 2019/2020 kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi; katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara inakadiria kutumia shilingi bilioni 30.8 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 24.8 sawa na asilimia 80.6 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo na shilingi bilioni sita sawa na asilimia 19.4 zinaombwa ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Uchambuzi wa Kamati imeonesha kuwa fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo, zimepungua kutoka shilingi 8,700,000,000/= mwaka 2018/2019 hadi shilingi 6,000,000,000/= mwaka 2019/2020 kuwa na upungufu wa shilingi 2,700,000,000. Kwa ujumla Bajeti yote ya Wizara Fungu 96 kwa Mwaka 2019/2020 imepungua kwa kiasi cha shilingi 2,470,192,000 sawa na asilimia 7.4. kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Na.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati, Baada ya uchambuzi huo wa Kamati, naomba kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Kupungua kwa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo; kama ilivyobainishwa kwenye uchambuzi wa Kamati, Bajeti ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Wizara imepungua. Si hivyo tu, lakini pia Mradi wa Eneo la Changamani la Michezo na hususan Uwanja wa Taifa na Uhuru haujatengewa fedha wakati Mkataba wa Ushirikiano baina ya nchi yetu na Jamhuri ya Watu wa China unafikia ukingoni mwezi Agosti, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa wastani wa gharama za uendeshaji wa Uwanja wa Taifa na Uhuru kwa mwaka ni takribani shilingi milioni 781. Kamati inashauri Serikali kwa mara nyingine kuongeza Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Wizara hii ili zipatikane fedha kwa ajili ya uendeshaji na ukarabati wa Uwanja wa Taifa na Uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)*; Kamati inatambua bado *TBC* inakumbana

na changamoto mbalimbali kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa hii. Changamoto hizi nyingi zinatokana na uhaba wa fedha. Pamoja na jitihada zinazoendelea kufanywa na Serikali katika kutatua changamoto hizi, Kamati inaona bado nguvu zaidi inahitajika na hivyo basi Kamati inashauri Bajeti ya *TBC* iongezwe ili:-

(i) Inunue vitendea kazi kama Kamera za kisasa na magari ya utangazaji;

(ii) Usikivu uweze kufika maeneo mengi zaidi ikibidi kuzidi malengo ya TBC ya kusikika katika Wilaya 117 sawa na asilimia 73;

(iii) Studio ziboreshwe ziendane na Shirika la Utangazaji la Taifa;

(iv) Itoe ajira kwa Watumishi ili kupunguza changamoto ya uhaba wa Watumishi husus an wa Chaneli ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Chaneli ya Utalii (Tanzania Safari), Kamati inapongeza Serikali kwa kuamua kuanzisha Chaneli ya Utalii (Tanzania Safari) kwa lengo la kuvutia Watalii. Ni kweli wote tunafahamu mchango wa Sekta ya Utalii kwenye Pato la Taifa ni takribani asilimia 17.2. Kamati ina amini kuwa, Sekta hii inaweza kuchangia zaidi endapo tutaboresha chaneli hii. Kamati inashauri kuwa maudhui ya chaneli yaboreshwe, *subtitles* za lugha mbalimbali ziwekwe, vipindi viandaliwe katika maeneo ya vivutio na chaneli ianze kuonekana nje ya Tanzania kwa kuwa lengo la uanzishwaji wa Televisheni hii ni kwa ajili ya kuonesha vivutio mbalimbali vilivyopo katika nchi yetu na kuwavutia watalii wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Taasisi ya Sanaa Bagamoyo; Taasisi ya Sanaa Bagamoyo (TaSuBa) pamoja na majukumu mengine, pia ni Kituo cha Ubora uliotukuka cha Jumuiya ya Afrika Mashariki tangu Mwaka 2012. Taasisi hii imekuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za miundombinu kwa muda mrefu. Kamati inashauri Serikali

itenge fedha kwa Taasisi hii ili iweze kujenga ukingo utakaosaidia kuzuia bahari isiendelee kuharibu miundombinu ya chuo pamoja na kukarabati miundombinu mingine kama madarasa na kumbi za maonesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN)* Kamati imebaini kuwa moja ya sababu inayosababisha kupungua kwa mapato ya TSN ni pamoja na mauzo duni ya magazeti yake kama vile *Daily News*. Kamati inaona ni wakati sasa kwa *TSN* kuboresha maudhui ya magazeti yake ili yaweze kushindana kwenye soko na hivyo kuongeza mapato ya Kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Baraza la Michezo la Taifa (BMT); Kamati inatambua kazi kubwa iliyonayo BMT hususan katika Mwaka huu ya kuratibu na kusimamia ushiriki wa Timu za Taifa katika Mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kama vile *All Africa Games,* Olympiki na *EACG*. Hata hivyo, Kamati inaona bado Taasisi hii haijawezeshwa kikamilifu kifedha ili kuweza kuratibu shughuli hizi. Kamati inashauri Serikali kuiruhusu BMT iweze kubakia na sehemu ya mapato yake *(Retention)* ili iweze kuratibu vyema majukumu yake kwa ustawi wa michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, mchango wa Wadau katika Michezo; Maendeleo ya Michezo yanahitaji nguvu ya pamoja. Kamati inaishukuru Kampuni ya *SportPesa* kwa mambo mbalimbali inayoendelea kufanya katika Sekta ya Michezo nchini. Kamati inatambua kuwa *SportPesa* imekuwa ni mdhamini wa baadhi ya timu zetu nchini, lakini pia ndiyo iliyoingia Mkataba wa uwekaji wa nyasi katika Uwanja wa Taifa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.3. Sambamba na *SportPesa*, Kamati inaishukuru na kuipongeza pia Kampuni ya *MultiChoice* Tanzania kwa kuendelea kudhamini mchezo wa riadha nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inazipongeza Kampuni hizi za *SportPesa* na *MultiChoice* Tanzania na inatoa wito na kuzisihi Kampuni nyingine ziweze kujitokeza kudhamini Sekta ya Michezo nchini. Kamati inatambua kuwa kwa

kufanya hivyo, kutasaidia Sekta hii kukua. Kuna msemo usemao "*Team Work makes the Dream Work*". Kamati inaamini kuwa Makampuni mbalimbali yakijitokeza kudhamini Sekta hii basi ndoto ya nchi yetu kuwa juu kwenye michezo itafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa muda wa kuwasilisha taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kukupongeza kwa uongozi wako thabiti ulionao katika kuendesha Bunge letu. Nawashukuru na kuwapongeza pia Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee naomba kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, majina yameambatanishwa na naomba yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe; Naibu Waziri Mhe. Juliana Shonza; Katibu Mkuu Ndugu Susan Mlawi; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Nicolaus Benjamin; pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati ikiwa ni pamoja na kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizojitokeza wakati wa uchambuzi wa Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Dickson Bisile; Makatibu wa Kamati Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Agnes Nkwera kwa kuratibu vyema shughuli zote za Kamati ikiwa ni pamoja na kuishauri Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo - Fungu 96 kwa mwaka wa fedha 2019/2020, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja jumla ya Shilingi 30,879,483,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Ngalawa kwa niaba ya Mwenyekiti.

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Msingi wa uwasilishwaji wa Taarifa hii ni Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kuipongeza Timu ya Taifa (Taifa Stars) kwa kuendelea kufanya vizuri katika Michezo kama ambavyo tumeshuhudia hivi karibuni Timu yetu imefuzu kushiriki Fainali za Michezo ya AFCON inayotarajiwa

kufanyika nchini Misri mwezi Juni, 2019. Haya ni mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka 39 tangu Tanzania ishiriki kwa mara ya mwisho mwaka 1980. Tunaitakia kila la kheri katika Maandalizi ya AFCON. Aidha, Kamati inawatakia kila la kheri vijana wetu wa *Serengeti Boys* kwenye mashindano ya Mpira wa Miguu kwa vijana wenye umri chini ya Miaka 17 barani Afrika (AFCON –U17) ambayo yanafanyika hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 6(5)(b) na 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, pamoja na majukumu mengine, Kamati hii inasimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inaeleza masuala makuu manne (4) ambayo ni pamoja na hatua zilizofikiwa katika kutekeleza Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka unaoisha, Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa utekelezaji wa maoni ya Kamati, Mpango wa Bajeti ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha na kubainia yafuatayo:-

### 2.1 UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Katika Taarifa ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii ya Mwaka 2018/2019 iliyowasilishwa Bungeni

mnamo tarehe 27 Aprili, 2018, jumla ya maoni 11 yalitolewa na Kamati kwa lengo la kwenda kufanyiwa kazi na Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya tathmini ya utekelezaji wa maoni hayo na kubaini kuwa utekelezaji ni wa kuridhisha. Baadhi ya maoni ambayo Wizara imetekeleza ni pamoja na uanzishwaji wa kanzidata ya kusajili wataalam wa Kiswahili, Kamati inapongeza jitihada hizi. Aidha, baadhi ya maoni utekelezaji wake unaendelea kwa mfano suala la maandalizi mazuri ya Timu za Taifa ili ziweze kushiriki kikamilifu kwenye mashindano ya Kimataifa kama ambavyo tumeona hivi karibuni Timu yetu ya Taifa Stars ilivyofanya vizuri na kuifunga timu ya Uganda na hivyo kufuzu kushiriki kwenye Mashindano ya AFCON yatakayofanyika nchini Misri mwaka huu 2019.

**Mheshimiwa Spika,** ni matumiani ya Kamati kuwa Timu itaendelea kufanya vizuri kwenye Mechi zijazo na hivyo kufuzu kuingia kwenye Mashindano ya Kombe la Dunia. Ikumbukwe kuwa kufanya vizuri kunahitaji umoja na ushirikiano kama ambavyo mwanamichezo Babe Ruth alivyowahi kusema "***The way a team plays as a whole determines its success. You may have the greatest bunch of individual stars in the world, but if they don't play together, the club won't be worth a dime"***. Aidha, kuhusu uundwaji wa bodi ya ithibati na Baraza la Habari, Kamati iliarifiwa kuwa mapendekezo ya wajumbe wa kuteuliwa kwenye Bodi yamekamilika na hatua za upekuzi zinaendelea na mara zoezi hili litakapokamilika Baraza la Habari litaundwa kwani miongoni mwa wajumbe wake wanategemewa kutoka katika Bodi ya Ithibati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kukamilisha utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendelezo yaliyobaki ikiwemo kutoa fedha kwenye maoni ambayo utekelezaji wake unahitaji fedha.

### 2.2 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi **33,839,424,000/=.** Kati ya makadirio hayo ya makusanyo,shilingi

**1,077,804,000/=** sawa na **asilimia 3.1** zilikadiriwa kukusanywa kutoka kwenye Idara ya Habari Maelezo na Idara ya Maendeleo ya Michezo. Aidha, kiasi cha shilingi **32,761,620,000/=** sawa na **asilimia 96.9** kilikadiriwa kukusanywa kutoka katika Taasisi saba zilizo chini ya usimamizi wa Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa kufikia mwezi Februari 2019, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi **12,604,628,187/=** sawa na **asilimia 37.2** tu ya lengo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, ukusanyaji kwa upande wa Taasisi siyo wa kuridhisha kwani kati ya makadirio ya makusanyo ya shilingi **32,761,620,000/=** ni shilingi **11,882,125,629/=** sawa na **asilimia 36** ndiyo zimekusanywa kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 1.**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) pamoja na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) makusanyo yao ni chini ya **asilimia 50.** Kamati ilihoji sababu za makusanyo hayo madogo na ilielezwa kuwa mabadiliko ya Teknolojia yamesababisha utangazaji kupitia mitandao ya kijamii kutumika zaidi na kupunguza matangazo kwenye televisheni lakini pia wateja wengi kupunguza kununua magazeti na kuhamia katika habari mtandao kupitia tovuti na mitandao ya kijamii.

**Kielelezo Na. 1: Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Fungu 96 kwa Mwaka 2018/2019**

| UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA FUNGU 96 KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 | | | |
|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **MAKADIRIO** | **MAKUSANYO** | **ASILIMIA** |
| **IDARA NA VITENGO** | 1,077,804,000/= | 722,502,558/= | **67.0** |
| **TAASISI** | 32,761,620,000 /= | 11,882,125,629/= | **36.3** |
| **JUMLA** | **33,839,424,000/=** | **12,604,628,187/=** | **37.2** |

***Chanzo: Randama ya Wizara (2019) na Usanifu wa Kamati***


**Mheshimiwa Spika,** ***Kamati inatoa Rai kwa Wizara kwa kuwa imetambua changamoto ya teknolojia imeathiri ukusanyaji wa maduhuli ni vyema basi makadirio kwa Mwaka wa Fedha ujao yakazingatia changamoto hii.***

## 2.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA KWA MWAKA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara **(Fungu 96)** iliidhinishiwa shilingi **33,349,675,000/=** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida yaliidhinishiwa shilingi **24,649,675,000/=** sawa na **asilimia 73.9** (Mishahara shilingi **15,253,265,000/=** na Matumizi Mengineyo shilingi **9,396,410,000/=**) na Miradi ya Maendeleo iliidhinishiwa shilingi **8,700,000,000/=** sawa na **asilimia 26.1.**

**Mheshimiwa Spika,** kufikia mwezi Februari 2019, Wizara ilipokea shilingi **19,177,850,436/=** sawa na **asilimia 57.5** tu ya makadirio. Kamati ilielezwa kuwa fedha zilizopokelewa kwaajili ya mishahara ni shilingi **8,936,283,336/=** (**asilimia 58.6** ya makadirio), na kwaajili ya matumizi mengineyo shilingi **5,067,661,100/=** (**asilimia 53.9** ya makadirio) zimepokelewa. Aidha, kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo shilingi **5,173,906,000/=** sawa na **asilimia 59.5** ya makadirio zimepokelewa kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na.2.**

**Kielelezo Na. 2: Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2018/2019**




***Chanzo: Randama ya Wizara (2019) na Usanifu wa Kamati***

***Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha fedha zote zinapatikana kabla ya Mwaka wa Fedha kuisha zikiwemo fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo kiasi cha shilingi 3,526,094,000/= zinazojumuisha shilingi 2,500,000,000/= za Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ambazo Kamati inatambua fedha hizi ni muhimu kwa TBC ili iweze kutekeleza majukumu yake ya upanuzi wa usikivu nchini.***

## 2.4 MAELEZO KUHUSU MIRADI YA MAENDELEO ILIYOKAGULIWA

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Katika kutekeleza Kanuni hii, Kamati ilifanya ukaguzi wa Miradi 2 ifuatayo mnamo tarehe 22 Machi, 2019 Jijini Dar es Salaam:-

### a) Mradi wa Ujenzi wa Eneo la Changamani la Michezo Dar es salaam (Namba ya Mradi 6523 – Fungu 96).

**Mheshimiwa Spika,** Katika Taarifa ya Mradi iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilielezwa kuwa, Mradi wa Eneo la Changamani la Michezo Dar es salaam ulianza katika Mwaka wa Fedha 2004/2005 kwa ajili ya kutumika kwenye michezo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Utekezaji wa Mradi ulikuwa katika Awamu tatu ambazo ni:-

i) Ujenzi wa Uwanja wa Taifa uliokamilka mwaka 2007 ukiwa na hadhi ya Viwanja vya FIFA uliojengwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania kwa gharama ya **Dola za Marekani Milioni 23 sawa na asilimia 40.8** na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China waliotoa **Dola za Marekani Milioni 33.4 sawa na 59.2;**

ii) Ukarabati wa Uwanja wa Uhuru uliokamilika mwaka 2016 na ulioongeza uwezo wa kuchukua watazamaji 22,000 kutoka 15,000;

iii) Ujenzi wa Bwawa la kuogelea lenye hadhi ya Olimpiki, uwanja wa ndani, jumba la maonesho ya michezo, hosteli,

hoteli ya hadhi ya nyota tano, maduka makubwa na viwanja vya mazoezi ambayo bado haujaanza kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka huu wa Fedha 2018/2019, Wizara iliidhinishiwa shilingi **1,000,000,000/=** kwaajili ya kufanya marekebisho mbalimbali katika Uwanja wa Taifa na Uhuru ili iweze kutumika katika Mashindano ya Afrika ya Mpira wa Miguu kwa vijana chini ya Miaka 17 (AFCON –U17) ambayo yanafanyika mwezi huu wa Aprili, 2019 yakihusisha nchi 8 zikiwemo Nigeria, Cameroon na Angola. Ukaratabati ulilenga vyumba viwili vya kubadilisha nguo wachezaji, ujenzi wa paa la V.I.P, Sehemu Maalumu ya Waandishi wa Habari, kurekebisha mifumo ya maji taka, na uwekaji wa nyasi za bandia (pitch).

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati Kamati inatembelea Mradi huu fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu shilingi **Bilioni 1** zilikuwa zimepokelewa na Wizara. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa tayari shilingi **Milioni 82.4** zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa viwanja hivyo. Kamati imeelezwa kuwa ukarabati unafanywa na Kampuni ya Beijing Construction Engineering Group Co. kutoka China ambayo ndiyo iliyohusika na Ujenzi wa Uwanja wa Taifa pamoja na ukarabati wa Uwanja wa Uhuru. Aidha, Kamati ilitembelea maeneo hayo yaliyofanyiwa marekebisho na kukuta baadhi ya kazi zikiwa zimeshatekelezwa na nyingine zikiendelea.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi hiyo inayofanywa, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto mbalimbali ikiwemo ya Bajeti ndogo isiyoendana na gharama za kutunza viwanja vya Taifa na Uhuru na kufutwa kwa utaratibu wa kubaki na sehemu ya mapato (Retention) yanayokusanywa katika Viwanja kwaajili ya kugharamia uendeshaji wa viwanja hivyo. Pamoja na changamoto hiyo, Kamati pia ilielezwa juu ya Kampuni ya Beijing Construction inayofanya ukarabati katika Uwanja kuwa itamaliza Mkataba wake mwezi Agosti, Mwaka huu 2019 na hivyo Uwanja kutokuwa na mdhamini wa kukarabati.

**b) Mradi wa Upanuzi na Usikivu wa Shirika la Utangazaji la Taifa- TBC**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Upanuzi wa Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) ulitengewa kiasi cha shilingi **Bilioni 5** kilicholenga kutekeleza Ujenzi wa Makao Makuu ya TBC Mkoani Dodoma (**shilingi Bilioni 2**), shilingi **Milioni 913** zilitengwa kwaajili ya ukarabati wa studio za Redio na Televisheni Dodoma, Ununuzi wa Magari 11 ulitengewa shilingi **Bilioni 1.5**. Aidha, kwa ajili ya kuboresha mifumo ya Tehama Dodoma shilingi **Milioni 143** zilitengwa na shilingi **Milioni 443.3** zilitengwa kwa ajili ya kuanzisha Chaneli ya Utalii. Hadi kufikia mwezi Machi wakati Kamati inatembelea TBC shilingi **Bilioni 2.5** zilikuwa zimetolewa na kupokelewa na TBC sawa na **asilimia 50.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Ofisi za TBC Dar es Salaam na kujionea maboresho makubwa ya Ofisi hiyo. Kamati inapongeza sana jitihada hizi za Serikali na ina amini kuwa itaendelea kuipa fedha TBC ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, Kamati ilioneshwa Chaneli ya Utalii (Tanzania Safari) ambayo imeanzishwa kwaajili ya kutangaza vivutio vya utalii, mali asili, mali kale na utamaduni wa Tanzania ili kuvutia Watalii wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuongeza Pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi kubwa ambayo TBC imefanya, Kamati ilibaini kuwa Taasisi hiyo inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i) Uhaba wa Vitendea kazi kwaajili ya shughuli za utangazaji (Magari, Kamera na Studio pamoja na ukosefu wa studio za televisheni katika Makao Mkuu ya Nchi –Dodoma);

ii) Uhaba wa Wafanyakazi kuendesha chaneli za TBC hususan Chaneli Mpya ya Utalii (Tanzania Safari);

iii) Ukosefu wa chanzo cha uhakika cha mapato; na

iv) Upungufu wa Bajeti ya Maendeleo kwa ajili ya kuboresha Miundombinu ya utangazaji.

## SEHEMU YA PILI

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** Katika kikao baina ya Kamati na Wizara kilichofanyika mwishoni mwa mwezi Machi, 2019 katika viwanja vya Bunge – Dodoma, Kamati ilipokea, ilijadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara imepanga kutekeleza majukumu mbalimbali kama yalivyowasilishwa na Mhe. Waziri. Aidha, Kamati ilielezwa kuhusu Mpango wa Ukusanyaji wa Maduhuli na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kama ifuatavyo: -

### 3.1 UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara inakadiria kukusanya jumla ya shilingi **38,284,700,000,00/=.** Kati ya fedha hizo, shilingi **959,905,000/=** sawa na **asilimia 2.5** zinakadiriwa kukusanywa katika Idara na Vitengo na Shilingi **37,324,804,000/=** sawa na **asilimia 97.5** zinakadiriwa kukusanywa kutoka katika Taasisi saba zilizo chini ya Wizara.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka huu 2019/2020 kwa kulinganisha na Makadirio ya Mwaka 2018/2019. Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa, Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka huu wa Fedha 2019/2020 ya Idara na vitengo vya Wizara yamepungua kwa shilingi **117,899,000/=** sawa na **asilimia 11**. Aidha, kwa upande wa Taasisi, Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yameongezeka kwa shilingi **4,563,184,000/=** sawa na **asilimia 14**. Hata hivyo, kwa ujumla Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 yameongezeka kwa shilingi

**4,445,285,000/=** sawa na ongezeko la **asilimia 13** ikilinganishwa na shilingi **33,839,424,000/=** zilizokadiriwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 3.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitafakari chanzo cha ongezeko la Makadirio hayo ya Makusanyo ya Maduhuli na kugundua kuwa, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TasuBa) inatarajia kuongeza udahili wa Wanafunzi, kuanzisha mitaala mipya lakini pia itakuwa na jukumu la kuratibu Tamasha la 38 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo hayo yote yatasaidia kuongeza mapato.

**Mheshimiwa Spika,** ***Kamati inapongeza ongezeko hili la Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli na ina imani kuwa lengo litafikiwa kabla ya mwaka ujao wa fedha 2019/2020 kuisha. Ni rai ya Kamati kuwa mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli iboreshwe ili kuepuka udanganyifu na wizi unaoweza kujitokeza.***

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2018/2019 na 2019/2020**




***Chanzo: Randama ya Wizara (2019) na Usanifu wa Kamati***

## 3.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara inakadiria kutumia **shilingi 30,879,483,000/=** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi **24,879,483,000/=** sawa na **asilimia 80.6** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha Mishahara **15,483,073,000/=** na Matumizi Mengineyo **9,396,410,00**0/=. Aidha, shilingi **6,000,000,000/=** sawa na **asilimia 19.4** zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Tathmini ya Uchambuzi wa Kamati imeonesha kuwa, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na hususan Mishahara imeongezeka kwa takribani shilingi **229, 808,000/=** sawa na ongezeko la **asilimia 1.5** ikilinganishwa na makadirio ya Mishahara yaliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. **Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa ongezeko hili ni kutokana na ajira kwa watumishi wapya, kupandishwa vyeo kwa baadhi ya watumishi pamoja na kubadilishwa kada kwa baadhi ya watumishi kutokana na kupata sifa za muundo.**


**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa fedha zimepungua kutoka shilingi **8,700,000,000/=** Mwaka 2018/2019 hadi shilingi **6,000,000,000/=** Mwaka 2019/2020 sawa na upungufu wa shilingi **2,700,000,000/=** (**asilimia 31).** Kwa ujumla Bajeti yote ya Wizara (**Fungu 96**) kwa Mwaka 2019/2020 imepungua kwa shilingi **2,470,192,000/=** sawa na **asilimia 7.4**. Aidha, upungufu zaidi unaonekana kwenye fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama ilivyobainishwa hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuna haja na umuhimu wa kuongeza fedha za Miradi ya Maendeleo, ikumbukwe kuwa Mradi wa Ujenzi wa Eneo la Changamani la Michezo Dar es Salaam na Dodoma haijatengewa fedha pamoja na kwamba miradi hii ipo kwenye utekelezaji, si hivyo tu lakini pia ni miradi hii ni moja kati ya miradi ya kipaumbele iliyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa

Mwaka 2019/2020. Kamati inaona kutoitengea miradi hiyo fedha katika mwaka 2019/2020 siyo sawa.

**Mheshimiwa Spika**, **Kielelezo Na. 4** kinaonesha hali halisi ya ulinganisho wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na 2019/2020.

**Kielelezo Na. 4: Ulinganisho wa Bajeti kwa Mwaka 2018/2019 na 2019/2020**




***Chanzo: Randama ya Wizara (2019) na Usanifu wa Kamati***

**SEHEMU YA TATU**

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya uchambuzi huo wa Kamati, naomba kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo:-

### 4.1 Kupungua kwa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kama ilivyobainishwa kwenye uchambuzi wa Kamati, Bajeti ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Wizara imepungua. Si hivyo tu, lakini pia Mradi wa Ujenzi Eneo la Changamani la Michezo na hususan Uwanja wa Taifa na Uhuru haujatengewa fedha wakati Mkataba wa Ushirikiano

baina ya nchi yetu na Jamhuri ya Watu wa China unafikia ukingoni mwezi Agosti, 2019.

**Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kuwa wastani wa gharama za uendeshaji wa Uwanja wa Taifa na Uhuru kwa Mwaka ni takribani shilingi Milioni 781. **Kamati inashauri Serikali kwa mara nyingine kuongeza Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Wizara hii ili zipatikane fedha kwaajili ya uendeshaji na ukarabati wa Uwanja wa Taifa na Uhuru.**

### 4.2 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi Februari, 2019, ukusanyaji wa maduhuli kwa Wizara kama ilivyoelezwa awali ulikuwa ni **asilimia 37.2** tu! **Kamati inaitaka Wizara kuongeza kasi ya ukusanyaji ili ifikapo mwisho wa mwaka lengo la makadirio ya makusanyo liwe limefikiwa. Aidha, Kamati inashauri Wizara kuboresha mifumo ya ukusanyaji ili hata malengo ya makadirio ya mwaka huu ambayo yameongezeka yaweze kufikiwa**.

### 4.3 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua bado TBC inakumbana na changamoto mbalimbali kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa hii. Changamoto hizi nyingi zinatokana na uhaba wa fedha. Pamoja na jitihada zinazoendelea kufanywa na Serikali katika kutatua changamoto hizi, Kamati inaona bado nguvu zaidi inahitajika na hivyo basi Kamati inashauri Bajeti ya TBC iongezwe ili:-

a) Inunue vitendea kazi kama Kamera za kisasa na magari ya utangazaji;

b) Usikivu uweze kufika maeneo mengi zaidi ikibidi kuzidi malengo ya TBC ya kusikika katika Wilaya 117 sawa na asilimia 73;

c) Studio ziboreshwe ziendane na Shirika la Utangazaji la Taifa;

d) Itoe ajira kwa Watumishi ili kupunguza changamoto ya uhaba wa Watumishi hususan wa Chaneli ya Utalii.

Aidha, Kamati inaona ipo haja ya kuangalia mfumo wa Shirika hilo ambalo ni tofauti na Mashirika mengine ya Umma. TBC ina idadi kubwa ya viongozi (Wakurugenzi na Mameneja) jambo ambalo linaongeza gharama kubwa ya uendeshaji. Kamati inashauri TBC kama chombo cha habari (Media House) isiendeshwe kama mashirika mengine mfano Bandari, Reli, n.k.

### 4.4 Chaneli ya Utalii (Tanzania Safari)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza Serikali kwa kuamua kuanzisha Chaneli ya Utalii (Tanzania Safari) kwa lengo la kuvutia Watalii. Ni kweli wote tunafahamu mchango wa Sekta ya Utalii kwenye Pato la Taifa ni takribani **asilimia 17.2**. Kamati ina amini kuwa, Sekta hii inaweza kuchangia zaidi endapo tutaboresha chaneli hii. **Kamati inashauri kuwa maudhui ya chaneli yaboreshwe, *subtitles* za lugha mbalimbali ziwekwe, vipindi viandaliwe katika maeneo ya vivutio na chaneli ianze kuonekana nje ya Tanzania kwa kuwa lengo la uanzishwaji wa Televisheni hii ni kwa ajili ya kuonesha vivutio mbalimbali vilivyopo katika nchi yetu na kuwavutia watalii wa ndani na nje ya nchi.**

### 4.5 Taasisi ya Sanaa Bagamoyo (TaSuBa)

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Sanaa Bagamoyo (TaSuBa) pamoja na majukumu mengine, pia ni Kituo cha Ubora uliotukuka cha Jumuiya ya Afrika Mashariki tangu Mwaka 2012. Taasisi hii imekuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za miundombinu kwa muda mrefu. Katika Taarifa ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii ya Mwaka 2016/2017 iliyowasilishwa Bungeni mnamo tarehe 13 Mei, 2016, Kamati ilishauri umuhimu wa Serikali kutoa fedha kwaajili ya kuboresha miundombinu ya Taasisi hii. Hata hivyo, fedha hizi zimekuwa hazitolewi na ikumbukwe kuwa Taasisi ipo pembeni mwa ufukwe wa bahari na ipo kwenye tishio la bahari kutokana na mawimbi ya bahari kukaribia majengo ya Taasisi.

**Mheshimiwa Spika**, ***Kamati inashauri Serikali itenge fedha kwa Taasisi hii ili iweze kujenga ukingo utakaosaidia kuzuia bahari isiendelee kuharibu miundombinu ya chuo pamoja na kukarabati miundombinu mingine kama madarasa na kumbi za maonesho***.

### 4.6 Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa moja ya sababu inayosababisha kupungua kwa mapato ya TSN ni pamoja na mauzo duni ya magazeti yake kama vile *Daily News*. **Kamati inaona ni wakati sasa kwa TSN kuboresha maudhui ya magazeti yake ili yaweze kushindana kwenye soko na hivyo kuongeza mapato ya Kampuni.**

### 4.7 Baraza la Michezo la Taifa (BMT)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kazi kubwa iliyonayo BMT hususan katika Mwaka huu ya kuratibu na kusimamia ushiriki wa Timu za Taifa katika Mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kama vile *All Africa Games,* Olympiki na EACG. Hata hivyo, Kamati inaona bado Taasisi hii haijawezeshwa kikamilifu kifedha ili kuweza kuratibu shughuli hizi. **Kamati inashauri Serikali kuiruhusu BMT iweze kubakia na sehemu ya mapato yake (Retain) ili iweze kuratibu vyema majukumu yake kwa ustawi wa michezo hapa nchini.**

### 4.8 Mchango wa Wadau katika Michezo

**Mheshimiwa Spika**, Maendeleo ya Michezo yanahitaji nguvu ya pamoja. Kamati inaishukuru Kampuni ya SportPesa kwa mambo mbalimbali inayoendelea kufanya katika Sekta ya Michezo nchini. Kamati inatambua kuwa SportPesa imekuwa ni mdhamini wa baadhi ya timu zetu nchini, lakini pia ndiyo iliyoingia Mkataba wa uwekaji wa nyasi katika Uwanja wa Taifa kwa gharama ya shilingi Bilioni 1.3. Sambamba na SportPesa, Kamati inaishukuru na kuipongeza pia Kampuni ya Multichoice Tanzania kwa kuendelea kudhamini mchezo wa riadha nchini.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inazipongeza Kampuni hizi za SportPesa na Multichoice Tanzania na inatoa wito na kuzisihi Kampuni nyingine ziweze kujitokeza kudhamini Sekta ya Michezo nchini. Kamati inatambua kuwa kwa kufanya hivyo, kutasaidia Sekta hii kukua. Kuna msemo usemao "*Team work makes the Dream Work*". Kamati ina amini kuwa Makampuni mbalimbali yakijitokeza kudhamini Sekta hii basi ndoto ya nchi yetu kuwa juu kwenye michezo itafikiwa.**

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa muda wa kuwasilisha taarifa hii ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kukupongeza kwa uongozi wako thabiti ulionao katika kuendesha Bunge letu. Nawashukuru na kuwapongeza pia Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yenu.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee naomba kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya ikiwa ni pamoja na kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa weledi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mb | Mjumbe |
| 2. Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb | Mjumbe |
| 3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Peter Ambroce Lijualikali, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Bernadeta K. Mushashu, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Vicky Paschal Kamata, Mb | Mjumbe |
| 10. Mhe. Deogratius Francis Ngalawa, Mb | Mjumbe |
| 11. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb | Mjumbe |
| 12. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb | Mjumbe |
| 13. Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb | Mjumbe |
| 14. Mhe. John Peter Kadutu, Mb | Mjumbe |

| | |
|---|---|
| 15. Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb | Mjumbe |
| 16. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb | Mjumbe |
| 17. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb | Mjumbe |
| 18. Mhe. Mch. Dkt. Getrude Rwakatare, Mb | Mjumbe |
| 19. Mhe. Seleman Said Bungara, Mb | Mjumbe |
| 20. Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto, Mb | Mjumbe |
| 21. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb | Mjumbe |
| 22. Mhe. Joseph Leonard Haule, Mb | Mjumbe |
| 23. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb | Mjumbe |
| 24. Mhe. Maulid Ally Mtulia, Mb | Mjumbe |
| 25. Mhe. Hawa Abdulrahmani Ghasia, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kumshukuru Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (Mb), Naibu Waziri Mhe. Juliana Shonza (Mb), Katibu Mkuu Ndg. Susan Mlawi, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Nicolus Benjamin pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati ikiwa ni pamoja na kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizojitokeza wakati wa uchambuzi wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, namshukuru Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Dickson Bisile, Makatibu wa Kamati Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Agnes Nkwera kwa kuratibu vyema shughuli zote za Kamati ikiwa ni pamoja na kuishauri Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (**Fungu 96)** kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, kama yalivyowasilishwa na mtoa jumla ya shilingi **Bilioni Thelathini, Milioni Mia Nane Sabini na Tisa, Laki Nne, Themanini na Tatu (30,879,483,000/=**).

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

Peter Joseph Serukamba (Mb),
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**
**18 Aprili 2019**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi nami ya kusoma hotuba yangu leo. Hotuba yangu imejikita zaidi kwenye uhuru wa habari kutokana na mazingira ya nchi tuliyokuwa nayo hivi sasa, kwa hiyo maeneo mengine nitagusa ngusa lakini zaidi niko kwenye Uhuru wa habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, napenda kuwasilisha kuhusu bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai na kuniinua…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sugu, nadhani ulishapewa taarifa ya maneno ambayo yameshaondolewa kwenye taarifa yako, naomba usome taarifa ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayo na mimi ninayo hapa mbele, tafadhali. Ondoa maneno yote ambayo yalikuwa yameshaondolewa nenda kwenye yale ambayo yapo kwenye vitabu walivyonavyo Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hata kumshukuru Mungu kumekatwa jamani, ehe, naomba nimshukuru jamani halafu niendelee. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sugu tafadhali, naomba usome hotuba ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda niwe naenda halafu uniambie kwamba hiyo toa, kwa sababu mimi siko hapa na *copy* ile ambayo,

**NAIBU SPIKA:** Sawa kama huna, Katibu mpatie nakala ya hiki kitabu kwa sababu ndiyo taarifa Wabunge wanayo, Katibu mpatie taarifa hii, ya kitabu hiki. Hiyo ndiyo iko sawa sawa, kwa hiyo tusomee hiyo Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya siyo maoni yangu, kwa sababu nikiangalia naona maoni yangu yamekatwa kwa asilimia 80, sasa kwa nini tunaogopa maoni? Ningeshauri tu *let's take care of democracy* alafu maendeleo yatakuja tu kwa sababu sasa hii ni sehemu ya ku-*debate, to enjoy debate* tulete hoja, mlete hoja, sasa mimi naleta hoja...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sugu hapo utakuwa na uchaguzi kwa sababu mwanzo ulisema una hii nakala ambayo Wabunge wanayo na wewe unafahamu kanuni zetu zinasema nini kwa sababu wewe ni mzoefu, umepewa nakala ambayo imeondoa maneno ambayo yapo kinyume na kanuni, kwa hivyo tusomee taarifa ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayo na umeshapewa hiyo nakala, endelea kusoma kama unataka kutoa hayo maoni, kama pia hutaki kutoa hayo maoni una uhuru, kwa sababu hii siyo mara ya

kwanza kutokuweka maoni. Kwa hiyo ni sawa, kama hutaki kutoa maoni unaweza kusema sitayasema, lakini kama unataka ni haya humu yaliyoko kwenye kitabu, nitakuruhusu uendelee kama unasoma yaliyoko humu, tafadhali.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika na mimi nimegundua huwa mnai-*temper* makusudi hotuba yangu ili niache kusoma na ndiyo maana nataka niwa-*condemn* hapa kwenye *podium*
kwamba mnavyofanya siyo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mbilinyi...

**WABUNGE FULANI:** Soma ya kwako, soma ya kwako.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mbilinyi, shukrani. Mheshimiwa Mbilinyi, naomba ukakae, tafadhali naomba ukakae.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumesikia taarifa ya Mheshimiwa Waziri aliyetusomea hapa, tumesikia pia taarifa ya Kamati ambayo imefanya kazi kwa niaba yetu Waheshimiwa Wabunge na sasa tutaendelea na utaratibu wetu wa uchangiaji. Kwa maana hiyo, hii taarifa haijaombwa kwamba iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kwa hivyo, haipo.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na wachangiaji ninayo orodha hapa mbele, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Khatib Haji ajiandae.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu. Kwa upande wangu, mara nyingi nasema Wizara hii ya Utamaduni ni Wizara mama ya Wizara zote ambazo zipo kwa sababu ndiyo Wizara ambayo inajenga misingi ya utaifa wetu ikiwemo uzalendo, maadili, udugu, mshikamano na ujamaa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kweli niwapongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wote akiwepo Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya ili kuweza kufikia malengo ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujikita sehemu kubwa moja ambayo kwa kweli bila kukumbushana maendeleo yote tunayoyapanga, bajeti yote tunayoipitisha katika Taifa letu haitaweza kufikiwa kama Watanzania leo hatutakuwa kitu kimoja na wazalendo katika nchi yetu. Tumeona mifano mingi ambayo inaendelea katika Taifa letu ambayo kwa kweli uzalendo wetu tusipoendelea kujikumbusha nchi hii itagawanyika katika misingi ya ukabila, udini, vyama vingi na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi dunia tunaona imeingia katika *crisis* ya uchumi, kwa hiyo, kila mtu anatafuta namna ya kumtawala mwingine ili aweze kupata masoko na kujua rasilimali zitatoka wapi. Watanzania tusipokuwa na mshikamano katika uzalendo na utaifa wetu kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kwa kazi anazozifanya hatutaweza kufikia maendeleo hata tungekuwa na Wizara ngapi au bajeti kubwa kiasi gani. Kwa sababu uzalendo ndiyo ambao unasema Taifa kwanza halafu mimi baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niombe kwamba fedha zote walizoomba Wizara hii wapewe lakini pia hata zile zilizobaki za 2017/2018 wapewe katika misingi niliyoisema ya umuhimu wa Wizara hii. Kwa nini nasema hivi? Kwa mfano, katika katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 18,

*item* ya 31 na ukurasa 24, *item* ya 42 amezungumzia suala la uzalendo. Sasa uzalendo maana kama nilivyosema nchi kwanza mengine baadaye, tumeona sasa hivi nchi inaweza ikawa na amani na utulivu lakini bila uzalendo maana yake rasilimali za nchi hazitatumika kwa tija ya Taifa zitatumika kwa mtu mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nisisitize kwamba katika nchi yetu kuna vipengele vya uzalendo. Vijana wengi sasa hivi wamechukua madaraka lakini wamezaliwa katika kipindi cha mageuzi, miaka ya 80 kuja mbele wakakutana na sera za ubinafsishaji, vyama vingi, haki za binadamu, kwa hiyo, kama alitoka kwenye familia ya ufisadi na uhujumu anachokijua ni hiko. Kwa hiyo, Wizara hii ina jukumu kubwa kushughulikia suala hili. Mlizindua Kampeni ya Uzalendo nafikiri 2017, nilikuwa nategemea katika ripoti yenu hiki kipengele jinsi ya kuwalea hawa vijana kuanzia mtu anapozaliwa, uzalendo ndugu zangu unazaliwa, unakua na unaweza ukafa. Kwa hiyo, lazima tulinde misingi ya uzalendo ambayo waasisi wetu walituwekea. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Tisekwa kuna taarifa, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa Daktari kwa kile anachokichangia na mimi namuunga mkono. Hata hivyo, nataka kumwambia uzalendo unaanzia kwenye nyumba hii hii ambayo ndiyo tunatunga sheria. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba uzalendo unaanzia humu ndani ndiyo utafika nje. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru anatambua kwamba wote tunatakiwa tuwe

wazalendo kuanzia kwenye nyumba hii. Pale tunapotunga sheria wote tukae ndani ya nyumba hii tutunge sheria, tunapopitisha bajeti wote tukae tupitishe bajeti kwa umoja wetu kwamba ndani ya nyumba hii hoja ndiyo zishike mshiko na siyo vitendo vya kususa na kadhalika. Kwa hiyo, nashukuru kwa kulitambua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme kwamba kuna Tunu zetu za Taifa ambazo zimejenga uzalendo nchi hii. Kwa mfano, Uhuru, Muungano na Mwenge wa Uhuru. Hivi vitu lazima watoto wetu wanapozaliwa, kama nilivyosema uzalendo toka mtu anapozaliwa kwa sababu unazaliwa na unakua, hizi tunu tunatakiwa tuzienzi lakini leo hii Uhuru, Muungano na Mwenge wa nchi hii unaonekana kama wa chama fulani. Kuna wenzetu bado wanadai Uhuru, kuna watu ambao wanataka Muungano uvunjike, kuna watu ambao wanataka Mwenge wa Uhuru usitishwe lakini hivi vitu vimebeba *philosophy* kubwa ya mshikamano, udugu, utaifa wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nashauri Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Waziri nyingine Mwenge wa Uhuru uheshimiwe kitaifa, bajeti yake iende kwenye Taifa isiwe sasa kuomba kama ilivyo sasa kwa sababu tunapoomba watu wanafikiri labda hii ni ya kichama lakini ndani ya Mwenge wa Uhuru ndiyo tunasema imulike, ilete amani, upendo na umoja. Kwa hiyo, naomba Kampeni hii ya Uzalendo mwende kule chini kuanzia chekechea mpaka vyuo vikuu tujenge taifa la uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusema hayo kwa mfano sasa hivi, Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kuna miradi hii mikubwa, mimi nimesomea maendeleo, kuna *stimulus* za maendeleo ambazo ni usafiri wa uhakika lakini pia *energy* (umeme) wa uhakika. Nachukulia mfano hii *Stigler's Gorge,* kwanza neno *Stigler* lenyewe limetoka wapi, huyu ni mkoloni, upembuzi yakinifu wa hii *Stigle'rs Gorge* ilifanywa toka wakati wa ukoloni na walikubali. Je, hili bwawa

kwa mfano lingejengwa wakati wa ukoloni haya masuala ya mazingira wangeyazungumza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika Awamu hii ya Tano hii *Stigler's* hakuianza yeye ni *strategic plan* ya miaka toka ya ukoloni, ndugu zangu tuwe wazalendo. Ulaya na Amerika wameharibu mazingira kiasi gani? Leo umeme tunalipa senti 12 wenzetu wanalipa senti 0.0 *something,* hivi hatuoni? Kwa hiyo, suala la uzalendo ni muhimu sana kulijenga katika nchi yetu, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa maendeleo ya nchi yetu, tusipokuwa wazalendo tutakuwa wabinafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimejikita kwenye sekta ya uzalendo na utaifa. Uzalendo hauwezi ukaja kwa kuzungumza lakini nachotaka kuzungumza pia rushwa, ufisadi, uonevu, dhuluma, hivi vyote vinamong'onyoa msingi wa uzalendo. Kwa hiyo, wenzetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daktari, muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, oooh, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemuita Mheshimiwa William Ngeleja atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Haji na Mheshimiwa Angelina Malembeka ajiandae.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema, nasimama hapa kuiunga mkono Serikali, kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote walioko katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yako mengi na muda ni mchache katika hotuba hii. Mimi nitajielekeza katika sekta ya michezo lakini pia sanaa. Mwaka huu umekuwa ni wa Taifa la Tanzania kwa mafanikio katika sekta ya michezo na hasa soka pamoja na tasnia ya sanaa. Wote tumeshuhudia tokea mwaka jana wakati ambapo Bunge lako Tukufu lilivyokwenda kushiriki Mashindano ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kule Bujumbura, Burundi, wachezaji wako wa timu ya *Bunge Sports Club* wakijumuisha michezo mbalimbali walishiriki kwa ufanisi mkubwa sana. Tumepata medali nyingi za kumwaga za Dhahabu, Fedha na nyingine ambazo zilikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachotaka kusema tu ni kwamba yote hii imetokana na maandalizi mazuri. Kwa nafasi ya *Bunge Sports Club* tunampongeza sana Mheshimiwa Naibu Spika, wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati na Wabunge wote kwa ujumla kwa namna ambavyo mmekuwa mkiunga mkono sekta hii na sisi ndiyo wasimamizi wa sheria zinazohusisha mambo ya michezo, sanaa na mambo mengine. Kwa hivi tumetembea katika maneno yetu na tumeonyesha kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na tunampongeza sana Mheshimiwa Spika. Ndiyo maana hata leo asubuhi wakati anasimamia *session* ya maswali na majibu ametoa taarifa kwa Watanzania kupitia Bunge hili Tukufu kwamba tarehe 26 Aprili, tutakuwa na mechi ya kirafiki kati ya *Bunge Sports Club* kwa *football* na *netball* pamoja na Baraza la Wawakilishi, ni jambo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ushiriki wetu si wa kupoteza muda kwa sababu tunatumia fedha za Serikali lakini pia zinatupa fursa sisi kama Taifa kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujua na kufanya itifaki ama kufanya utafiti kwa yale ambayo yanatuhusu kwa manufaa ya Taifa letu. Kupitia hili dirisha la ushiriki wetu naamini kwamba Serikali kimkakati inaweza kujua kinachotokea kwenye nyumba za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitazungumza kwa maneno mengi lakini nayafahamu Watanzania na hasa wanaoshiriki katika mambo yao kusimamia maeneo haya wanajua namaanisha nini. Ukijua kwa jirani kunatokea nini ni rahisi sana kujipanga na kujua kesho kutakuwaje kwa manufaa ya Taifa letu, kwa hivi tuendelee kuuunga mkono ushiriki wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili naipongeza sana Timu ya Taifa, mmefanya kazi kubwa Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, Daktari na Mwalimu wetu pamoja na wenzako mmefanya jambo kubwa. Ni miaka 39 imepita tangu tushiriki Mashindano ya Fainali za *AFCON* mwaka huu tunakwenda kushiriki. Ni jambo jema sana, hatujafikia hapa kwa bahati mbaya ni kwa sababu ya maandalizi. Tumeona ushiriki wa Serikali na hata Mheshimiwa Rais amekuwa akitoa hamasa. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali yake, wananchi kwa ujumla na sisi kama Bunge tukiwa sehemu ya wahamasishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda fainali lakini fainali hizi zimechagizwa sana na ushindi wa Simba uliopatikana katika ushiriki wa Klabu Bingwa ya Afrika. Wote tunafahamu kwamba Simba imefikia kuingia hatua ya robo fainali, kuanzia ushiriki wa Mashindano haya Klabu Bingwa Afrika kwa ligi ya mwaka 2021 Tanzania kwa hatua iliyofikiwa na *Simba Sports Club* tunakwenda kuingiza timu nne; Kombe la Shirikisho zitakwenda timu mbili na Kombe la Klabu Bingwa zitakwenda timu mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini? Ushabiki pembeni ukweli ni kwamba kama Taifa tunatembea vizuri. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na safu yako. Kwa ushiriki wa Simba tumepata pointi 15 kujumlisha na tatu ambazo Yanga aliziweka katika ushiriki wake wa miaka mitano, tumepata kile kigezo ambacho kinatuwezesha kuingia kwenye timu 12 na sasa tunapata ruksa ya kushirikisha timu nne katika mashindano haya makubwa, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kupata fursa hiyo tunakwenda kutangaza Taifa letu. Wachezaji wetu wanajitangaza, Mbwana Samata Samata alikuwa mchezaji wa Timu ya Taifa kabla hajakwenda TP Mazembe pale na sasa hivi anacheza katika ligi ya nchi ambayo kwa vigezo vya ubora wa soka duniani, Ubelgiji ndiyo timu ya kwanza kwa ubora wa viwango vya *FIFA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna mchezaji anatoka Tanzania Mbwana Samata aliyewahi kukipiga katika Soka la *Simba Sport Club* na baadaye akaenda kule TP Mazembe, huyu ni mchezaji anayecheza ligi katika nchi ambayo kwa viwango ni *FIFA* namba moja duniani. Si jambo dogo na ni mfungaji bora anaongoza ana magoli 21 kwenye ligi, wapo akina Msuva na wapo wengi wanakuja. Kwa hiyo, ushiriki wa timu zetu nne utakwenda kuleta faida kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine nataka kusema tunakwenda kwa sababu Serikali, wadau na sekta binafsi zinashiriki. Jambo langu ambalo nataka kulipendekeza kwa Serikali na hasa kupitia kwa Waziri mhusika hapa ni kwamba tuimarishe sana *Sports Academy.* Watu wote hatuwezi kuwa Wabunge, ma-*engineer*, walimu au kusoma mpaka vyuo vikuu, hizi ni fursa kwa manufaa ya Watanzania. Tujenge *Sports Academy* nyingi na ikiwezekana tujenge *Sports Academy* Kikanda na pale Sengerema tuna uwanja mkubwa sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu nilishamuomba na nishaiomba Serikali, tutakapofikia hatua hiyo kama Serikali itaridhia utaratibu huo, niiombe sana Serikali ije pale Sengerema ijenge *Sports Academy* kwa maana ya Kanda ya Ziwa, tutapeleka zingine Kanda mbalimbali lengo lake ni kujenga fursa kwa ajili ya kuendeleza michezo na ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naishauri Serikali, sasa tunahitaji kufungamanisha sekta ya michezo na hamasa tunayoiona pamoja na uchumi wake. Dunia nzima imeshuhudia na sisi wote ni mashahidi kwamba mataifa makubwa kiuchumi duniani yanawekeza pia katika michezo. Miaka 30 iliyopita Marekani ambalo ni taifa kubwa kiuchumi

duniani lilikuwa halijajielekeza sana katika michezo lakini kuanzia mwaka 1994 waliibuka sasa na kuanza kushiriki Mashindano ya Kombe la Dunia hasa soka na hata michezo mingine. Nachotaka kusema sisi tufungamanishe uchumi wetu, kama tunasema uchumi wetu sasa unakua kwa kasi na tuko katika miongoni mwa nchi tano Afrika ambazo uchumi wake unakua kwa kasi ni lazima i-*reflect* katika kuendeleza sekta za michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia uchumi mkubwa hapa Afrika, South Africa, Nigeria, Egypt, wote wanafanya vizuri katika michezo. Kwa hiyo, tusibaki nyuma katika hilo na sisi ni ma-*giant* watarajiwa katika uchumi wa Afrika, tutumie nafsi hii ku-*link* uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna watu wengi maarufu (*celebrities)*, leo ukingia madukani pale *New York City,* utakuta majina ya Watanzania wamejifungamanisha kupitia shughuli za kibiashara na makampuni makubwa ya *design*. Wapo akina Flaviana Matata, Happiness Magesa (Millen), wapo Watanzania wengi. Leo tunao akina Diamond, Rayvan, Ally Kiba, hawa tunahitaji kuwafungamanisha wakashirikiana na sekta ya utalii naamini kwamba tunaweza kuendeleza vizuri sana sekta ya utalii na kufungua fursa kwa Watanzania wengi na hatimaye tukafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye mafanikio hapakosi *challenges* na nafahamu katika hili yako mambo ambayo tunaweza kufanya vizuri kwa sababu ya hamasa tu. Nataka nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mhamasishaji na Msemaji Mkuu wa *Simba Sports Club,* mtani wetu, Ndugu Haji Sunday Manara, amekuwa ni kigezo ni kielelezo mpaka *FIFA* wamemtambua. Juzi nimeona hata *Instagram* amefikisha *followers* zaidi ya milioni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Simba Sports* kwa miaka imekuwa ndiyo timu pekee ambayo inaujaza Uwanja wa Taifa kwa kuingiza zaidi ya watu 60,000 kwa kiingilio. Maana yake ni nini? Tunahitaji kuhamasishana kama Taifa tusimame pamoja. Nafahamu wako wasemaji wa vilabu vikubwa hapa

Tanzania, wao wanacheza kwenye *Blog* tu, lakini huwezi kuwasikia lakini michezo hii inahitaji kusema na kusikika. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Msemaji wa *Bunge Sports. (Kicheko)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachoomba Watanzania tusimame kwa ujumla wetu, tuhamasishe michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona mahali fulani kwamba baadhi ya mambo yaliyosababisha makusanyo yakawa machache katika Wizara hii ni pamoja na kuonyeshwa michezo hii *live* kwenye *television* na kwenye *App*. Nasema kama Simba waliweza kuujaza uwanja na hii michezo inaonyeshwa kwenye *television* kwa nini tusihamasishane kama Taifa, tutumie hiyo fursa watu kuonyeshwa hii michezo *live* isiwe kigezo cha kupunguza mapato yetu kwa sababu tunao sisi kama Taifa kupitia *Simba Sports Club. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba sana Watanzania tutumie huu uzoefu ambao tumeupata kutoka kwa Msemaji wa *Simba Sports Club*, Ndugu Haji Sunday Manara tuupeleke sasa katika *level* ya kitaifa zaidi. Naamini kwa kufanya vile Taifa litaendelea kunufaika na fursa zinazojitokeza katika michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie jambo moja, tuna *Television* ya Taifa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Khatib Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Angelina Malembeka, Mheshimiwa Devotha Minja ajiandae.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama hapa kuchangia katika hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilimsikia Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Profesa Kabudi akiisifia nchi yetu juu ya mafanikio na sifa waliyoipata duniani kutokana na uhuru wa vyombo vya habari. Juzi alikuwa akizungumza hapa na aliisema nchi yetu kwamba imepokea sifa kwa uhuru wa vyombo vya habari. Moja kati ya eneo alilolizungumzia ni kwamba Tanzania imesifiwa kwa kuwa na idadi kubwa sana ya magazeti. Kwa hiyo, hiyo ilikuwa ni sifa moja kubwa sana kwa Taifa letu, nadhani alikuwa akieleza aliyokutana nayo huko nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku mbili baadaye tumemsikia Msemaji Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo akiyataka magazeti yaliyoripoti taarifa aliyoitoa Kiongozi wa Chama cha *ACT* cha majirani, kwamba waende wajieleza kwa namna walivyochambua taarifa ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo kwa kweli limetupa mashaka. Anakwenda duniani anapata sifa juu ya uhuru wa vyombo vya habari, lakini nyumba yake Serikali, vyombo vya habari kuripoti taarifa ambayo ilitolewa siyo taarifa ya msituni, ni taarifa iliyokuwa *public* na ya wazi ambayo vyombo vya habari wana haki na ni moja katika kutimiza majukumu yao katika kuwaelimisha Watanzania ni nini kimezungumzwa na kiongozi yule wa chama cha siasa. Hilo limekuwa ni kosa; na wenzetu wahariri wa wahabari wanakiwa wajieleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaposifiwa, ni kwa lipi? Tunaporudi, tunafanya nini? Maana inakuwa

hatueleweki. Leo vyombo vya habari vinatakiwa vijieleze kwa kosa lao, lipi? Watu wa habari, wanalipwa mishahara, wanafanya kazi kwa kutengemea habari zinazotoka wawaelimishe Watanzania ni kipi kinachoendelea katika nchi. Inatokea sasa tayari Msemaji Mkuu na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, Dkt. Hassan anavitaka vyombo vya habari vileze hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha zaidi; na Mheshimiwa Waziri naomba unisikilize; yapo mambo ambayo kama Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na wewe Waziri, mngevitaka baadhi ya vyombo vya habari vijieleze, ni muhimu zaidi. Kwa mfano, kuna vigazeti fulani hapa, kimoja kinaitwa Jamvi la Habari na kingine kinaitwa Fahari yetu na kingine kinaitwa *Tanzanite*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vigazeti kazi yake kubwa kuchafua watu, kufitinisha watu, kuleta ugomvi baina ya watu. Mheshimiwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari hajawahi kuviita, hajawahi kuwaita Wahariri wa Magazeti haya akawaambia njooni mjieleze kwa namna namvyowachafua watu. Wamewachafua watu wengine tunaowaheshimu sana ndani ya nchi hii. Mfano, *Comrade* Kinana, huyu mtu muhimu kwenye nchi hii, lakini amechafuliwa na watu hawa, lakini hakuna Mkurugenzi wa la Waziri ambaye amemwita Mhariri wa Gazeti hili, Mkurugenzi wake Musiba mkamwambia ajieleze kwa namna ambavyo anawachafua watu. Kwa nini haitwi? Yuko nyuma ya nani anayejiamini mpaka aweze kumchafua yeyote? Yeyote kwenye nchi hii Musiba akiamua kumchafua anachafua na hakuna lolote linakuwa. Yupo nyuma ya nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani watu kama huyu ndio wangeitwa wakajieleza, wakaelekezwa, *TCRA* wakamwelekeza kama anachofanya sicho, lakini yeye yupo huru. Watu wengine wakitoa kwenye mtandao maoni tofauti kidogo na Serikali, wao wataishia kupelekwa sehemu kushitakiwa na wengine kwenda kufungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa tunafanya nini? Mimi nataka hili lizingatiwe.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. KHATIB S. HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatibu kuna taarifa. Mheshimiwa Mlinga.

**TAARIFA**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Anayoongea Mheshimiwa Khatib ni kweli, ila amesahau kuna kijigazeti kimoja kinaitwa Tanzania Daima na chenyewe kazi yake ni kuchafua Serikali pamoja na watu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatibu Haji, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KHATIB S. HAJI:** *Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wapemba tuna mila moja, yule kijana Bunge lililopita tuliishi na mama yake, kwa hiyo, mimi namchukulia kama mwanangu, siwezi kumjibu. (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib, mama yake alikuwa ameshafariki wakati huo, nadhani una hiyo taarifa. Sasa sijajua umekuwa umeishi naye wakati gani.

Waheshimiwa Wabunge, kuna mambo ambayo mnaweza mkafanya utani na kuna mambo ambayo siyo ya utani. Kwa hekima kabisa na heshima ambayo mnaitwa Waheshimiwa, Mheshimiwa Khatib tafadhali, huyo mama amefariki na ninaamini wewe ni sehemu ya watu ambao umefanya naye kazi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunasikilizana. Hata wewe angekuwa ni mama yako anayezungumziwa hapa ningesema vivyo hivyo ninavyozungumza sasa hivi. Mheshimiwa Khatib, tafadhali mtunzie Marehemu heshima yake.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sikuwa na nia mbaya, lakini kama limekwaza, naomba nifute hilo neno. Naomba kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niendelee na fungu kuhusu mgao wa fungu na fedha zinazotoka *FIFA* kwa Tanzania. Kuna siku nimewahi kuuliza swali; na katika hili Naibu Waziri alinijibu sijui kwa makosa au kwa bahati mbaya; akasema *ZFA* ipo chini ya *TFF,* jambo ambalo siyo kweli. *TFF* ni chombo mbali, Wizara ya Habari na Michezo Zanzibar, ni kitu mbali; na Wizara ya Michezo Bara na *TFF* ni kitu mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *ZFA* ipo Zanzibar chini ya Wizara ya Habari na Michezo Zanzibar na *TFF* ipo hapa chini ya Wizara ya Michezo. Ni vyombo ambavyo havina mwuingiliana wa kisheria wala kikatiba. Hapa linalojitokeza ni kwamba mara nyingi sana tunapolilia juu ya haki ya Zanzabar katika vitu vinavyopatikana ambavyo ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati mwingine tunahisiwa kama sisi ni walalamishi sana, lakini hayo tuliyoyapata na faida zilizotokana na mengine tuliyoyalalamikia, bila shaka kulikuwa na haki ambayo labda ilikuwa imejificha sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kazi yetu moja iliyotuleta hapa Wabunge wa Zanzabar ni kutetea maslahi ya Zanzibar kwenye Muungano. Kama wapo Wabunge wametoka Zanzibar wamekuja hapa, mfano ndungu yangu Ally King, kama yeye amekuja kucheza taarab, atacheza taarab; lakini sisi tuliokuja kutetea maslahi ya Zanzibar, tutatetea maslahi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hakuna mgao halali kutoa fungu la *FIFA*. Mheshimiwa Mwakyembe hili naliomba leo anapohitimisha aliweke wazi, kwa sababu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajumisha nchi mbili; Zanzibar na Tanganyika.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpe taarifa kaka yangu Mheshimiwa Khatib, Mheshimiwa Ali King hakuja Bungeni kucheza taarab, Mheshimiwa Ali King ni Mbunge ambaye kachanguliwa na wananchi wake wa Jimbo la Jang'ombe kuja kuwatetea. Namwomba sana Mheshimiwa Khatib aweze kurekebisha maneno yake ambayo ameyasema na afute kauli yake ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, najua Mheshimiwa Ali King aliletwa hapa kama nilivyoletwa mimi, lakini pia nami nimeletwa hapa kuwakilisha, lakini navuta Mchezo wa Kamba na tunachukua kombe kule Burundi na nchi nyingine tofauti. Kwa hiyo, hii ni michezo na hii michezo imo humu, unakataa nini? Kwa hiyo, kama yeye nyanja yake ni taarab, mimi nipo kwenye kuvuta kamba, timu simika. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili jambo namwomba Mheshimiwa Waziri, hebu akutane na wenzie wa Zanzibar tuone kile kidogo kinachopatikana kutoka *FIFA* na sisi Wazanzibar tunafaidika nacho vipi? Ile ni haki ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo, Watanzania wote wanapaswa kufaidika na mgao ule wa *FIFA* kwa Zanzibar. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Leo hamtanipa nafasi, Pasaka hii. Naomba nimalizie muda wangu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hii itakuwa taarifa ya mwisho kwa Mheshimiwa Khatib, Mheshimwa Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Khatib kwamba *ZFA* ni mwanachama wa *TFF (Tanzania Football Federation)* kama mikoa mingine ya Tanzania ilivyokuwa wanachama. Kila Chama cha Mpira ni mwanachama wa *Tanzania Football Federation;* na vilevile, kwa mfano, naomba nitoe mfano...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mpeni nafasi amalize, Mheshimiwa Zitto naomba ukae, unazifahamu kanuni. Mpeni nafasi amalize, naomba mkae anazungumza. Kaa chini Mheshimiwa Juma tafadhali. Mheshimiwa Khatib, wewe unapewa taarifa, kwa hiyo, kaa utapewa fursa. Wewe kaa, amalize. Mheshimiwa Nyongo...

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mfano mzuri ni kwa *United States of America*. California wana Chama cha Mpira, ukienda Majimbo mengine yote yana Chama cha Mpira; na wote ni Wanachama wa *Football Federation of United of States America.* Kwenda *World Cup* haiendi California, haiendi nchi nyingine, inakwenda *United States of America* na kuna *more than 50 sets of United State of America.* Wasipotoshe wananchi, *ZFA* ni Mwanachama wa *TFF*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshangaa sana. Hayo maandishi umetoa wapi, hata unakuja kusimama hapa unasema *ZFA* ni mwanachama wa *TFF?* Kwanza...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib zungumza name. Nimeuliza swali, unaipokea ama huipokei? Zungumza na Kiti, usizungumze naye. Zungumza nami, atakusikia ukizungumza nami.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipokee nini hapo utumbo huo anaozungumza yule! Mheshimiwa *TFF, TFF...*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib, una uwezo wa kukataa hiyo taarifa bila kuiita majina ambayo unataka kutuaminisha hapa kwamba ndiyo hayo aliyoyasema. Wewe ikatae taarifa yake, endelea na mchango wako, ndiyo kanuni zetu zinavyosema. Sasa hii habari ya nyama, ya utumbo umefanyaje, hebu ondoa hiyo habari ya utumbo hapo. Siyo lugha ya kibunge, ondoa maneno "utumbo" uendelee kuchangia kama umeikata taarifa yake.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakuheshimu sana, mimi nakataa hiyo taarifa yake ni *rubbish* kabisa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

## KUHUSU UTARATIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna kanuni inavunjwa. Mheshimiwa Jenista, kanuni iliyofunjwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu, nakwenda kwenye kanuni ya 64 (1) (b) ambayo inakataza Mbunge ama Wabunge kutokuzungumzia jambo ambalo halipo kwenye mjadala.

Mheshimiwa Naibu Spika ninaanza kuona *sprit* ya majadiliano yetu leo inahama kutoka kwenye hoja iliyopo mezani, sasa watu wanataka kuwachanganya Wabunge na kulichanga Taifa kuhusu Muungano wetu katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, wakati tukiendelea na mjadala huu, Wizara iliyokuwa inashughulika na masuala Muungano tulishaifunga jana. Watu wajikite kwenye maudhui ambayo yanaenda sambamba na Wizara ambayo hoja yale iko mezani, lakini masuala nyeti yanayohusu Muungano naomba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Zitto! Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, masuala yanayohusu tafsiri za Kikatiba kuhusu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano yasiwe ni *part* ya mjadala huu katika siku ya leo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize jambo hili ili kuondoa mkanganyiko wa mtazamo wa Kimuungano katika mjadala unaondelea hapa Bungeni.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Jenista akitukumbusha kwamba kanuni ya 64(1)(a) na (b) na ameweka mazungumzo yake kwa kirefu

na sikusudii kuyarudia; ametupeleaka kwenye fasili ya (b) kwamba Mbunge hatazungumzia jambo ambalo halipo kwenye mjadala.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani hii kanuni ya 64 sote tunaifahamu, kwa hiyo, Mheshimiwa Jenista ametukumbusha. Mheshimiwa Khatib na Waheshimiwa Wabunge wengine waliotoa taarifa na waliochangia tuendelee na mjadala wa Wizara hii kwa yale mambo ambayo yanahusika. Wapo wengine hawajapewa fursa ya kuzungumza, lakini namna wanavyoyazungumza kwa kuwa yale wanayoyasema mengine yanasikika, basi yanaleta upotoshaji kwenye hoja nzima, hata ambayo alikuwa anazungumza Mheshimiwa Khatib. Wakati hoja yenyewe ni ya wazi na imenyooka.

Kwa hiyo, nawaomba Waheshiwa Wabunge tufuate kanuni zetu, mambo yasiyoruhusiwa tusiyafanye. Kwa sasa mjadala ulioko mbele yetu tunaufahamu, ni hoja ya Mheshimiwa Waziri; na yale aliyoyasoma Mheshimiwa Waziri na yaliyosomwa na Kamati ndiyo ambayo tunapaswa kujikita katika hayo ili tutoe maoni katika kuhakikisha tunaboresha ama tunataka Wizara kwenye yale mambo ambayo imeyaleta irekebishe wapi. Ndiyo maana Kamati imetuletea kwenye yale maoni yake.

Kwa hiyo, nawaomba tufuate hiyo kanuni ya 64 tujikite kwenye mjadala hasa kwa kuzingatia maoni....

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** ...ya Kamati ili tutakapokuwa tunasonga mbele tuone wenzetu wametuongoza mambo gani ambayo tunapaswa kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Khatib.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Eeeh, hee!

**KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Najma ukisimama sasa hivi, maana yake mimi ndio nimekosea tena.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA**: Mheshimiwa Naibu Spika, hapana siyo hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Kama hilo siyo lengo lako, inabidi nimpe fursa Mheshimiwa Khatib.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA**: Haya ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaendelea kwa lugha ya upole kabisa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Eeeh!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unipe muda nimalize.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa, alinitaja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali King, kwa kuwa nilikuwa nimeshasema taarifa ya Mheshimiwa Nyongo itakuwa ni ya mwisho kwa Mheshimiwa Khatib, utapewa fursa wakati wa kuchangia. Mheshimiwa Khatib. *(Makofi)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nadhani nitakuwa sijatoka nje ya mada na sitaki kutoka nje ya mada. Hapa nilichokieleza ni kwamba tulikuwa tunalilia lile fungu la mgao unaotoka *FIFA* kwa Zanzibar. Ni

ukweli ambao nitaendelea kuuamini kwamba Zanzibar sio Mwanachama wa *TFF* na Zanzibar ni chombo huru, kipo kiko chini ya Wizara ya Habari kwa Zanzibar.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib, kuna kanuni inavunjwa, Mheshimiwa Najma.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie Kanuni ya 64(1)(a) ambayo hairuhusu humu ndani mtu kuzungumza jambo ambalo si la kweli.

Mheshimia Naibu Spika, Mheshimiwa Nyongo wakati anatoa taarifa alizungumza kauli ambayo inasema kwamba Zanzibar ni sawasawa kama mikoa mingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba tu Mwongozo wako kwamba hili suala aliweke sawa au aondoe kauli yake kwa sababu Zanzibar ndani ya Tanzania ni nchi, nje ya Tanzania ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimetoka kuzungumza hapa na kama kuna mtu mwingine hakumsikia sawasawa Mheshimiwa Nyongo anaweza akapewa fursa ya kuangalia *Hansard.* Amezungumzia chama cha michezo sio Zanzibar kama mkoa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kila mtu ana masikio na amesikia na kwa kawaida walimu wapo wengi sana humu ndani. Kuna watu ambao huwa wana kitu kile ambacho kwa kiingereza kinaitwa *selective listening*, yeye anasikiliza anachotaka kusikia yeye. Kwa hiyo, tuelewane vizuri kwenye hili Mheshimiwa Nyongo hajasema Zanzibar ni

mkoa, amesema chama cha mpira cha Zanzibar ni mwanachama wa *TFF* kama ambavyo vyama vingine. Kwa hiyo...

Mheshimiwa Zitto naomba utupe fursa tafadhali tuendelee na shughuli nyingine.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mimi nampa fursa Mheshimiwa Khatib amalizie mchango wake, mtu yeyote mwenye taabu na mchango wa Mheshimiwa Nyongo ataenda akaisome *Hansard* yale aliyoyasema Mheshimiwa Nyongo. Kwa hiyo, hajaasema Zanzibar ni mkoa, tuelewane vizuri.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib nimeshamjibu Mheshimiwa Najma naomba tusirudi pale, malizia mchango wako.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kosa alilolifanya Nyongo ni kubwa sana, hawezi kuifananisha Zanzibar na mkoa hata siku moja na kama ni mchango bora niishie hapa, haina haja ya kuchangia tena. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip* kabla hujazungumza, Waheshimiwa Wabunge nadhani tunafahamu Kanuni zetu. Jambo linalohusu utaratibu, Kiti kikishatoa Mwongozo, Kanuni zetu zinasema huo ndio Mwongozo wenyewe na tunakwenda hivyo.

Kwa hiyo, tusome Kanuni Waheshimiwa Wabunge, tunakaribia kumaliza Bunge na inasikitisha kwamba mpaka sasa hivi kuna watu hawazijui Kanuni. Mwongozo ukishatolewa na kiti kuhusu jambo la utaratibu ni mwisho wa hilo jambo. Mwenye tabu nao anatumia Kanuni, kupeleka malalamiko yake kwenye Kamati ya Kanuni si zaidi ya hapo.

Kwa hiyo, tusitake kulikuza hili jambo humu ndani, mwenye shida na hilo anapeleka kwenye Kamati ya Kanuni, ndiyo utaratibu wetu. Kwa hiyo, tutaendelea, Mheshimiwa Japhary, tafadhali sana, tafadhali sana.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea sasa, nilikuwa nimekwishawataja wachangiaji, nilimtaja Mheshimiwa Angelina Malembeka, kwamba atafuatiwa na Mheshimiwa Devotha Minja ambaye atachangia kwa dakika tano.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, lakini pia nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya katika sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi za Waziri pamoja na timu yake yote, nichukue nafasi hii pia kutoa pongezi kwa *Taifa Stars, Serengeti Boys, Simba Sports Club, Chimo Olympic Maalum,* Mabondia na timu ya *Bunge Sports* kwa kutuwakilisha vyema katika mashindano mbalimbali yaliyofanyika nje ya nchi. Aidha, nichukie nafasi hii pia kuwapongeza Wabunge wote Wawakilishi wote na Madiwani wote ambao wamekuwa wakiendeleza michezo katika maeneo yao kwa gharama zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sanaa Bagamoyo na Chuo cha Michezo Malya, wanafanya kazi nzuri sana, naomba Wizara isisite kuwapa fedha za kutosha ili waweze kutimiza wajibu wao na kuleta tija kwa malengo yaliyokusudiwa. Sasa hivi tunawasifia wasanii wetu na wanamichezo, lakini wengi wao hawajapita kwenye vyuo, ni vizuri basi vyuo hivyo vitumike vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kuipongeza Taasisi ya Tulia kwa kuanzisha tamasha la ngoma za asili kila mwaka ambapo wameweza kutuletea burudani, kudumisha utamaduni lakini pia kutoa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, msichoke kwa pongezi zangu, niwapongeze pia wasanii wote kwa ujumla. Naomba wasanii wadogo wawe wanaungwa mkono, wengi wao wana kazi nzuri, lakini wanashindwa kutuletea kwa sababu hawana fedha, aidha za kurekodi au kuziendeleza. Sasa ningefikiria itakuwa jambo zuri kama na wao wangeingizwa katika lile kundi la wajasiriamali ili wale wasanii wadogo waweze kurekodi kazi zao na kuweza kutuwasilishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mavazi kwa wasanii wanawake bado halijakaa sawa. Wasanii wanaume bado wanavaa vizuri, wanapendeza lakini wanawake, naona mpaka labda vitu fulani fulani vionekane ndiyo wanaona ngoma inanoga. Hata hivyo, nimpongeze dadayangu Vicky Kamata na dada mmoja anaitwa Siza Mazongela au mama Segere, wanaimba, wanacheza lakini bado wako katika mavazi mazuri ya heshima na wanapendeza. Kwa hiyo, naomba Wizara iendelee kulifanyia kazi suala la mavazi ya wasanii wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niombe wasanii hao wajitahidi sana kutumia ala za asili katika nyimbo zao. Kwa sababu, hasa wasanii wa kizazi kipya, wamekuwa wakitumia sana kompyuta, wakishatengeneza ile mistari yao wanakwenda kwenye kompyuta, sasa unaweza ukamkuta mwimbaji hata ukimpa gitaa, hawezi kutumia. Sasa ni vizuri basi wasanii wetu wawe wanatumia pia na ala za asili na wajitahidi kwenda katika chuo chetu cha sanaa ili waweze kupata mafunzo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la filamu, filamu zetu wasanii wetu wanakwenda vizuri. Kuna tatizo moja katika zile *scripts*, niseme yale maneno ambayo yanapita chini pale wakati picha inaendelea kuangaliwa. Maneno yale naona mengi hayajahakikiwa vizuri, kuna Kiingereza kinachotumika pale nafikiri bado hakijakaa sawa. Aidha *spellings* zimekosewa na matokeo yake yanapoteza maana kabisa, ni vizuri basi ziwe zinapitiwa na kuangaliwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vyombo vya habari, niwashukuru wana habari wote, wanafanya kazi nzuri na wanajitahidi kutuletea habari nzuri na zile mbaya tusizozipenda zote tunazipata. Tunawashukuru sana, lakini sasa kuna suala zima la vijana wabunifu ambao wametengeneza *blogs* zao na wengine wako *online TV*, lakini masuala ya usajili, ada na nini gharama imekuwa kubwa, kwa hiyo, ubunifu wao wanashindwa kuendelea nao wamekaa nao. Tuangalie jinsi gani tunaweza tukawasaidia ili tupate vyombo vingine zaidi vya habari vya kutufanyia kazi na kutupa taarifa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la utamaduni, tusiangalie tu ngoma, tuna suala pia la lugha. Katika suala la lugha matumizi sahihi ya lugha yetu ya Kiswahili ni mazuri zaidi na hili tulichukue hata huku Bungeni, unapomwona Mbunge ambaye ni mzazi na mwenye hadhi ya kitaifa anatamka maneno ya ajabu ajabu ndani ya Bunge, basi ujue huko nyumbani kwake ngoma kubwa. Hii inabidi tujirekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBC* naomba iboreshwe, kama *TBC Taifa,* kuna wakati inatukwaza, tunasema hebu twende kwanza kwenye *TV* hii tuangalie, lakini inafika katikati, picha imeganda, ukienda kwenye *television* nyingine, picha inaendelea. Utakuta saa nyingine hotuba nzuri inayotolewa pale, unataka usikilize hotuba, maneno yameganda. Kwa hiyo, naomba,*TBC* ifanyiwe marekebisho ya kweli ili tunaposema hii *TBC Taifa*, iwe *TBC Taifa* kweli. Marekebisho yanafanywa, lakini sijaona bado, naomba.....

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malembeka kuna taarifa!

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kumpa taarifa kwamba, kuganda kwa picha katika Shirika la Utangazaji la *TBC* ni kutokana na ubovu wa baadhi ya mitambo, vifaa vingi vimechakaa. Kwa hiyo, siyo

tatizo kwa *TBC* bali ni umuhimu kwamba tuweze kutetea ili fedha zaidi ziweze kwenda *TBC.* Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel, nilifikiri hiyo ndiyo hoja yake, kwamba *TBC* iweze kupelekewa vifaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Malembeka unaipokea taarifa hiyo!

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, huyo ni pacha wangu, kwa hiyo, nikiongea na yeye akichangia si mbaya, lakini neno kuboreshwa lina maana sahihi kama alivyozungumza, labda kama anataka uchambuzi tuanze kutoa mojamoja, kitu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nazungumzia hoja yangu ya kuboresha *TBC Taifa,* pia nishukuru *Azam TV* kwa *channel* yake ya Sinema Zetu. Imejitahidi sana kuwachukua wasanii hasa wadogo, tumewaona tulikuwa hatuwajui, tunaangalia picha zile zina maadili mazuri, waendelee hivyo hivyo. Halafu, huo mkakati wao wa kuwasaidia wasanii, basi uende vizuri ili wasanii waweze kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika zangu ni kumi, muda ni mchache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na huu ndiyo utekelezaji wa Ilani ya CCM. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Devotha Minja atafuatiwa na Mheshimiwa Ally King, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kwa dakika tano pia ajiandae. Mheshimiwa Devotha Minja, una dakika tano.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nilimsikiliza Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha taarifa yake, alisema kwamba kwa sasa tuna magazeti 216 na redio 163. Hoja si wingi wa kuwa na *media* nyingi. Hoja, *media* hizi zinafanya kazi kwa uhuru au ndiyo zile ambazo Waziri akiamuka asubuhi anafungia kwa sababu tu hazijaandika habari nzuri za kumpendeza mwenye nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Habari Maelezo hivi sasa imegeuka kama ni kitanzi kwa Waandishi wa Habari. Kazi kubwa ya habari maelezo sasa hivi, ukienda katika *News Media* zote, utakuta kuna mafaili ya maonyo ya kuwaambia kwa nini wasifutiwe, ya kujieleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, habari maelezo badala ya kuwaelekeza vyombo vya habari vifanye nini, Wahariri wafanye nini, sasa hivi imegeuka kama kitanzi kwa ajili ya kuhakikisha inafungia magazeti yoyoteyale ambayo hayaandiki habari nzuri ambazo zinaipendeza Serikali, badala yake yanahangaika na magazeti ambayo yanaandika habari za kuikosoa Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* alizungumza na *Media*, kama haitoshi, Mwenyekiti *ACT* naye akaitisha *media* kwa lengo la kuchambua taarifa ya *CAG*, Dkt. Abasi, anawaandikia wahariri ambao waliandika habari ambazo ni za uchambuzi zilizofanywa na chama cha *ACT*. Haki iko wapi, *CAG* ambaye ndiye aliyekuwa chanzo cha taarifa hizo, asichukuliwe hatua, lakini kwa sababu Zitto ametoa ufafanunzi na waandishi wameandika, basi vyombo hivyo havina mamlaka, vinataka kufungiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuendesha nchi kwa nama hii. Maana yake ni nini, kwamba sasa hata vyama vya upinzani, visifanye *press*, maana yake ni hiyo kwa sababu kama umepewa onyo usifanye *press* za upinzani, maana yake ni kwamba tunataka kuvinyima uhuru vyombo vya habari vifanye kazi za kuchagua, zifanye kazi za Serikali tu peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kulikuwa kuna *defamation* yoyote, ilipaswa, kabisa, angewajibika Zitto na si vyombo vya habari! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya muda, suala la *Bunge Live,* tuliambiwa *Bunge Live* hatuonyeshi kwa sababu wananchi wako *busy* kufanya kazi. Sasa hivi Rais anafanya

ziara, ziko *live*, je, hao wananchi sasa hivi hawafanyi kazi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoyazungumza haya, tunataka kuangalia upande mwingine wa shilingi, lakini kama haitoshi, hata hapa Bungeni tulipo, tukichangia chochote hapa, kinakatwa! Wakati mwingine *clips* za Wabunge hazitolewi kwa wandishi, kwa nini? Tunaogopa nini! Hili Bunge ni huru tumekuja kwa ajili ya kuwawakilisha wananchi, taarifa zinazoandikwa kwa maandishi hazikatwi, lakini ikifika kwenye jambo ambalo tunaikosoa Serikali, *clip* haitaonekana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna haja gani ya kuendelea kuwa na Bunge ambalo, tuna haja gani ya kuendelea kuwa na waandishi ambao wanafanya kazi ya Bunge hapa ambao mwishoni *clips* zote zinafutwa, hakuna kazi iliyofanyika. Hili halikubaliki na tunasema kwa masikitiko makubwa, tuna haki ya kupewa kile tulichochangia hapa. Kama ilivyo upande wa CCM wanapewa na sisi Upinzani tuna haki ya kupewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizungumza kuhusu kufungiwa kwa magazeti, sijui Waziri anatoa wapi mamlaka ya kufungua magazeti. Kwa mujibu wa Sheria ya Habari tuliyoipitisha 2016, hakuna sehemu ambayo inamtaka waziri kufunga magazeti. Anapofanya kosa Mwandishi kama Mwandishi, anawajibika yeye, unapokifungia chombo, kuna wafanyakazi wengine, kuna madereva, kuna wahudumu, kuna watu wengine Waandishi, wanawajibika kwa kosa la moja mmoja, si sawa! Haya ndiyo mambo ambayo tunasema Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Devotha, kengele imeshagonga.

Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe kidogo ili Taarifa Rasmi za Bunge zikae vizuri, mwongozo umeshatolewa na nadhani jana ilikuwa ni mara ya tatu kuhusu jambo hilo hilo la kuhusu Waheshimiwa Wabunge kutokupewa michango yao. Mwongozo umetolewa jana na jana nadhani ilikuwa ni mara ya tatu, likizungumziwa jambo moja hilo hilo, na mimi nataka kuamini Mheshimiwa Devotha Minja unaifahamu hiyo miongozo mitatu iliyotolewa kuhusu Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Ali King, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Joseph Msukuma ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii adhimu ya kuchangia katika Bunge hili. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imegusa katika Kiswahili na ili tuweze kuenzi Kiswahili hiki, nakumbushia, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, wajaribu kutazama michezo ambayo inakuza Kiswahili chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna tabia ya michezo kutafsiriwa, sisi tuna mila zetu na tuna Kiswahili chetu, mchezo kama unatafsiriwa Kiswahili bora ukaonyeshwe huko nchi nyingine ili Kiswahili kienee. Siyo mchezo unatafsriwa Kiswahili hapa kwetu, haiwezi kuchangia kitu. Hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, alisimama hapa mtu mmoja akazungumza Mheshimiwa Khatib, Mheshimiwa Khatib, najua amezungumza hivyo ili anichafulie katika uteuzi katika chama changu. Kwa sababu najua yeye hana wasiwasi kwenye uteuzi, kwa sababu Mheshimiwa Khatibu ni pete na Maalim ni chanda. Kwa hiyo, najua tu kwamba yeye atachaguliwa na hilo jambo linajulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema mimi naimba taarab, ni sawa, na starehe kwa mwenye kuimba, taarab inazungumzia sana mapenzi na mapenzi mara nyingi yanakuwa ni baina ya jinsia mbili, mwanamke na mwanamume, *mwenzangu yeye hana hilo, hata mke hana! Sasa siwezi kujua kwamba yeye ana kitu gani maana...*

*(Kicheko)***[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali King, hayo ya kutokuwa na mke mwachie yeye mwenyewe kama anayo. Kwa hiyo, hebu endelea na mchango wako, ondoa hayo maneno ya yeye kutokuwa na mke. *(Makelele)*

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, na yule aliyesimama namjua vizuri tu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali King, kuna taarifa, Mheshimiwa Juma!

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Ally King ya kistaarabu tu Mheshimiwa ana mke na ana watoto sita, mke wake yuko Tanga, familia yake iko Tanga, kwa hiyo, suala la kwamba Mheshimiwa Khatibu hana mke hili Mheshimiwa Ally King siyo la kweli kabisa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa All King, unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea hii taarifa, *ni sawasawa na mchicha wenye miiba lakini huliwa*! *(Kicheko/Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali King hebu ondoa hayo maneno yako ya mwisho hapo. *(Kicheko)*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, naondoa haya maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye michango ya Bunge hili kama watu watakumbuka hoja ya umeme kwenye

*VAT*, hilo lilizungumzwa, kazungumza Mheshimiwa Saada Mkuya nimezungumza mimi, kule hakujakuwepo mtu hata mchango wake. Hoja ya *VAT* ya bidhaa zinazokwenda Zanzibar, zinazotengenezwa Zanzibar kuja bara, hakuna mbunge aliyeweza kulizungumza hilo nililolizungumza mimi. Sasa hii kupiga makelele, kujikamua na kujidhihirisha ile tabia yake ambayo anayo, hicho siyo kitu ambacho labda kila mmoja anaweza akafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nimshauri tu Mheshimiwa Khatibu, sie tushamjua na vijana huko nje wanapata taabu sana, waosha magari, tunajua! *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba ajaribu kueleza vitu ambavyo viko kweli. Kwenye masuala ya Muungano sisi Wabunge wa CCM ndiyo tuliozungumzia sana, nami nina hoja nyingi sana ambazo nikiziweka hapa mezani, watu watajua nini nimechangia katika Bunge hili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Khatib mimi namwambia hiki kitu aache, mimi muimbaji taarab sawa, lakini yeye asitumie *mic* nyingine atumie *mic* ileile ambayo mimi naimbia taarab. Sasa hii mimi napenda kumwambia kitu hiki. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ninachopenda kuchangia katika Bunge hili, tuanze kuandaa vijana vizuri kwa michezo! Michezo, tukiandaa vijana vizuri, timu zetu zitaenda mbele! Watanzania tutakuwa tuna furaha, tusiwe na *programmes* hizi za zimamoto. Juzi tulifurahi kidogo tatizo tulifungwa na hata siku ile ambayo Simba amefungwa nne, Yanga walifurahi lakini Simba tulinuna, lakini sasa tukiwa na timu zilizoandaliwa itakuwa ni vizuri, kwa nini tusiwe na *academy*. *Academies* zipo lakini za watu binafsi!

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko taasisi zinao uwezo wa kuhamasishwa hata hizi nyingine, zikaandaa hizo *programmes* kwa sababu sasa hivi michezo ni uwekezaji, leo tukiwa tuna wanamichezo 20 wanacheza ligi za nje, watachangia katika mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, Wizara ya Michezo izingatie haya ambayo nimeyazungumza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Msukuma, Mheshimiwa Venance Mwamoto ajiandae.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba iende kwenye rekodi pia, hata kukata hotuba za upinzani ni shambulio dhidi ya uhuru wa habari. Ni kuwazuia wananchi kupata mawazo mbadala yanayotoka upande mwingine. Hii inatuharibu sana kama Taifa. Jana nilikuwa naangalia kipindi cha *The Stream* kwenye *Al-jazeera*, *topic* ilikuwa uhuru wa habari na demokrasia Tanzania. Dunia imeanza kutumulika na tunatia aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee ku-*stress* kwamba, kigezo cha kuwa na magazeti sijui 200 *plus*, kwamba ni uhuru wa habari, hiyo si hoja ni hoja mfu, kwa sababu hatutaki *quality* tunataka *quantity*. Haina maana kuwa na magazeti 216 ambayo waziri au Dkt. Abbasi anaweza akaamuka tu asubuhi kwa *strike* ya *pen* au penseli akayafuta yote kwa dakika moja tukawa tuko tumerudi kwenye *zero*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tatizo la uhuru wa habari katika hii nchi, ni *very serious...*

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antony Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa msemaji kwamba ni kweli kuwa na idadi kubwa ya vyombo vya habari si kigezo peke yake cha kuwa na uhuru wa habari. Hii ni kwa sababu hata kule Zaire wakati Mobutu anatawala na dunia nzima ikipiga kelele

kwamba hakuna demokrasia na uhuru wa habari kulikuwa na vyama vingi vya siasa vikifika 400 kuliko mahali pengine popote duniani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea na ni hatari sana kwa sababu mambo kama haya angalia Zaire walivyofanya na mwisho wao na sasa hivi angalia Sudan na mwisho wa Ali Bashir…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Nakuambia vile. Jana Ali Bashir amehamishwa kutoka *house arrest* alipokuwa amezuiwa amepelekwa kwenye gereza kuu la Khartoum ambako alikuwa anawafunga wapinzani wa kisiasa. *Leaders beware. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana niwapongeze sana *MCT, LHRC* na *THRDC* kwa hatua yao ya kupeleka Mahakamani baadhi ya vifungu vibovu vilivyopitishwa vya Sheria ya Habari ya mwaka 2016. Hawa walienda kwenye Mahakama ya Afrika Mashariki na imetoa hukumu kwamba vifungu vile vinazuia haki ya watu kupata habari au vinazuia uhuru wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tujiulize sisi Wabunge tunakaa humu ndani tunawawakilisha watu, tunatunga sheria inaenda inapingwa Mahakamani halafu inatupiliwa mbali si tunaonekana mapoyoyo. Tunatia aibu kimataifa kwa sababu nchi za *East Africa* zamani zilikuwa zinaiangalia Tanzania kwenye maeneo mbalimbali ya kidemokrasia na kadhalika, Mheshimiwa Kikwete alituweka vizuri sana lakini leo hii Mahakama za nje zinatengua, zinatuambia kwamba Bunge la Tanzania lilitunga sheria ya kukandamiza uhuru wa habari, hawalaumu hata Serikali, sasa hivi vitu ni vibaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mashambulio haya yalianza toka Awamu ya Tano ilivyoingia. Shambulio la kwanza la uhuru wa habari lilikuwa ni kuzuia Bunge *live,* tena nakumbuka Naibu Spika ndiyo ulikuwa umekalia Kiti siku hiyo, nakumbuka vizuri sana. Sasa unazuia Bunge *live* kwamba watu wafanye kazi lakini leo Mkuu kila siku yuko kwenye *TV* asubuhi, mchana, jioni, usiku mbaya zaidi unakuta Wakuu wote wa Taasisi za...

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, kuna kanuni inavunjwa, Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu, ninazo Kanuni mbili ambazo Mheshimiwa Mbunge mchangiaji anakokwenda anakwenda kuzivunja. Kanuni ya kwanza ni Kanuni ya 53(8), inasema, Mbunge yeyote hataruhusiwa kufufua jambo lolote ambalo Bunge lilikwishakuliamulia katika Mkutano huu uliopo ama mikutano iliyokwishakupita. Hiyo ni kanuni ya kwanza ambapo anapoendelea kuzungumza na kuchangia Mheshimiwa Mbunge maamuzi yote ya Bunge *live* na taratibu nyingine zote zilishafanyiwa maamuzi kwenye mikutano iliyopita na jambo hili lilikwishaondolewa katika mijadala yetu kwa kuwa lilishafanyiwa maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Kanuni nyingine aidha wewe ulikaa kwenye Kiti ama hukukaa kwenye Kiti lakini Bunge lilishakwishafanya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni nyingine tunaposhughulikia masuala ya utendaji kazi wa Mheshimiwa Rais, kwanza yanasimamiwa na Katiba kama Kiongozi Mkuu wa nchi inamlinda kufanya kazi kwa sheria ambazo zinatumika kusimamia utendaji kazi na mwenendo wa Rais.

Kwa hiyo, suala la kujadili mwenendo wa shughuli Rais kwa mujibu wa Katiba, hata akitaka kuwa na TV, akitaka kutangazwa saa 24, hili siyo suala la Bunge ni la Kikatiba na la mhimili wa Urais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye Kanuni yetu ya 64(1)(e) inatukataza pia kuzungumzia mwenendo na utendaji kazi wa viongozi wanaotoa maamuzi na mwenendo hasa wa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, kama mchangiaji ana hoja kuhusu vyombo na uhuru wa habari, uhuru wa habari huo usimwingize Mheshimiwa Rais katika utendaji wake wa kazi kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa Kanuni tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nirudi kusema Kanuni ya 53(8) ni lazima Waheshimiwa Wabunge yale ambayo yalikwishakufanyiwa maamuzi hayatakiwi kuwa tena ni *part* ya mjadala mpya ndani ya Bunge letu.

Mheshmiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Jenista akiomba kuhusu utaratibu wa Kiti kwa Kanuni ambazo amezirejea kwamba zilikuwa zinavunjwa. Ameanza na Kanuni ya 53(8) inayozungumzia kuhusu jambo ambalo lilikwishaamuliwa na Bunge katika mikutano iliyokwisha ama katika mkutano huo unaohusika. Pia ametupeleka kwenye Kanuni ya 64(1)(e) inayokataza kuzungumzia mwenendo wa Rais.

Waheshimiwa Wabunge, sikusudii kurejea kwenye mchango wa Mheshimiwa Mbilinyi na ambao Mheshimiwa Jenista ameona kwamba unazigusa hizi Kanuni mbili. Huwa siku zote tunakumbushana kufuata utaratibu ule ambao tumejiwekea wenyewe kwa ajili ya majadiliano humu ndani.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 53 inakataza kuzungumzia jambo ambalo lilikuwa limekwishaamuliwa isipokuwa kama unaleta hoja mahsusi ili Bunge liweze

kuliangalia upya jambo ambalo liliamuliwa. Jambo ambalo kwa sasa hivi hakuna hoja inayozungumzia Bunge kuliangalia upya jambo ambalo lilikwishaamuliwa. Nadhani kwenye hilo linazungumzia maelezo ya Mheshimiwa Mbilinyi kuhusu uamuzi si hata wa Bunge, uamuzi wa Serikali kutokuonesha tena moja kwa moja mijadala inayoendelea Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kama Bunge lilihojiwa kuhusu jambo hilo ilikuwa ni hoja ambayo ililetwa ili Bunge lifanye maamuzi. Kwa sababu ililishapita ni vizuri kuzingatia masharti ya Kanuni zetu. Kama jambo hilo bado linaleta tabu miaka mitatu au minne baada ya uamuzi huo, Kanuni zetu zinatoa fursa kwa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ama mtu mwingine yeyote kufanya hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 64 kuhusu mchango wa Mheshimiwa Mbilinyi pia ambao Mheshimiwa Jenista ametupeleka kwenye fasili ya (1)(e) kutokuzungumzia mwenendo wa Rais. Ni vizuri kukumbushana kwamba Kanuni hii inazungumzia mambo yasiyoruhusiwa Bungeni na hilo ni mojawapo isipokuwa ikiwa hoja iliyoko Mezani imeletwa mahsusi kwa ajili ya kuzungumzia mwenendo wa Rais, jambo ambalo silo lililoko Mezani sasa. Kwa hiyo, niwaombe tuzingatie Kanuni zetu tulizojiwekea ili majadiliano yetu yawe yanaenda vizuri bila kukatisha kila wakati kwa kuvunja hizi Kanuni.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbilinyi utakuwa umepata mwongozo wa mambo haya yote mawili katika dakika zako zilizobaki uendelee kuchangia hoja iliyoko Mezani na siyo hoja ambayo kwanza ilifanyiwa maamuzi lakini pili usizungumzie mwenendo wa Rais ama mtu mwingine yeyote ambaye siyo hoja iliyoko mezani sasa. Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachogundua watu wamejaa hofu na kujipendekeza, mimi hakuna sehemu hata tukienda kwenye *Hansard* nimesema Rais, nimesema Mkuu. Sasa haya ndiyo mambo tunayosema mnajiongeza mpaka mnaharibu mpaka Rais anawaambiwa kwamba Watanzania siyo wajinga kwa sababu hata hili

watalifuatilia kwenye mitandao na watajua tofauti yangu na yenu katika hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia jambo mnaweza mkawa mmesema ninyi humu ndani kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sugu, kwani Mkuu ni nani? Ni Mheshimiwa Mbowe?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizngumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Siyo nikija Mbeya tu hata sehemu nyingine lakini usiendeleze jambo ambalo nimekwishalitolea ufafanuzi hapa mbele. Malizia mchango wako ukiwa umeondoa hayo ambayo tumesema yanavunja Kanuni.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Katibu, dakika ngapi zimebaki nijue kabisa?

**NAIBU SPIKA:** Huwezi kumwongelesha Katibu Mheshimiwa Mbilinyi, wewe si ni Mbunge mzoevu, wewe mwenyewe umesimama kwa kuwa mimi nimekuruhusu ili uzungumze. Unapomuuliza Katibu yeye anazungumza humu ndani? Mheshimiwa Mbilinyi, tafadhali.

**MBUNGE FULANI:** Maliziamalizia Jimbo la Mbeya linaondoka hilo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, unajua mimi nawaambia, *don't go personal on me, I am just doing the job for this country.* Tukiendelea hivi tunakubali kuingizwa kwenye giza, tutajikuta kama North Korea ambapo wameelekezwa mpaka namna ya kupiga makofi. Nchi nzima wanatakiwa kupiga makofi kwa inchi tatu, kutoka hapa kuja hapa, paa, paa, paa, sasa mnataka hili Taifa lifike huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajizuia kwenye kila eneo la uwazi, hebu angalia hivi ni sababu gani iliyofanya tujitoe *OGP (Open Government Partnership),* huu mkataba wa

kimataifa? Mkataba huu unataka nchi wanachama kukuza uwazi katika uwajibikaji na utendaji wa Serikali. Serikali hii inajinasibu kwamba inapenda uwazi, inataka kila kitu kiwe wazi, kwa nini sasa tunajitoa katika vyombo ambavyo vinatu-*endorse* kwamba sisi ni watu ambao tunataka uwazi. Halafu tukisema mnatutafutia mbinu mbadala, mnatuvizia, matokeo yake mnaleta Taifa katika mtanziko mkubwa kwa kufanya mambo bila kushirikisha Wabunge kama mlivyofanya kwenye vitambulisho vya wajasiriamali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mmekaa huko wenyewe, mmepeana vitambulisho, Mbeya Mjini mmeleta vitambulisho 45,000 wakati Wamachinga hawafiki hata 3,000. Watendaji wanalia kule na kwa sababu hawana uwazi hawawezi kutoka na kuitisha *press* kusema hiki kitu hakiwezekani wanalia chinichini, huku ndiko mnakolipeleka Taifa. Uhuru wa habari, uhuru wa kupata taarifa, uhuru wa kutoa taarifa hakuna, wanabaki kunong'ona tu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiriakwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi, muda wako umekwisha.

*(Hapa Mhe. Joseph O. Mbilinyi aliendelea kuongea bila kutumia kipaza sauti)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hajasimama Mheshimiwa Mwamoto, niwakumbushe tu umezuka utaratibu ambao vitu ambavyo vinatoka, kama hivi hapa nimezima kisemeo lakini Mheshimiwa Mbilinyi anaendelea kuzungumza halafu yeye mwenyewe ama rafiki yake ama jirani yake anachukua maneno hayo kana kwamba ni mchango wake Bungeni wakati yeye ameshakatwa. Mzifahamu vizuri Kanuni zetu, jambo hilo haliruhusiwi kwa sababu si mchango uliotoka Bungeni, ninyi mnaendelea kuzungumza huku umeshakatazwa unatoa hiyo habari nje kana kwamba ni mchango wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Salome, nimekusikia muda mrefu na nimekustahi, usifikiri sijakuona ama sikufahamu jina, tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tafadhalini sana tufuate utaratibu tuliojiwekea wenyewe.

Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Venance Mwamoto.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwa hotuba yake nzuri na pia taarifa ya Kamati. Nimwambie Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wamefanya vizuri sana kwenye tasnia ya muziki. Watanzania wengi tunawaelewa na tunaamini mnawasimamia vizuri vijana na tunapata burudani za kutosha ikiwemo na hii aliyomaliza kuitoa msanii mkubwa nguli Sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitazungumzia sana kipande cha wasanii kwa sababu nimejaribu kumsikiliza Mheshimiwa Sugu kama msanii mkubwa nilitegemea atazungumza matatizo makubwa ya wasanii badala yake Mheshimiwa Sugu leo kageuka kuwa mwanasheria kuzungumzia mambo ya magazeti na vitu vingine.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wasanii wa muziki kwa nini wanafanikiwa? Wanafanikiwa kwa sababu hawategemei kuuza filamu, wanapotoa nyimbo zao wanachokitegemea wao ni kufanya matamasha na kukodiwa na kuchukua viingilio. Ni lazima Wizara ione huruma kwenye tasnia ya filamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kuangalia kwenye kitabu hiki mipango ya Bodi ya Filamu siamini kama

watu waliotengeneza hiki kitabu ni hawa wanaosimamia tasnia ya filamu. Tasnia ya filamu iko hoi bin taaban na ndiyo maana unakuta wasanii wetu wa Bongo Movie hawana kitu, sasa hivi wanategemea misiba wapate michango na kufungua madanguro na kuwa makuadi kwa wanaume. Wako hoi bin taaban, kwa nini? Tumeruhusu vitu vya kijinga ambavyo vimekuja kuuwa kabisa tasnia ya filamu na filamu ndiyo sehemu kubwa ambayo sisi Watanzania ilikuwa inatupa mafunzo ya utamaduni wetu wa kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kuna filamu inaitwa Sultan hakuna Mtanzania ambaye haiangalii na mbaya zaidi imetafsiriwa Kiswahili. Hivi ni nani anaweza kwenda kumuangalia Marehemu Majuto akaacha kwenda kuangalia Sultan? Tunapata faida gani kwenda kuzungumza mambo ya Waturuki tunaacha kukuza utamaduni wetu wa ndani? Hakuna Mtanzania anayeangalia *Bongo Movie* leo hayupo na hawa hawa watu wanaotafsiri Kiswahili ni wasanii wanatulipa nini kama Serikali? Kwa hiyo, nimwombe Waziri anusuru wasanii wa Tanzania wanamfia mikononi mwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ukitengeneza filamu ya Kibongo ina ukaguzi zaidi ya 1,000 lakini zikija filamu za Kikorea hakuna ukaguzi, nani atakayeenda kuangalia sinema ambayo mmewaambia Watanzania wavae madera na kanzu wakati filamu za Kikorea watu wamepiga *miniskirt* lazima watu wataenda kwenye *miniskirt*. Kwa hiyo, niombe sana kama tunaweka ukaguzi wa filamu lazima na filamu zinazotoka nje zikaguliwe ziendane na maadili yetu ya Kitanzania *otherwise* wasanii wetu wa Kitanzania wote tunaenda kuwapoteza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitengeneza filamu ya Tanzania unapoitoa inabidi ulipe kodi, mfano iwe shilingi milioni moja na mwakani lazima uilipie shilingi milioni 1, hii kitu siyo sawa. Filamu inaangaliwa mara moja inachuja lakini wewe unamweka kwenye *library* yako kumtoza shilingi milioni moja kila mwaka. Wasanii wetu wamekata tamaa na Mheshimiwa Waziri naomba sana uitumie kauli ya Mheshimiwa Rais kwamba chukua maamuzi ya kusafisha hiyo

Bodi ya Filamu, wametuulia filamu yetu ya Kibongo na ukitaka nikutajie hata majina ya wanaouwa nitakueleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wako vinara Tanzania Bodi ya Filamu inawafahamu wako Kariakoo, hawa watu wanaleta makontena na makontena ya *dublicate* kazi za Watanzania. Hata Waziri unawafahamu ukitaka nikutajie kwa ruhusa yako nakutajia. Hawakamatiki, wanatengeneza *dublicate* ya kazi za Kitanzania wanazileta kama *export* wanazipeleka Kongo na Kenya. Ukifika Kongo leo filamu ya Tanzania inauzwashilingi 500, hivi ni nani atakayeweza kufanya kazi ya kutengeneza filamu hapa Tanzania? Makontena yanaingia kutoka Korea, China na wanaoyaleta wanafahamika. Hata wakikamatwa na hizo *dublicate* faini yake ni shilingi milioni tano, mtu ana mzigo wa bilioni kumi na makontena yake anarudishiwa. Ni nani atakayeangalia kazi za wasanii wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wewe unatokana na CCM hawa wasanii ni watu wakubwa sana kuanzia mwaka huu mwezi Novemba kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa tutawatumia, mwakani tutawatumia, tusipowasaidia hawa wakipotea tutakuja kuchaguana watu wenye sauti nzuri humu tutageuka wasanii na kufurahisha kwenye majukwaa wakati wa uchaguzi. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, mimi nalalamika na wewe na nakueleza vizuri kwamba shughulika na wasanii wa Bongo *Movie* wamepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukiingia Sinza madanguro makubwa yote ni ya wasanii. Ukitokea msiba, watu wanaokwenda kusimamia michango ni wasanii angalau wapige ganji wapate kitu. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, usiopochukua hatua kwenye hili, nami natarajia kuja kushika shilingi, uhakikishe kwamba unanifuata hapa tuongee unieleweshe vizuri vinginevyo nitalia na wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yanayozungumzwa humu tunakoelekea yatatokea tu, kwa sababu hakuna cha kuzungumza. Sera ya Chama cha Upinzani ilikuwa ni kukosoa;

na kweli walikuwa na sababu za msingi, mimi nilikuwa shabiki wao kuwaangalia. Walikuwa wanasema Tanzania hatuna ndege; haya mambo yametengenezwa yote. Sasa hawana cha kuzungumza. Mbunge anasimama anakwambia unaenda na ving'ora. Hiyo ndiyo kazi wamemtuma watu wa Mbeya, wala tusishangae, hakuna kitu cha kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anasimama hapa kwa mujibu wa kitabu chetu tumegaiwa hapa, unamwambia badilisha, anasusa kusoma taarifa nzima ya Kambi ya Upinzani, halafu na wenyewe wanampigia makofi. Naamini ukitamka neno baya kwa mwenzio, utegemee linakurudi wewe. Humu ndani tuliitwa mboyoyo, lakini tumeona leo mboyoyo ni nani; mtu anaacha kusoma taarifa ya Kambi ya Upinzani, watu wanampigia makofi. Kwa hiyo, mboyoyo wanaeleweka kwenye hili Bunge. *(Makofi)*

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Jimbo la Mbeya linaondoka, Jimbo la Mbeya.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Basi kwa vile amemaliza, nilikuwa nataka nimwambie...

**NAIBU SPIKA:** Ameshamaliza, kwa hiyo, hawezi kupewa taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Tunza Malapo, naomba ukae. Mheshimiwa Haonga! Wabunge muwe mnasikiliza, kwa nini mnakuwa na

haraka na jambo? Kwa nini msisikilize? Kwa nini usisikilize nataka kusema nini?

Kanuni zetu zinatoa utaratibu; mtu anapopewa taarifa, lazima awe anazungumza ili nimkalishe chini. Kama unaona kuna shida katika mchango wake, soma Kanuni, unayo nakala hapo, tumia kanuni nyingine. Sasa unataka utumie kanuni ya taarifa wakati kanuni imekaa vizuri taarifa inatolewa wakati gani? Msifanye mambo kana kwamba Bunge limeanza jana, tumeanza siku nyingi, mnapaswa kuzijua Kanuni.

Mheshimiwa Venance Methusalah Mwamoto, atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii niweze kukushukuru kwa niaba ya *Bunge Sports Club,* nami mwenyewe. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya na kutusaidia kupelekea timu zetu nyingi kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kuchangia, nitajielekeza zaidi kwenye ushauri kuhusu michezo. Tulikuwa na mfumo mzuri sana wa kuwapata wachezaji kwenye timu zetu za Taifa toka zamani. Tulikuwa tuna michezo ya UMISETA, UMISHUMTA, SHIMUTA, michezo ya majeshi na michezo mingine. Huko ndiko ambako timu zetu za Taifa zilikuwa zinapatikana na ndizo *academy* zetu zilikuwa, lakini leo hivi vyote havipo, tumeua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ule uwezekano wa kupata timu nzuri umeanza kuwa shida. Kwa sababu ukiangalia pamoja na kuwa tumefanya vizuri kwenye Timu ya Taifa ambayo bahati mbaya jana na juzi imefungwa, jinsi walivyopatikana wachezaji inaonesha kabisa bado mfumo siyo mzuri, kwa sababu wale wachezaji wamepatikana kwenye *academy.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika wachezaji ambao wako kwenye timu ya Taifa ile ya vijana; ni vijana wanane wanatoka kwenye Shule ya *Alliance,* Mwanza. Kwa hiyo, tungekuwa na *academy* au tungekuwa na michezo mingine mingi, maana yake tungepata wachezaji kutoka nchi nzima, lakini leo wanatoka sehemu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naweza kusema kwamba hatuwezi kuwa na timu nzuri ya Taifa. Kwa hiyo, naomba, tuangalie ni mfumo gani sasa Serikali itaingia nao ili kushirikisha vijana wetu toka wadogo na wa kati mpaka kupata wanamichezo wazuri. Michezo yote; ukiangalia kwenye riadha sasa hivi *the way* jinsi ambavyo wanapatikana ni kubahatisha, lakini zamani ilikuwa unawapata kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali itoke iangalie ni mfumo gani ambao tunaweza tukatoka nao. Kwa sababu ukisema *academy* ni gharama na siyo rahisi ukawa na *academy* nchi nzima, lakini kuna vitu ambavyo tukikaa na kubuni vinaweza vikatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nichangie tena kitu kingine ambacho nimekuwa nikisema siku zote, *TFF* bahati nzuri wapo. Niliwahi kusema kwamba Uingereza naweza kusema ndiyo nchi yenye ligi bora, lakini Timu ya Taifa ya Uingereza siku zote siyo nzuri kwa sababu ya utitiri wa wageni. Kwa hiyo, Tanzania, sipingi sana, mwanzo nilipendekeza kwamba tupunguze idadi ya wageni kwenye timu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kinachosikitisha zaidi ni kwamba bidhaa zinapoletwa Tanzania zinakaguliwa, kuna chombo kabisa kimeundwa kwa ajili ya kukagua zile bidhaa ambazo zinaingia nchini, zile ambazo zinakuwa siyo bora zinateketezwa. Wachezaji wanaotoka nje kuja kucheza Tanzania leo hawana ubora. Kwa hiyo, Watanzania hakuna wanachojifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bado narudi kusema hivi, tuweke sheria kama nchi nyingine wanavyofanya, kwamba mchezaji anapokuja kuchezea

kwenye nchi yetu, lazima angalau awe anachezea Timu ya Taifa kwenye nchi yao. Leo wachezaji wanaokuja kuletwa hapa ni wachezaji ambao kule wameshindikana, hawachezi; wakija hapa ni majeruhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia upande wa Simba, kuna wachezaji wawili au watatu; Kagere, Okwi labda na Chama. Ukija upande wetu wa Yanga, unamkuta yuko mmoja tu pale, sasa wengine hata benchi hawakai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri hebu *TFF* mtusaidie ili tuweze kuboresha timu zetu za Taifa. Bila kufanya hivyo, hatutakuwa na Timu ya Taifa nzuri hata siku moja. Tutakuwa tunaendelea tu kuzifurahisha Simba na Yanga, Azam lakini Watanzania watakuwa wanaendelea kukasirika kwa timu yao ya Taifa. Kwa hiyo, naomba tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia wenzetu juzi kwenye benchi la ufundi la Timu ya Taifa ya Nigeria, pale kwenye benchi la ufundi kulikuwa kuna wachezaji ambao walicheza *Olympic* mwaka 1996 alikuwepo mtu anaitwa *Mateo Atepigu na Peter Lufly* walikuwa kwenye benchi la ufundi, lakini ukiangalia Timu yetu ya Taifa kocha umri wake analingana karibu sawa na wale vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu huwa kwenye timu ya vijana wanaweka mtu ambaye ana umri mkubwa kwa ajili ya kuwalea kama watoto wake, watamwelewa. Sasa unaweka kijana ambaye ana umri unafanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ahadi. Wale watoto ni wadogo unapomwahidi gari, unaahidi fedha nyingi, wale watoto wanachanganyikiwa. Afadhali tungewaahidi basi kwamba utasomeshwa, nakadhalika. Ukiangalia kwenye Timu ya Nigeria wachezaji wanane wanacheza nje *professional,* lakini  wa kwetu wale kama unavyoona. Kwa hiyo, hatulaumu, lakini tulipofikia siyo pabaya isipokuwa tujirekebishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mashindano mengine yanakuja. Kuna Mashindano ya Walemavu ya Afrika Mashariki, tunapata heshima tena kama ambayo tumeipata hii. Kwa hiyo, kwa sababu tunapata hiyo heshima, haya ambayo yanaendelea siyo rahisi tena kushinda, tukishinda basi Mungu atakuwa ametusaidia, lakini yanakuja ya walemavu. Afrika Mashariki tumepata heshima hiyo tena na wanatupa heshima hiyo kwa sababu ya amani na usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, Mheshimiwa Mwakyembe, tusiende kama tulivyokwenda ile, kwa sababu ile timu ndogo Taifa maandalizi ya *AFCON* yalikuwa siyo mazuri. Wenzetu walianza miaka mitatu kuziandaa hizi timu, sisi tumefanya miezi sita au mitatu tu. Kwa hiyo, hii timu ya walemavu angalia, inaitwa *Tembo Warriors*, tuangalie jinsi ya kuwasaidia sasa angalau tutoke na hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vijana wenye mtindio wa ubongo hapa, wamechukua dhahabu kadhaa. Wale wazima wanashindwa kutuletea chochote; tuendelee basi tuwasaidie hawa wenzetu ambao wana uwezo. Kama hawa wenye mtindio wa ubongo na walemavu wengine ambao tuna uhakika wanaweza kufanya vizuri, michezo mingine imetushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TBC,* namwomba ndugu yangu, Mkurugenzi, rafiki yangu, kuna hawa wenzetu wenye ulemavu wa usikivu, kuna mtu ambaye anatakiwa apewe kazi pale kwa ajili ya kutafsiri alama zile ili wapate haki ya habari na wenyewe. Ni muda mrefu toka tumeomba, lakini bado hajaajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hebu tuwatendee haki ili tuweze…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, lakini usikivu pia *TBC* kule Nkasi na Kibondo bado siyo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cosato David Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi. Nianze kwa pongezi kwa hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri. Pia niipongeze kama walivyosema wenzangu wengine; Mheshimiwa Mwamoto, na Mheshimiwa Ngeleja, kwamba umekuwa ni mwaka wenye mafanikio katika soka letu na katika michezo kwa ujumla. Tukianza na *Taifa Stars* kufuzu kwenda *AFCON,* hatujawahi kufanya hivyo karibu miaka 40. Ni jambo la kujipongeza na sasa tuelekeze nguvu katika maandalizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vile haitoshi, tumekuwa waandaaji wa *Under Seventeen* ya *AFCON.* Ile kuandaa, pamoja na matokeo ambayo hayaridhishi katika Timu yetu ya Serengeti, lakini kule kuweza kuandaa mashindano haya maana yake ni kwamba kama tunavyosema michezo ni ajira, michezo ni biashara, wakati ujao tunaweza tukaandaa pia mashindano makubwa zaidi. Kwa hiyo, ni kama *lesson* ya sisi kujiandaa katika kufanya maandalizi ya kufanya mashindano haya makubwa ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitakuwa siyo mwingi wa fadhila kama sitapongeza *Bunge Sports Club*, tulikwenda pale Burundi wote kuanzia wavuta kamba, soka, riadha, wavu na *netball*. Kwa kweli kwa sababu mimi nacheza soka kama kiungo mchezeshaji, napenda pia kutoa pongezi za pekee kwa Walimu wetu Mheshimiwa Venance Mwamoto na Mheshimiwa Ahmed Ngwali, walitufundisha na tulicheza mchezo wa kuvutia mpaka walikuwa wanashangaa, ninyi kweli ni Wabunge? Kwa hiyo, pongezi sana kwao na kwa

timu nzima ya *Bunge Sports Club,* lakini kwa uongozi mzima kuanzia Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Sekretarieti kwa maana ya Katibu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima niseme kuhusu *Simba Sports Club,* wamefika robo fainali, ni hatua kubwa katika mashindano ya Vilabu katika Bara la Afrika, nayo imetusaidia sisi kutubeba kama ambavyo wamesema wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo mara zote nimesema michezo inaenda na hamasa. Pia nitakuwa siyo mwingi wa fadhila nisipowataja baadhi ya wasemaji wa Vilabu ambao kwa kweli wanatia chachu na hamasa kubwa sana. Mtu kama Masau Bwire, nadhani kuna watu hawamjui kwa sura lakini wanamjua kwa kumsikia; mtu kama Thobias Kifaru wa Mtibwa, Masau Bwire yuko Ruvu; mtu kama Haji Manara; watu kama kina Jafar Idd Maganga; watu hawa wanaleta hamasa ya kuwezesha watu kwenda viwanjani, lakini kama ambavyo tuliona tulipokwenda Burundi, Bunge tulikuwa kitu kimoja. Michezo inaweza kuleta umoja, michezo inaweza kuleta mshikamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema pongezi hizi, niseme kwamba michezo, sanaa na burudani ni biashara. Kwa takwimu nilizonazo, nchi kama kama Nigeria na Marekani, yaani baada ya ajira inayotolewa na Serikali, inayofuatia ni ile inayotolewa na Sekta ya Michezo, Sanaa na Burudani. Watafiti wamekadiria kwamba, kufikia mwaka 2020, mapato katika Sekta hizi za Michezo, Sanaa na Burudani yatafikia shilingi trilioni 2.2 dola za Kimarekani. Unaweza ukaona ni fedha kiasi gani. Kwa hiyo, nasi hapa nchini ili tuweze kunufaika, vyombo vinavyohusika kama walivyosema wenzangu, viweze kusimamia ipasavyo kutengeneza mazingira bora ili sanaa, michezo na burudani iweze kuwa chanzo cha mapato lakini kama ambavyo sasa ni chanzo cha ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo hivi ni pamoja na *BASATA*, *TFF*, Bodi ya Filamu, Shirikisho la Riadha na kadhalika,

wajielekze kutengeneza mazingira bora ya kuvutia pia hata wadhamini. Kwa sababu, kwa mfano mchezo wa soka leo hii hatujapata wadhamini kwenye ligi kuu yetu. Kwa sababu gani? Inawezekana mdhamini anakuja mahali ambapo anaona kuna umakini na usimamizi bora. Leo hii ligi yetu ukianzia waamuzi, ni mambo ambayo kwa kweli yako shaghalabaghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliendа kuangalia mchezo wa Panama na Baobab hapa katika uwanja wa Jamhuri, hakuna hata huduma ya kwanza. Kuna mambo yanahitaji fedha. Mchezaji kaumia, nimeona amebebwa mgongoni. Kuna mambo ni *management*, ni usimamizi tu wa kawaida ambao unaongea na Mganga Mkuu wa eneo husika, tunaomba huduma ya kwanza, anawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bila kuwa na usimamizi ambao ni madhubuti katika michezo, naamini kabisa hatuwezi kuvutia wadhamini; na ile dhana ya kwamba michezo, sanaa na burudani ni sehemu ya ajira na ni chanzo cha mapato, hatutaweza kuifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati tunajielekeza kutafuta fedha, lakini wale wanaohusika na dhamana ya michezo tuhakikishe kwamba tunasimamia kwa ufasaha ili kusudi makampuni yaweze kuwekeza fedha zao. Leo hii tunapozungumza ligi kama ya Uingereza, *Champions Leage,* inakuwa na mvuto. Wadhamini wanapigana vikumbo kutia fedha zao, kwa sababu iko *well organized*. Kwa hiyo, kuna mambo yanataka tu usimamizi, kuna mambo tu yanataka *management*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, nami nimpongeze pia mwamuzi pekee anayechezesha kwenye *AFCON* ambaye ni mwana mama Jonesia Rukyaa Kabakama. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule *AFCON* Mheshimiwa Waziri kati ya waamuzi 56, hakuna hata mmoja ambaye anatoka Tanzania. Hii nayo ni sekta ambayo tunatakiwa

kuiangalia, tulee waamuzi, tuwasaidie, walipwe vizuri. Kwa sababu kama tunasema ni chanzo cha ajiria, pia tunapopata waamuzi wanaokwenda kuchezesha michezo ya Kimataifa, kwanza tunatangaza Taifa letu, lakini wanachopata wanakuja kuwekeza hapa nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, nami naomba kuunga mkono hoja. Naomba tujielekeze sasa kuishangilia Serengeti. Pamoja na yanayotukuta, lakini tusikate tamaa, hakuna mwanzo mwepesi, mwanzo daima ni mgumu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana kwa michango yenu. Kuna mambo mawili halafu nina tangazo hapa.

Mheshimiwa Waziri kuna mchango ulitoka hapa na ninaamini utakapopewa fursa ya kuhitimisha hoja yako utaliweka jambo hili vizuri. Umekuja mchango kuhusu wasanii kuwa ndio wenye umiliki wa madanguro mengi ikitajwa Dar es Salaam. Nadhani hili Mheshimiwa mwenye hoja utakuja uliweke hili vizuri, halitakuwa ni jambo jema kama halina ukweli wowote kuwadhalilisha wasanii wetu.

Jambo lingine ni kuhusu ushiriki wa wasanii kwenye misiba na kwamba wanakusanya michango na wanaweza aidha kuitumia hiyo michango siyo kwa makusudi yale ambayo wamekusanya. Mambo hayo mawili yanawaweka wasanii wetu katika mazingira ambayo siyo mazuri. Kwa hiyo, naamini mtakuwa mmelipata wakati wa mchango na mtaweza kulitolea ufafanuzi wakati mkifafanua hoja nyingine mtakapokuja hapa.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo hapa ambalo linatoka kwa Mheshimwa Mwamoto na linamhusu msanii wetu Banana Zorro, kwamba siku ya leo tarehe 18 Aprili, 2019 saa mbili usiku atakuwa akizindua wimbo wake mpya *New Club Seven*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa sana kwenye kumuunga mkono msanii huyu ambaye anatarajia kuzindua wimbo wake na mmeambiwa itakuwa saa mbili usiku leo tarehe 18 na mnakaribishwa sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka siku ya tarehe 23 Jumanne, saa tatu asubuhi.

*(Saa 6.56 Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 23 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*